ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
4.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
5.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
6.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
7.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni.
8.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.
9.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo La Kwamtipura.
10.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.

11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
12.Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
15.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
16.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
18.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
19.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.
20.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
21.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.
22. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.

23. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.
24. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
25.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
26.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
27.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
28.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake.
29.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando.
31.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
32.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.
33.Mhe. Hamad Masoud Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.

34.Mhe. Omar Ali Shehe	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake.
35.Mhe. Rashid Seif Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
36.Mhe. Mohamed Ali Salim	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.
37.Mhe. Asaa Othman Hamad	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
38.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
39.Mhe. Najma Khalfan Juma	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Muhyddin Moh’d Muhyddin	“Waziri Kivuli”–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
41. Mhe. Abass Juma Muhunzi	Jimbo la Chambani.
42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
43.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.
44.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.
45.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.
46.Mhe. Ali Moh’d Bakari	Jimbo la Tumbe.
47.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.

48.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
59.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.
50.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
51.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
52. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni.
53.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
54.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
55.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
56.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
57.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
58.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
59.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais.
60.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
61.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
62.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.
63.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
64.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.
65.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.
66.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.
67.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.

68.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.
69.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.
70.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
71.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
72.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
73.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
74.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
75.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.
76.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Nafasi za Wanawake.

Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

Kikao cha Nane – Tarehe 26 Oktoba, 2009

(Kikao Kilianza saa 3:00 za asubuhi)

Dua

Mhe. Spika, (Mhe.Pandu Ameiri Kificho) Alisoma Dua.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani hotuba kuhusu Mswada wa Sheria ya Usafishaji wa Fedha Haramu na Mapato ya Uhalifu na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo, ahsante.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi): Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi juu ya Mswada wa Sheria ya Usafishaji wa Fedha Haramu na Mapato ya Uhalifu na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Said Ali Mbarouk: (Mhe. Waziri Kivuli wa Wizara ya Fedha na Uchumi): Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Maoni ya Upande wa Upinzani kuhusu Mswada wa Sheria ya Usafishaji wa Fedha Haramu na Mapato ya Uhalifu na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 8

Mhe. Mjumbe aliyeuliza swali hili amelifuta

Nam. 68

Mhe. Mjumbe aliyeuliza swali hili amelifuta

Nam. 47

Ujenzi wa Viwanda – Micheweni

Mhe. Ali Abdulla Ali - Aliuliza:-
Katika kujiimarisha kiuchumi Serikali ilitenga maeneo Huru ya Uchumi huko Micheweni Pemba kwa ajili ya Uwekezaji wa Ujenzi wa Viwanda vya Kutengenezea Bidhaa, ili kuuza ndani na nje ya nchi kwa dhamira ya kuinua kipato cha nchi. Muda mrefu umepita na eneo hilo bado halijaendelezwa na kusababisha baadhi ya wananchi kuchimba matofali ya mawe kwa kasi kubwa. Kitendo ambacho kinaharibu mazingira na kupelekea lengo la Serikali kutotekelezeka.

(a) Je, Mhe. Waziri suala hili unalifahamu?

(b) Kwa kuwa tayari eneo hilo linaharibiwa, Je Wizara ina mkakati gani wa kuzuwia uharibifu huo?

(c) Kwa kuwa sababu ni muda mrefu umepita na eneo hilo halijaendelezwa, Je, serikali ina mpango gani wa kuliimarisha ili kufikia lengo lililolikusudia?

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 47 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, naelewa kuwa eneo la chuo lililotengwa kwa ajili ya kujenga viwanda (*Industrial park*) katika Maeneo Huru ya Uchumi – Micheweni yamevamiwa na baadhi ya wananchi wanaochimba matofali ya mawe. Katika tathmini iliyofanyika mwezi Machi 2009 imebainika kuwa kiasi cha hekta moja imeshaathirika kati hekta 547.4 za eneo hilo.

(b) Mhe. Spika, Wizara yangu kwa kupitia Mamlaka ya Ukuzaji Vitega Uchumi (ZIPA) imeandaa mikakati ifuatayo kuzuwia uharibifu wa eneo hilo:-

i. Maafisa wa Mamlaka kwa kushirikiana na Maafisa wa Ardhi na Mazingira walioko Pemba hulitembelea eneo hilo mara kwa mara kwa lengo la kudhibiti uharibifu unaofanywa.

ii. Mamlaka imeandaa semina itakayowashirikisha Masheha, Wakuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba pamoja na baadhi ya viongozi wa vikundi vya wajasiriamali wa Wilaya ya Micheweni ili kuwahamasisha juu ya umuhimu wa kutunza mazingira, hasa katika maeneo huru yaliyotengwa ya Micheweni. Semina hii inatarajiwa kuendeshwa kwa mashirikiano makubwa na Idara ya Mazingira – Pemba.

iii. Wizara inahamasisha kupanda miti katika mashimo yanayotokana na uchimbaji wa matofali ya mawe, ili kuirudisha ardhi katika mashimo hayo.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, maeneo huru ya uchumi huko Micheweni Pemba yamewekwa kwa ajili ya kuleta maendeleo katika nchi yetu, hasa tukizingatia kwamba ukanda ule ni mzuri na upo katika mwelekeo ambapo wawekezaji kama miundo mbinu itafika basi watakuwa wako tayari kufanya hivyo.

Mhe. Spika, bahati mbaya iliyojitokeza katika suala hili inasemekana kwamba sasa hivi eneo hilo limevamiwa na linachimbwa matofali ya jasi kwa wingi na kuharibu yale mazingira yaliyokusudiwa juu ya kupatikana azma hiyo ya kupatikana wawekezaji.

Je, kwa kuwa suala hilo linaendelea, na Mhe. Waziri ametuambia kwamba yuko mbioni kuitisha mikutano mbali mbali ya wadau mbali mbali ili kuhakikisha kwamba uharibifu ule usiendelee. Pamoja na juhudi hiyo, je, ana wito gani kwa wawekezaji kutoka sehemu mbali mbali kwa kuwa eneo bado lipo na tunaamini kwamba kama watatangaza ipasavyo, basi wanaweza kuja kuliona eneo hilo na wakapenda kuliwekeza na manufaa yaliyokusudiwa yakapatikana.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, wizara yangu inajitahidi sana kuyatangaza maeneo yote huru Unguja na Pemba. Kwa upande wa Unguja wawekezaji wameanza kujitokeza na kwa upande wa Pemba ni matarajio yetu kwamba kujengwa kwa njia pamoja na kufika umeme katika eneo lile, basi kutaanza kufungua uwekezaji katika maeneo huru. Lakini wizara kupitia ZIPA tunajitahidi kuyatangaza maeneo haya.

Mhe. Ame Mati Wadi: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji naomba kuuliza swali moja la

nyongeza. Mhe. Spika, eneo lililotengwa la Micheweni ni eneo ambalo lilikuwa ni la matumizi ya wananchi. Hivi sasa wananchi wanalitumia sivyo. Maana kuna kuvamia na kutumia sivyo. Lakini hili limetokezea baada ya kuwa muda mrefu serikali haijaendeleza na wale wananchi hawapati taafia ya mara kwa mara.

Mhe. Spika, nimuulize Mhe. Waziri, sheria ya kutenga eneo ili lisitumike kiasi liwe muda gani linawekwa na litakapokiuka kipindi hicho, basi ijulikane kwamba labda eneo linarudi mikononi kwa wananchi.

Je, sheria hiyo ipo, au sheria hiyo bado haipo, kwa sababu ardhi ni mali ya serikali na wananchi ndio serikali yenyewe?

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, sheria ya kutenga eneo na muda gani lisipotumika litarudishwa kwa mwekezaji binafsi ni miaka 2. Akipewa eneo hakulitumia wala hakuna maelezo yoyote yanayoonesha maendeleo au hatua zinazochukuliwa kwenye eneo lile, basi baada ya miaka 2 linarudishwa.

Swali la pili Mhe. Spika, Mhe. Ame Mati amejijibu mwenyewe, kwamba ardhi ni mali ya serikali na eneo hili lilitengwa na serikali. Kwa hivyo, halina muda wa kurudi kwa sababu sijui lirudi kwa nani? Kwa hivyo, linabakia mpaka litakapotumika.

Nam. 51

Mgomo kwa Wenye Mashamba ya Karafuu

Mhe. Ali Abdulla Ali - Aliuliza:-

Hivi karibuni tulisikia katika vyombo vya Habari kuwa baadhi ya wakulima wenye mashamba ya Karafuu kisiwani Pemba walifanya mgomo wa kutokuchuma karafuu, ambazo ndio zao la Taifa katika nchi yetu tukiacha sekta kiongozi Utalii pamoja na kilimo. Maamuzi yao haya ni ya kusikitisha kwani yanadhamira kurudisha nyuma maendeleo yetu, kwa kuwa zao hili ni miongoni mwa mapato ya nchi.

(a) Je, Mhe. Waziri suala hili lilikuwa la kweli?

(b) Ni hasara ya kiasi gani imepatikana kwa makisio?

(c) Je, Serikali ilichikua hatua gani kwa kulihami zao hilo, lakini pia kwa wakulima waliofanya kadhia hiyo?

(d) Je, Serikali imetoa kauli gani ili suala kama hilo lisitokeze tena?

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 51 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, suala hili si la kweli. Wakulima wa karafuu Pemba hawakufanya mgomo wa kutochuma karafuu. Lililojitokeza ni kwamba baadhi ya wakulima wa karafuu walichelewa kuvuna karafuu zao kwa sababu mbali mbali. Aidha, baadhi ya wenye mashamba huwa wanaishi nje ya Pemba, kwa hivyo inawachukua muda kurudi na kuanza kujiweka vizuri na kuanza kuchuma karafuu hizo. Hivyo basi Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba kwa hekima zake, alichukuwa hatua za kuwahamasisha wakulima ili wazichume karafuu lakini hakukuwa na mgomo, ahsante.

Nam. 56

Kukamatwa kwa Bidhaa Zisizofaa kwa Matumizi ya Binadamu

Mhe. Ali Abdulla Ali - Aliuliza:-

Lengo Kuu la ukaguzi wa bidhaa ni kumlinda mtumiaji kutokana na majanga yatakayosababishwa na bidhaa ambazo zimeharibika kwa sababu yoyote ile. Hivi karibuni katika kisiwa cha Pemba, Wilaya ya Chake Chake kulibainika Tani 19 za Mchele, Juice Katuni 10 na Tende katuni 15 za wafanyabiashara mbali mbali zimeharibika na hazifai kutumiwa na binaadamu.

(a) Je, Mhe. Waziri suala hili unalifahamu?

(b) Kwa kuwa mali hizo ziliangamizwa kwa manufaa ya jamii. Je, ni adhabu gani wamepewa Kisheria wafanyabiashara hawa?

(c) Kwa kuwa suala hili kwa wafanyabiashara sio la kwanza linaendelea siku hadi siku. Wizara ina mkakati gani kuondoa kabisa tatizo hili?

(d) Baadhi ya wakati bidhaa zilizoharibika huangamizwa kwa kutupwa baharini. Je, kitendo kama hiki hakiharibu mazingira ya bahari?

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 56 lenye kifungu (a), (b), (c), na (d) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ni kweli bidhaa zilikamatwa katika maeneo tofauti yakiwemo Chakechake, Wete na Micheweni. Aidha, bidhaa hizo ziliangamizwa kwa mashirikiano kati ya Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji na Bodi ya Chakula Madawa na Vipodozi.

(b) Mhe. Spika, bidhaa hizo ziliangamizwa kwa kutumia Sheria Nam. 2 ya 1995 ya Kumlinda Mtumiaji na Sheria Nam. 2 ya 2006 ya Chakula, Dawa na Vipodozi. Adhabu zilizotolewa ni kuzuiwa kwa bidhaa hizo kuuzwa, kulipia gharama za uangamizaji pamoja kulipa faini.

(c) Mhe. Spika, miongoni mwa mikakati iliyowekwa na Bodi ya Madawa, Chakula na Vipodozo pamoja na wizara yangu ili kuondokana na tatizo hilo ni pamoja na:-

- Kufanya mapitio ya Sheria ya Kumlinda Mtumiaji ili iendane na wakati ambayo tayari Tenda imeshatangazwa na maombi yameshafanyiwa uchambuzi.

- Kuimarisha ukaguzi katika maeneo ya bandarini.

- Kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa bidhaa katika maduka na maghala.

- Kutoa taaluma kwa wafanyabiashara na wananchi kwa ujumla juu ya athari zinazopatikana katika kutumia bidhaa zisizofaa kwa matumizi ya binadamu.

(d) Mhe. Spika, naomba kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa bidhaa zinazoangamizwa kwa kutupwa baharini huwa haziharibu mazingira, zikiwemo mchele, maharage, kunde, chooko na njugu mawe. Aidha bidhaa hizo hazitupwi mahali pamoja. Bidhaa za makopo, tindikali (acid), juice na zisizoyeyuka kama unga wa ngano huwa hazitupwi baharini kwani zinaharibu mazingira. Uangamizaji wa bidhaa hufanywa chini ya usimamizi na ushauri wa Idara ya Mazingira.

Mhe. Ame Mati Wadi: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa bidhaa zinapoangamizwa huwa zimeonekana zina madhara kwa watumiaji binadamu, lakini kwa viumbe wengine kama ndege, ng'ombe na mbuzi huwa wanafaa kutumia bidhaa kama mchele. Hivi Mhe Waziri haoni kwamba ipo haja ya kubadilisha utaratibu, badala ya kuangamiza mchele baharini, basi wauziwe watu wa mifugo ili wapate

kunusuru mifugo yao, kwa sababu chakula hasa cha wanyama kama kuku ni ghali mno.

Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji: Mhe. Spika, wakati wa uangamizaji njia mbili maarufu ndizo zinazotumika, aidha kuchoma au kutumbukiza baharini. Madhumuni ya kufanya hivyo ni kuepusha wanadamu wasitumie bidhaa hizo. Kwa sababu kama utasema tunaweka ili tuwauzie wafuga kuku, bila ya kupata ithibati kwamba chakula cha kuku kinatengenezwa na mchele pamoja na vitu vingine.

Kwa hivyo, ni busara kuangamiza visiwepo, kwa sababu hatuna uhakika kama mwanadamu hatotumia bidhaa ile, hasa kwa ugumu wa maisha uliopo. Kwa hivyo, la busara ni kuangamiza ili kuepusha maradhi, ahsante.

SHUGHULI ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Usafishaji wa Fedha Haramu na Mapato ya Uhalifu Pamoja na Marekebisho yake

(Kusomwa kwa Mara ya Kwanza)

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mapendekezo ya Mswada wa Sheria ya Kudhibiti Usafishaji wa Fedha Haramu na Mapato ya Uhalifu na Mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, naomba nichukuwe wasaa huu kutoa shukurani za serikali kwa kupitia Wizara ya Fedha, kwa kamati yetu ya Fedha na Uchumi, inayoongozwa na Mwenyekiti wake Mhe. Salmin Awadh Salmin, kwa kazi kubwa kabisa na ustaamilivu wao Mhe. Spika, waliouonesha na uadilifu katika kuupitia, niseme neno kwa neno mswada huu. Kwa kweli mswada ulikuwa mkubwa, ulikuwa mgumu na umejaa taaluma za kisheria ya kifedha na niseme zaidi ni wa kitaalamu. Hasa unapozungumza mambo ya sheria. Kwa kweli, kwa uadilifu wao mkubwa Mhe. Spika, tumekaa siku tatu, tukajipinda kweli kweli na tukaweza kutoa huu mswada mpya kama ulivyosambazwa kwenu.

Kwa hivyo, naomba sana Waheshimiwa Wajumbe ule wa zamani uwe pembeni yenu tu, lakini hasa tuusome huu mpya ambao kwa busara walizotupa waheshimiwa kwamba ni bora tuuchapishe tena na tukakubali ushauri wao kuwa tuuchapishe tena na umelewa kwa wakati kabisa. Mhe. Spika, ni lazima nikiri kwamba kazi haikuwa rahisi. Kazi ilikuwa ni ngumu. Yote hii inatokana

na kwamba hili suala lenyewe ni suala zito na linagusa jamii na maisha ya watu wetu.

Mhe.Spika, aidha, naomba nitowe shukrani za dhati kabisa kwa Waheshimiwa Mawaziri, Manaibu Mawaziri na Wakuu wa Mikoa ambao wao walipata semina yao maalum kwa siku moja kuhusu suala hili zima.

Aidha, nikushukuru wewe Mhe. Spika, pamoja na wajumbe wote, kwa kupata wasaa wa kushiriki katika semina tuliyoitayarisha ili kupata uelewa mzuri wa hili suala. Kama nilivyosema mwanzo tulipolileta sote, hata mimi nisifiche nilikuwa kizani, haidhuru ndiye mwenye wizara, lakini kwa ugumu wa hili suala ilibidi tulifanyie kazi ya ziada. Kwa hivyo, Mhe. Spika, nitowe shukurani kwa Waheshimiwa Wajumbe wote kwa kukubali kuja katika semina yetu na kupata uelewa mzima wa hili suala.

Mhe. Spika, suala la msingi ambalo labda tutajiuliza kwa nini turidhie sheria hii hapa Zanzibar. Kumekuwa na maoni mengi kwamba inaelekea na sisi tunafuata tu maagizo au maelekezo ya wafadhili au ya watu kutoka nje, tunapta shindikizo kwamba na sisi turidhie suala hili.

Ukweli Mhe. Spika, ni lazima tukubali Zanzibar kama ni nchi kwa upande wetu na sisi hatuna budi ni lazima tufuate kanuni hizi za kimataifa, kwa sababu tusipozifuata basi tutaingizwa kwenye mkondo wa watu wanaoshiriki katika mambo kama haya. Sasa hili suala ni la kimataifa, lakini kwenye *Region* yetu iko taasisi moja inayoitwa *SM lagg East and Southern African Ant Money Laundry Association*, ambapo Tanzania ni washiriki. Sasa na sisi kama Zanzibar ni lazima tuwe mstari wa mbele ni lazima tu-*comply* na hayo maelekezo au maagizo ya hizo nchi ili na sisi tuweze kuonekana tunafuata hizo kanuni.

Mhe. Spika, utaona kwenye mswada huu labda kumeonekana kama kuna sheria kali zimewekwa na vifungo. Tumelizingatia sana suala hili na labda tukafikiria waheshimiwa wajumbe walituomba bora tupunguze, lakini kwa uzito wenyewe na hasa kufuatana na haya masuala yanavyozidi kuenea, hasa kimataifa tumehisi kwamba tuache hivi hivi kwa sasa. Kama nilivyosema adabu hizi au vifungu vitaonekana vikali, lakini suala zima ni kwamba tunapiga vita hili suala na sisi tunakubaliana na wenzetu kwamba hili suala limekuwa ni la kimataifa na hapa kwetu linaonekana, nasema linaonekana kama kwengine kwamba limeingia. Sisemi kwamba lipo, hapana limeonekana kama zilivyo nchi nyengine basi na kwetu nalo limeonekana labda lipo, kwa hivyo na hii sheria nayo inapaswa tuitekeleze.

Kwa hivyo, mambo mengine haya Mhe. Spika, niseme kwamba tumeya-*adopt* kutokana na maelekezo au marekebisho au kanuni za wenzetu hizo za kimataifa, lakini tumeziweka kwa hali yetu hapa.

Mhe. Spika, kama nilivyosema katika maneno yangu kwamba kazi kubwa imefanywa. Kwa hivyo, ukiupitia huu mswada mpya utaone sasa hivi uko moja kwa moja tu. Kwa hivyo, mimi sina haja tena ya kurejea vigungu kwa vifungu katika maneno haya ya utangulizi.

Mhe. Spika, niseme tu kwamba madhumuni makubwa ya mswada huu ni kutunga sheria ya kudhibiti usafishaji wa fedha haramu na mapato ya uhalifu. Mswada huu baada ya kuwa sheria utasaidia kuzuia usafishaji wa fedha haramu hapa nchini kama nilivyosema.

Mswada wenyewe Mhe. Spika, umegawika katika sehemu 10.

Sehemu ya Kwanza, inahusu utangulizi ambapo jina fupi na kuanza kutumika kwa sheria na tafsiri ya baadhi ya maneno yaliyotumika katika sheria hiyo.

Sehemu ya Pili, inahusu katazo la usafishaji sio usafirishaji ni usafishaji wa fedha haramu.

Sehemu ya Tatu, inahusu kuanzishwa kwa kitengo cha taarifa za fedha na kamati ya kitaifa ambapo kwa kifupi itajulikana kama FIU.

Sehemu ya Nne, inahusu usimamizi wa usafishaji wa fedha haramu.

Sehemu ya Tano, inahusu kutaifishwa kwa mali chafu na utaratibu wa amri ya kutaifishwa kwa mali chafu.

Sehemu ya Sita, inahusu amri ya kulipa faini ya fedha.

Sehemu ya Saba, inahusu amri ya kutaifisha kwa mujibu wa makosa yaliyotajwa.

Sehemu ya Nane, inahusu usimamizi wa mali inayotakiwa kutaifishwa, uwezo wa kupekua na kukamata mali chafu.

Sehemu ya Tisa, inahusu uwezo wa kukusanya taarifa na

Sehemu ya Kumi, inahusu mambo mengineyo ambapo waziri amepewa uwezo wa kutunga kanuni.

Mhe. Spika, kwa ufupi hiyo ndio ufupisho wa mswada wenyewe. Kama nilivyosema mswada ni mkubwa na ningewaomba sana Waheshimiwa Wajumbe ile *version* ya Kiingereza nayo wasiwe mbali nayo, kwa sababu itatusaidia sana kutafsiri wakati mwengine hasa mambo ya kisheria. Tulipata kazi hata kwenye kamati, kwa sababu inabidi wakati mwengine utafsiri labda kwa Kiswahili au kwa Kizungu cha kawaida. Wanasheria wanatuelekeza kwamba wao wanatafsiri zao za kisheria ambazo ni lazima tuzizingatie.

Kwa hivyo, ningewaomba sana waheshimiwa wachukuli katika kifungu cha kule kwenye ufafanuzi, naomba ninukuu kidogo katika sheria hii, 'Kama itaelezwa vyenginevyo lakini hayo maneno ya-*refer* kwenye mswada wenyewe huu', tusitafsiri moja kwa moja kwa kizungu, yaani u-*reflect* moja kwa moja kwenye mswada huu. Tumejitahidi sana na tutazidi kupokea ushauri wenu na maelekezo yenu waheshimiwa ili kuweza kufanikisha na kutekeleza vyema mswada wetu. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa Iamuliwe)

Mhe. Salmin Awadh Salmin: (Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi): Mhe. Spika, ifuatayo ni hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi juu ya Mswada wa Sheri ya Kudhibiti Usafishaji wa Fedha Haramu na Mapato ya Uhalifu na Mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, naomba kwanza nichukuwe nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu, kwa kutuwezesha kuendelea kutumia neema na rehema zake, tukiwa hai na wenye afya njema.

Pili nikushukuru wewe mwenyewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kwanza kutoa maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi, yanayohusiana na Mswada wa Sheria ya Kudhibiti Usafishaji wa Fedha Haramu na Mapato ya Uhalifu na Mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, naomba nichukuwe nafasi hii vile vile kwa kumshukuru na kumpongeza kwa dhati kabisa, Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha, kwa uwasilishaji wake mzuri. Pongezi hizi ziende pia kwa Katibu Mkuu na watendaji wake wote kwa kazi nzuri ambayo wameifanya inayohusiana na mswada huu.

Mhe. Spika, naomba pia nitumie nafasi hii adhimu niwashukuru wajumbe wenzangu wa Kamati ya Fedha na Uchumi, kwa mashirikiano yao mazuru wanayonipa. Wajumbe wenyewe ni kama hawa wafuatao:-

Kwanza ni mimi Mhe. Salmin Awadh Salmin	Mwenyekiti,
Mhe. Ali Abdalla Ali	Makamo Mwenyekiti,
Mhe. Assa Othman Hamad	Mjumbe
Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	Mjumbe
Mhe. Ashura Abeid Faraj	Mjumbe
Mhe. Mwajuma Faki Mdachi	Mjumbe
Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Mjumbe
Mhe. Said Khelef Ali	Mjumbe
Mhe. Rashid Seif Suleiman	Mjumbe
Ndg. Maryam Hussein Rajab	Katibu
Ndg. Amour Moh'd Amour	Katibu

Mhe. Spika, mswada huu umekuja kwa wakati, kwani dunia tunayoishi leo imekuwa na mambo mengi sana yanayowakwaza wakaazi wake. Dunia hii imekuwa na changamoto za hatari sana, kuna tishio la ugaidi, hatari za madawa ya kulevya na UKIMWI, ufisadi, rushwa iliyokithiri na mengi yanayohusiana na hayo. Mambo yote hayo yanaiweka dunia ionekane kama vile siyo pahala pazuri pa kuishi.

Mhe. Spika, tamaa ya binadamu ya kutaka kujitajirisha imekuwa kubwa na inayoongezeka kila siku na kasi yake hiyo haijali hata kidogo madhara ya wengine. Lakini kwasababu matendo hayo ni ya kibinadamu, basi hao ndio wanaotakiwa kujenga mazingira yatakayoiweka dunia hii kuwa pahala salama pa kuishi.

Mhe. Spika, utungwaji wa Sheria ya Kudhibiti Usafishaji wa Fedha Haramu na Mapato ya Uhalifu ya 2009, ina mtazamo wa kuweka mazingira salama katika nchi yetu. Tunaelewa kwamba kuna sheria nyingi tu zenye kuifanya kazi hiyo kama vile za madawa ya kulevya na nyingi zinazohusiana na kuzuia kutenda makosa.

Lakini kwa mapendekezo ya sheria hii pamoja na msisitizo wake juu ya kuwabana watendao makosa, kubwa zaidi hata pale ambapo mwenye kupata fedha kwa njia ya makosa yaliyoorodheshwa, endapo atakuwa anasafisha fedha zake hizo kwa njia ya kuzidi kujilimbikizia mali. Sheria itambana na kustahili adhabu; hata kama uwekezaji wake utakuwa na tija kwa taifa.

Mhe. Spika, Chombo chako hiki kimekuwa kikitunga sheria nyingi sana, lakini kwa bahati mbaya kumekuwa na udhaifu mkubwa kwa zile taasisi zinazosimamia utekelezwaji wa sheria hizo.

Sisi tunaamini kwamba ikiwa sheria hii itasimamiwa kisawasawa bila ya kuonea haya na muhali, basi yale makosa yaliyoorodheshwa yatakomeshwa.

Mhe. Spika, nchi yetu kama zilivyo nchi nyengine zinazoendelea inahitaji sana nyenzo za kuifikisha kwenye maendeleo, lakini maendeleo hayo yawezeshwe kwa njia halali na zenye kukubalika si kwa mitaji iliyopatikana kwa mizengwe hii, mizengwe inayotokana na fedha haramu. Hivyo, katu tusikubali hata kidogo kuweka mianya itakayoruhusu wale, ambao wanakusudia kuekeza kwa ajili ya kusafisha fedha zao.

Pamoja na Tafsiri zilizomo kwenye mapendekezo ya mswada huu, Sehemu ya Pili ya Mswada inasisitiza juu ya katazo la usafishaji fedha hizo haramu. Msisitizo huu unaonesha mazingira yote, ambayo mtu atakuwa amejihusisha au amechangia kujihusisha, kushiriki au kuchangia kushiriki wakati akijua kwamba mapato ya fedha hizo ni ya haramu atakuwa ametenda kosa.

Mhe. Spika, uzoefu unaonyesha kwamba watu wengi ambao hujipatia fedha kwa njia zisizo halali bila ya kukamatwa au kutiwa hatiani, hudhania kwamba wamevuka na ili sasa wazitumie, basi huziwekeza katika miradi mbali mbali kwa ajili ya kuzisafisha, watu hao waelewe kwamba kufanya hivyo ni kosa, sheria hii itashika mkondo wake *(Makofi)*.

Mhe. Spika, kamati yetu inaamini kwamba mafanikio ya utekelezaji wa sheria hii inayopendekezwa, yatatokana sana na upatikanaji wa taarifa zenye ukweli. Taarifa ambazo hazitatolewa kwa ajili ya kumkomoa mtu au kwa kusingizia kutokana na chuki na wala hazitakuwa ndio chanzo cha fitina, bali zitakuwa ni za ukweli zisizo na chembe yoyote ya visingizio na dhana.

Sehemu ya Tatu ya mswada huu, imeanzisha Kitengo cha Upelelezi wa Taarifa za Fedha pamoja na kuundwa kwa Kamati ya Kitaifa. Kitengo hichi kinachojulikana kama *Financial Investigate Unit (FIU)*, kitakuwa na jukumu kubwa la kuhakikisha kwamba kinapokea, kuchambua na kuzisambaza taarifa hizo muhimu zitakazopatikana kutoka katika vyanzo mbali mbali ambavyo vitapelekea kujua nani mkosa kwa mujibu wa sheria hii. Bila shaka huwezi kupeleleza bila ya kutilia shaka, hivyo kwenye kitengo hiki ndipo shaka au tuhuma hizo zinapochujwa.

Mhe. Spika, Kitengo hiki (*FIU*) kwa mujibu wa sheria hii, kitasimamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa sheria iliyotungwa na Bunge. Kwa bahati mbaya sana Mhe. Spika, muundo wa kitengo hiki hauonyeshi moja kwa moja kuwa ni cha Muungano wa Tanzania.

Mhe. Spika, kamati inamtaka Mhe. Waziri wa Fedha wa Zanzibar, wakae pamoja na mwenzake wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ili warekebishe kasoro hizi, hii ikiwa ni pamoja na kufungua afisi yake hapa Zanzibar *(Makofi)*.

Katika suala la usimamizi wa kudhibiti usafishaji wa fedha haramu taarifa na kumbukumbu za wenye biashara au wanaotaka kuhaulisha fedha zinakuwa katika mfumo uliokamilika, kiasi cha kuondoa ile dhana juu ya usafi wa fedha zinazofanyiwa biashara. Mtiririko wa maelezo hayo umo katika mapendekezo ya mswada huu kwenye sehemu ya nne.

Mhe. Spika, sheria hii inayopendekezwa imeweka adhabu kali kwa watakaokwenda kinyume ikiwemo kifungo, faini na utaifishaji wa mali. Adhabu hizo zinaonekana ni kubwa, lakini katika mazingira ya ustawishaji wa jamii yetu, kamati inaamini kwamba haki itatendeka na adhabu hizi zitawafikia walengwa tu na si kwa watu wengine.

Mswada huu katika kutoa adhabu utahusisha watu binafsi, makampuni au mashirika yoyote, ambayo kwa njia moja au nyengine yatakuwa yameshiriki katika kuekeza kupitia fedha hizi haramu. Tunaamini kwamba utekelezaji wa sheria hii hautakuwa mtego wa panya, ambao unaweza kuwanasa waliokuwemo na wasiokuwemo. Lakini ni dhahiri kwamba kama utatekelezwa kidhati basi aliekuwemo hatoki na asiyekuwemo hatoingia.

Mhe. Spika, kamati yetu inaamini kwamba sheria hii ina mazingira ya ugeni, ijapokuwa matendo ya jamii ambayo yameainishwa na sheria hii ni yale yale yanayotendwa kila siku. Hali hii inatokana na wengi wenye kupata mali kwa njia zisizo sahihi huona hili ni jambo la kawaida, kwa maana hiyo utekelezaji wa sheria hii unaweza kuwashtua sana. Hivyo tunawaomba wananchi waielewe sheria hii, kwani hao ndio watakaoweza kusaidia utekelezaji wake kwa kutoa taarifa.

Tunawategemea sana wananchi kwenye sheria hii, hivyo ni imani yetu kwamba bado taaluma kubwa inahitajika kwao kwani sheria hii ni kubwa kwa maana yake, lakini pia kubwa kwa maana ya urefu na idadi ya vifungu vinavyofikia tisini.

Jengine ni kwamba katika sheria hii kuna matendo mengine yametajwa vilevile kwenye sheria nyengine, nalo hilo kwa wananchi wetu wa kawaida linaweza kuwa ni tatizo. Kwa hivyo, narudia kusema ili tufanikiwe kwenye utekelezaji wa sheria hii Mhe. Waziri ajaribu kutoa elimu kupitia vyombo vya habari Televisheni na Redio, yenye kuainisha ufafanuzi wa vifungu vya sheria ili kuongeza wigo wa ufahamu wao.

Mhe. Spika, maadili ni usafi, hauishii kwenye usafi wa mwili na nguo tu, bali ni moyo wa matendo mema. Hili ni lengo kuu la sheria hii. Mafanikio makubwa kama itatekelezwa vyema. Hivyo wasimamizi nao wawe mfano wa

kuwa na maadili mema. Kamati yetu inaomba wahusika hili walielewe, waliamini na watekeleze majukumu yao kwa dhati ya moyo wao.

Mhe. Spika, sote tunaelewa kwamba wakosaji wengi wa makosa yaliyooredheshwa ni watu wenye uwezo mkubwa wa mali na fedha, kamati inaziomba Mahkama zetu ziendeshe kesi hizi kwa mujibu wa sheria bila ya aina yoyote ya vishawishi wala woga, na kuacha kuangalia kuwa huyu ni nani na anawadhifa gani. Kwani sheria ni msumeno.

Mwisho Mhe. Spika, kwa niaba ya Kamati ya Fedha na Uchumi pamoja na wananchi wote wa Jimbo la Magomeni tunaunga mkono hoja hii, tukiwaomba na wajumbe wenzetu wawe pamoja nasi na tuuchangie kwa nia ya kuufanya mswada huu uwe ni sheria bora.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Said Ali Mbarouk (Waziri Kivuli Fedha na Uchumi) Mhe. Spika, kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaaliya uzima kuwepo katika kikao hiki. Vile vile nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuzungumza machache kuhusiana na mswada huu mkubwa katika kikao hiki cha Baraza.

Mhe. Spika, Mhe. Salmin Awadh Salmin (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi) alianza kwa kumpongeza Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi kwa uwasilishaji wake, yeye anahisi kwamba amekuwa *very brief* leo.

Kwa hivyo, mimi nampongeza Mhe. Salim Awadh Salmin (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi) angalau kutupa ditals kidogo zinazohusiana na mswada huu *(Makofi)*.

Mhe. Spika, chimbuko la mswada wa sheria hii ni Mkataba dhidi ya Uhalifu wa Kimataifa uliopitishwa na Umoja wa Mataifa, yaani *The United nations Conventions Against Transitional Organized Crime and the Protocol Thereto* wa mwaka 2000.

Nchi yetu imetakiwa kupitisha sheria hii ili kukubaliana na Mkataba huo wa Kimataifa, kama ambavyo Tanzania ilivyoridhia mkataba huo.

Mhe. Spika, Kambi ya Upinzani ina mashaka makubwa na wasi wasi juu ya nia na uwezo wa kuitekeleza sheria hii, isije ikawa tunapitisha sheria kwa ajili ya shindikizo la Jumuiya za Kimataifa na wakubwa wa dunia na ikabaki makabatini, kwa sababu ya kuwa na sheria isiyotekelezeka.

Mhe. Spika, inafahamika wazi kwamba Bunge la Jamhuri ya Muungano lilikwishapitisha sheria hii tokea mwezi wa Novemba mwaka 2006, ambayo ilieleza wazi kwamba utekelezaji wake utakuwa hadi Zanzibar. Mhe. Spika kwa mujibu wa Kifungu cha 131(1) cha Katiba ya Zanzibar, na naomba kunukuu.

Katiba ya Zanzibar kifungu cha 132 (1) kinasema hivi:-

> "Hakuna sheria yeyote itakayopitishwa na Bunge la Muungano ambayo itatumika Zanzibar mpaka sheria hiyo iwe kwa ajili ya mambo ya Muungano tu na ipitishwe kulingana na maelekezo yaliyo chini ya vifungu vya Katiba ya Jamhuri ya Muungano".

Mhe. Spika, Kambi ya Upinzani inataka maelezo ni kwa nini Zanzibar ikaamua kuunda sheria yake baada ya kuipitisha ile iliyopitishwa na Bunge. Je, imekosa sifa za kua ni sheria ya Muungano au vipi.

Zanzibar kama tumeamua kuwa na sheria yetu, je ni kwa nini ndani ya sheria hii tukaridhia vipengele viwili vilivyomo ndani ya sheria iliyopitishwa na Bunge ambavyo ndio viungo muhimu vya sheria hii, yaani Kipengele 10 (1) na (2), vya mswada huu ambavyo ni kuwepo kwa Kamati ya Kitaifa ya Kushughulikia Usafishaji wa Fedha Haramu na kuwepo kwa Kitengo cha Taarifa ya Fedha (*FIU*) bila hata ya kuruhusu kuvijadili. Vipengele hivi kama ilivyoelezwa katika sheria hii vitakuwemo kwenye Kiambatanisho (*schedule*) cha sheria hii.

Mhe. Spika, kiambatanisho hicho hakikuambatanishwa na mswada huu kwa wajumbe, hii ina maana wajumbe wako watapitisha vipengele hivyo bila ya hata kujua maelezo yoyote kuhusiana navyo. Kwa mfano, nani wajumbe wa kamati ya Kitaifa ya Kushughulikia Usafishaji wa Fedha Haramu na uteuzi wao utafanyikaje? Vile vile nani wajumbe wa *FIU*, na watapatika vipi. Katika usimamizi wa sheria hii, nguvu na mamlaka ya Waziri wa Zanzibar itakua kwa kiwango gani kuhusiana na Kamati ya Kitaifa na Kitengo cha *FIU*, na nini majukumu yao.

Kambi ya Upinzani inahitaji pia kupatiwa maelezo ni vipi maslahi ya Zanzibar kama nchi, yatalindwa katika vifungu hivi viwili vya sheria ambavyo vimo katika sheria hio iliopitishwa na Bunge. Hakika Kambi ya Upinzani inasikitishwa na usiri uliogubika Kamati hio ya Kitaifa na Kitengo cha *FIU*.

Mhe. Spika, katika sehemu ya kwanza kwenye kifungu cha pili cha ufafanuzi, upangaji wa kifungu hicho si mzuri, kwani vifungu vya ufafanuzi havikuelewa nambari. Kwa mfano, katika ukurasa wa 62 mtu anapotaja kifungu a, b, c, d hawezi kufahamika, kwani kuna a, b, c, d namna mbili ambavyo havina mshabaha wa nambari husika, kwa kweli tatizo hilo limejirudia kwenye kurasa nyingi za sehemu kwanza kifungu cha pili cha mswada huu. Kambi ya Upinzani inashauri lifanyiwe marekebisho, ili sheria ikipitishwa iwe na mtiririko mzuri.

Mhe. Spika, katika Sehemu ya kwanza inayohusiana na tafsiri ya baadhi ya maneno yaliyotumika ndani ya mswada huu wa sheria, Kambi ya Upinzani inashauri kwamba ni vyema neno Ugaidi (*Terrorism*) likawekewa tafsiri ambayo itakua inajulikana na kufafanuliwa *(Makofi).*

Mhe. Spika, katika kifungu cha 4 cha mswada huu, Mhe. Spika, naomba kunukuu

> Kifungu cha 4 kinasema hivi:-
>
> > "Kwa madhumuni ya sheria hii, mtu atachukuliwa ametoroka ikiwa:-
> >
> > a) Taarifa zimepatikana kuhusiana na kutenda kwake kosa;"…

Sasa ikiwa taarifa imepatikana kwamba fulani ametenda kosa, na hivyo kuchukuliwa kwamba ametoroka, hili litakuwa jambo la ajabu na kwa kweli wengi tutakuwa watoro. Kambi ya Upinzani inahisi hapa panahitaji marekebisho *(Makofi).*

Mhe. Spika, adhabu inayotolewa katika kifungu cha nane cha sheria hii, 8 (1) na (2). Je hii kweli imezingatia hali halisi ya Wazanzibari maana viwango hivyo ambavyo ni vya Kimataifa havioani na hali hali ya uchumi wa Zanzibar na watu wake.

Mhe. Spika, mswada huu ni moja ya miswada ambayo utekelezaji wake utakuwa mgumu mno, hasa kutokana na uhodari na umakini wa hali ya juu unaotumiwa na wahalifu wa fedha haramu na ugumu unazidi pale mswada unapoainisha mazingira mbali mbali yanayopelekea fedha haramu kama kifungu *Predicative Offence* Kosa lililoorodheshwa.

Mhe. Spika, Kambi ya Upinzani inashauri kuwa serikali ijiandae vya kutosha katika kujenga na kuimarisha mazingira ya kiutendaji, mifumo ya upelekaji

habari, kujenga uwezo wa kitaaluma wa watekelezaji wa sheria hii, ili waweze kukabiliana na mabadiliko ya haraka ya kiteknolojia katika shughuli zao *(Makofi)*.

Serikali haina budi pia kutoa elimu hii kwa jamii, ili iweze kutoa mashirikiano na watekelezaji wa sheria hii.

Mhe. Spika, katika kipengele cha kumlinda mtoa taarifa, kwa mujibu wa tafsiri ya mtoa taarifa, haionekani kama mtu binafsi (*individual*) atakuwa naye anapatiwa kinga.

Je, ikwa mtu binafsi atatoa taarifa za kuwepo kwa vitendo vya uhalifu na inawezekana ikabidi kuwa shahidi. Hivyo, vipi sheria hii itawapatia ulinzi ili wasidhuriwe.

Mhe. Spika, Kambi ya Upinzani inatoa angalizo kwamba baadhi ya wasimamizi wa sheria hii wanaweza kutumia sheria hii kwa njia ya kuwakomoa wale ambao wana chuki nao, kwa kutumia kipengele cha kutoa taarifa kwa vyombo vya usimamizi kuwa mtu fulani anajihusisha kwenye uhalifu wa kusafisha fedha haramu.

Katika hili Kambi ya Upinzani inaishauri serikali kuandaa taratibu zitakazoweza kudhibiti hali hiyo isitokee, kwani isipodhibitiwa huenda ikaathiri maelewano na kuzua migogoro ndani ya jamii yetu.

Mhe. Spika, Kambi ya Upinzani inashauri kwamba katika kuhakikisha wahalifu ndani ya jamii wanapatikana, vyema kukaanzishwa utaratibu wa kuwapa motisha wale wote wanaoripoti taarifa kuhusu uhalifu wa aina hii. Jamii itahamasika na kusaidia katika kuwafichua wahalifu.

Vile vile katika kifungu cha 17 cha mswada huu inaeleza sera inayofuata, lakini hakuna maelezo sera inayokusudiwa ni ipi.

Mhe. Spika, kifungu cha 19 cha mswada huu, Kambi ya Upinzani inaomba ufafanuzi wa maana iliyokusudiwa, kwani katika nchi kuna masuala nyeti yanayohusiana na siri (*classified information*). Ikiwa wajibu huo unaondoka kwa sababu tu ya sheria hii, tunahitaji tupatiwe ufafanuzi zaidi kuhusu umuhimu wa kifungu hichi na siri nyeti za nchi.

Mhe. Spika, katika kifungu cha 25 kinatoa rai kwa mahkama kutia hatiani na kutolewa amri ya kutaifisha endapo mtu atakuwa ametoroka, huku katika kifungu cha 4, kuwa utata kuhusiana na maana ya kutoroka kwa mtu. Kifungu

hichi kitangulie kwanza na marekebisho na maana ya kutoroka ndio kifungu cha 25 kifanye kazi.

Pia kwenye kifungu cha 43, (7), (8) mswada huu unampa uwezo askari polisi kumvua nguo zote mtu na kumwacha uchi wa mnyama akiona ni muhimu katika kufanya upekuzi. Kambi ya Upinzani haikubaliani na udhalilishaji huu, na kwa hakika katika enzi hizi za maendeleo ya sayansi, serikali ijitayarishe kumiliki vifaa vya *electronics* kwa ajili ya upekuzi.

Masuala ya kuvuana nguo yamepitwa na wakati, na Baraza hili haliwezi kubariki aibu kama hio katika enzi hizi, kwa vyovyote vile hakuna heshima yoyote itayozingatiwa kwa mtu kupekuliwa kwa kuekwa uchi wa mnyama, na kwa hakika Zanzibar haiwezi kutunga sheria sawa na enzi za askari wa nazi za Hitler wa enzi hizo *(Makofi).*

Mhe. Spika, kifungu cha 47 kinampa mamlaka askari polisi kufanya upekuzi na kukamata bila ya kupata *search warrant* kutoka mahakamani, ikiwa anaamini kufanya hivyo kutazuia ufichwaji, upoteaji au uharibifu wa mali. Kambi ya Upinzani ina wasi wasi mamlaka haya yanaweza kutumiwa vibaya na polisi katika kufanya upekuzi bila ya *warrant* ya mahakama; na hivyo kuwa ni sababu ya kurudia enzi zile za upekuzi na ukamataji wa taswira ya kuonea watu na kuvunja haki za binaadamu.

Mhe. Spika, kifungu cha 83 cha mswada huu kinataja amri ya kunyang'anya mali. Kambi ya Upinzani inaomba ufafanuzi wa maana iliokusudiwa kabla ya Baraza hili halijatoa ridhaa kwa serikali kunyanganya mali za wananchi na wageni.

Mwisho Mhe. Spika, kifungu cha 90 cha mswada huu kinatoa mamlaka kwa Waziri anaehusika kutunga Kanuni, kimsingi Kambi ya Upinzani haipingi Waziri kupewa mamlaka haya, isipokuwa ushauri wa bure unatolewa kama ifuatavyo:-

a) Katika kipindi kifupi kama kinavyowezekana, kanuni zinazohitajika zitungwe, ili sheria itapotungwa iweze kutekelezeka, isije ikawa kama baadhi ya sheria zinazotungwa na Baraza lako zikachukua miaka kabla ya kanuni zake kutungwa. Kwa mfano, Sheria ya Mahkama ya Kadhi, habari niliyonayo tangu ilipotungwa miaka ya 1980 hadi leo haijatungiwa kanuni zake na hivyo kuyumbisha utekelezaji mzuri wa sheria hio *(Makofi).*

b) Kanuni zitazotungwa zisibadilishe maana ya sheria iliyopitishwa, isije ikawa kama baadhi ya sheria ambazo kanuni zake zilizotungwa zimeifanya sheria mama iwe inayumba na isiweze kutekelezeka vizuri au utekelezaji wake ukawa unawanyima fursa na haki wananchi. Kwa mfano, Sheria ya Kitambulisho ya Mzanzibari Mkaazi *(Makofi)*.

c) Kwa kuziepuka kasoro zilizomo kwenye aya (a) na (b) hapo juu na kwa utekelezaji mzuri wa sheri aitakayotungwa na mswada huu. Nadhani ni vyema Mhe. Spika, Baraza lako likaweka muda maalum kwa wizara kutunga kanuni hizo na kabla ya kutumika zipitiwe na kukubaliwa na kamati husika ya Baraza iliyojadili mswada huo.

Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii pamoja na Waheshimiwa Wajumbe kwa kunisikiliza.

Naomba kuwasilisha.

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja: Mhe. Spika, ahsante sana. Awali ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru *Allah Subuhanahuu Wataala* kwa kunipa uzima na kuweza kusimama katika Baraza lako hili, kwa ajili ya kutoa mchango wangu mdogo kwenye mswada huu.

Mhe. Spika, nilikuwa nimejiandaa vizuri sana katika mswada ule wa mwanzo. Lakini nataka nichukue nafasi hii kuipongeza sana Kamati ya Fedha na Uchumi, kwa kazi nzuri waliyofanya, yaani *points* zangu zote kwa kweli wameninyang'anya. Kwa kweli kazi waliyoifanya ilikuwa ni nzuri sana, kwa sababu mswada ule tuliopewa mwanzo ulikuwa na kasoro nyingi sana *(Makofi)*.

Mhe. Spika, nilikuwa nikitafuta maana halisi ya fedha chafu, lakini nimepata maana nyingi sana na nitazitaja mbili. Moja nilikuwa nikijiuliza ikiwa mtu ameokota fedha nafikiri sheria za dini zote zinasema, unapookota fedha kwanza unatakiwa uitangaze na kama hakutokea mtu ndio inakuwa halali yako.

Nakumbuka katika miaka ya 40 Mhe. Spika, kuna Mbaniani mmoja aliokota mfuko ndani yake ukawa una fedha, basi alikuwa akipita Darajani na kusema "nani napoteza fuko ndani yake ananyamaza halafu kwa mbali anasema pesa". Mhe. Spika, hali hii inatuonesha kwamba dini zote zinasema kwamba utangaze kama hukutangaza inakuwa si halali yako *(Kicheko/Makofi)*.

Sasa nilikuwa nikijiuliza kwa mfano nimepita pahala na kulikuta begi ndani yake zimo dola bilioni nimeliokota, nasema hapo umasiki umeshanitoka sitangazi. Lakini ghafla nimenunua shangingi (gari) moja la kwendea shamba, nimenunua *benz* moja ya kutembelea mjini, nimenunua nyumba moja nzuri naanza kujenga hoteli, serikali ndio inaposhtuka huyu fedha amepata wapi.

Mhe. Spika, nataka kumuuliza Mhe. Waziri fedha hizi halali au chafu na kama nimezitangaza hakutokea mwenyewe inakuwa vipi. Kwa sababu sheria inatueleze kwamba tuzitangaze.

Suala jengine nilikuwa nikimchokoza hapa swahibu wangu Kanuni zinatukataza tusitaje jina katika kujadili hizi fedha chafu. Lakini katika kuchokoza kwangu nilikosea kusema nilimwambia hivi Mhe. Mjumbe sisi hapa tunapewa *sitting allowance*, yaani ile *sitting allowance* ndio kosa lenyewe na halafu nyinyi hamsemi huoni kwamba hizi fedha chafu.

Mhe. Spika, aliniambia umeshajijibu mwenyewe, tunapewa *sitting allowance* na sio *speaking allowance*. Kwa hivyo, tukipewa *speaking allowance* Mhe. Spika hutopata tabu hapa watu watachangia sana.

Nikiendelea na mchango wangu kwa kweli tatizo la fedha chafu limekuwa ni la kitaifa. Mhe. Spika, juzi nilitaja mambo matano ambayo yameikabili dunia, lakini kumbe la fedha chafu lilikuwa la sita na wala sikulitaja siku ile. Kwa sababu tunaweza kujiuliza masuala mengi katika fedha hizi.

Kwa mfano, hivi sasa kuna vita Pakistan katika Mkoa unaoitwa Waziristan, Serikali ya Pakistan pamoja na Al-Qaida. Lakini suala ninalojiuliza hivi hawa Al-Qaida wanaopigana huko Waziristan hisi pesa za kununulia silaha wanazipata wapi? Lakini kwa kuwa huko Pakistan na Afghanistan ndio tunakoambiwa kunakotoka madawa ya kulevya sana. Je, hawatumii pesa hizi za madawa ya kulevya kwa kuleta matatizo ndani ya dunia?

Mhe. Spika, jengine kuna eneo Nigeria kunakotoka mafuta Jimbo la Delta nako kumekuwa na machafuko. Utakuta wapinzani pale wanaoipinga serikali, wana silaha nzito nzito za kivita, ukijiuliza swali hawa silaha hizi wanazipata wapi? Sio hizo pesa chafu zinazotumika katika kuwapa nguvu hawa? Ama kuna nchi nyengine nyuma inaowaunga mkono kwa sababu ya mafuta?

Mhe. Spika, vile vile ukiangalia vita vya Darfur, suala linakuja hivyo hivyo kwamba hivi vita vya Darfur hawa wanaopinga silaha wanazipata wapi? Halikadhalika vita vya Congo, vita vya Uganda, Somalia ukijiuliza masuala katika hizi nchi ambazo sasa hivi zimo katika vita, hivyo pesa hizi za kununulia

silaha wanazipata wapi? Hizo si ndio pesa chafu zinazoranda katika dunia zikasababisha matatizo?

Mhe. Spika, matatizo makubwa katika nchi hizo wanaopata ni wazee, wanawake na watoto. Mhe. Spika, utakuta hawa wanaowa-*support* pengine kwa pesa hizo haramu wanawatia hatiani wazee, wanawake na watoto, wakati hawana makosa yoyote. Ndio maana dunia yetu sasa hivi inapata misukusuko kwa sababu tunawatesa watu pengine kwa manufaa ya mtu mmoja au wawili.

Mhe. Spika, jengine lililojitokeza ambalo sasa hivi limo katika dunia ni usafirishaji wa watoto hasa watoto wa kike. Mbaya zaidi ni kwamba wanakwenda kufanyishwa biashara ya kujiuza kwa kutumia miili yao. Mhe. Spika, hili ni tatizo kubwa na tusipoliangalia hata na sisi huku linaweza kuja kutukumba. Kwa hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe watoe mifano kama niliyotoa mimi au pengine wao wanayo zaidi ili tuuzungumze mswada huu vizuri, tuchangie vizuri, penye kasoro tuseme hatimae tuipe uwezo serikali iweze kusimamia ili kama haya mabalaa niliyokwishayasema yasije yakaingia katika nchi yetu.

Mhe. Spika, ni kwamba matatizo ni makubwa, dunia imekabiliwa na changamoto nyingi, juzi nilisema kuna changamoto ya fedha sasa hivi, kuna changamoto ya joto lililozidi duniani. Juzi nilikuwa nikisoma kuna kisiwa kimoja ambacho kimo katika hatari ya kutoweka ni kwamba wameamua kwenda kufanya mkutano ndani ya bahari, mkutano wa mawaziri. Mhe. Spika, mawaziri wamefundishwa kuogelea pamoja na Rais wao, wameandaa karatasi maalum za plastiki ambazo haziharibiki kwa maji na kalamu maalum za kuandikia, wamekwenda kufanya mkutano ndani ya maji na wote wale mawaziri yakasaini. Mhe. Spika, hiyo ilikuwa ni kuishindikiza dunia kupunguza hili joto ambalo lipo.

Mhe. Spika, jengine ni kwamba tuna tatizo la chakula, tunaambiwa karibu watu milioni kumi na mbili wanaweza wakapoteza maisha kwa sababu ya chakula. Tuna tatizo la madawa ya kulevya, tuna matatizo ya ukimwi, tuna matatizo ya pesa haramu, hizi zote ndio changamoto ambazo dunia imeshakumbwa nazo. Mhe. Spika, na sisi tukiwa katika sehemu ya dunia hii tunatakiwa tukabiliane nazo kwa nguvu zetu zote ili tuweze kuepukana na hayo. Mhe. Spika, hilo linawezekana kama tutashirikiana vizuri tutakuwa na nguvu za pamoja na kila mmoja wetu akasema sasa tufanye hii kazi yakuweza kuondoa matatizo haya. Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo mafupi sasa nataka niingie kwenye mswada.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 58 amri ya kutaifisha. Hapa imeandikwa maana yake ni amri ya kutaifisha au amri ya kulipa faini ya fedha. Mhe. Spika, kulipa

faini ya fedha sio kutaifisha, sasa sijui Mhe. Waziri ataniambia kama alivyoniambia juzi kwamba kutoka Kiengerea kuja Kiswahili kidogo imempa tabu. Mhe. Spika, nafikiri hapa ingelikuwa amri ya kutaifisha maana yake ni amri ya kuitaifisha mali inayohamishika au isiyohamishika, hivyo ingeleta maana nzuri zaidi. Kwa sababu ukija hapa kulipa faini ukurasa wa 59 chini kabisa amri ya kulipa faini ya fedha imeelezwa vizuri. Mhe. Spika, hii amri ya kulipa faini nafikiri tungeiwacha huku, huku ikawa hii amri ya kutaifisha.

Mhe. Spika, vile vile katika ukurasa wa 61 kuna kosa la kawaida la kukamata, maana yake imeandikwa ni kosa la kukamata ambalo sio kosa kubwa,kosa la kukamata mheshimiwa lisiwe kosa kubwa. Nafikiri kosa la kukamata maana yake ingelikuwa kosa la kukamata mali ama mtu, hilo ndio kosa la kukamata. Lakini hakuna kosa la kukamata likawa dogo wakati mwengine unakwenda kumkamata mtu mbabe mnaweza mkapigana akakuumiza. Mhe. Spika, mimi naona hapa kwa mujibu wa Kiswahili haliko sahihi.

Pia hapo hapo chini, kuna eneo maana yake ni jingo, ndege, gari au meli hiyo imepangika vizuri lakini ningeomba kuongezwe neno na shamba. Maana yake hata katika shamba mtu anaweza akaficha pesa haramu.

Mhe. Spika, jengine ambalo limenitia wasi wasi kidogo, namuomba Mhe. Waziri akija atusaidie kwa jumla. Mhe. Spika, kuanzia kifungu cha 13-17 kinazungumzia mtoa taarifa, lakini mtoa taarifa amewekewa sharti nyingi kweli. Mhe. Spika, wasi wasi wangu mimi labda sijafahamu maana ya mtoa taarifa maana yake nini? Lakini ikiwa mtoa taarifa kama mimi mfano nimegundua kitu cha wizi. Mtu fulani kaiba, kenda kuficha pahali fulani natoka, nakwenda polisi, natoa taarifa pahali fulani pameibiwa, lakini aliyeiba fulani na vitu kaficha pahali fulani.

Kwa hivyo, mimi nawaachia polisi wafanye kazi ya kufuatilia tena sina masharti mengine, sharti langu labda nitatakiwa kwenda Mahakamani kutoa ushahidi. Hapa mtoa taarifa kuanzia kifungu cha 13-17 masharti mengi sana na katika mswada ule wa mwanzo niliousoma kabla ya kupewa huu, ilikuwa inaelezea kwamba mtoa taarifa aziweke taarifa zake kwa muda wa miaka 10. Mhe. Spika, nilikuwa najiuliza tena huyo ndio anatoa taarifa au amekuwa yeye ndio afisi ya kuweka hizo kumbukumbu. Pale nilisema ikija hii nitasema hapa basi atafutiwe na *laptop* ya kuweza kuweka taarifa.

Mhe. Spika, lakini masharti ya mtoa taarifa yako mengi sana, labda sijafahamu maana ya mtoa taarifa, Mhe. Waziri atakuja kunielekeza. Lakini haya yote ndio ya mtoa taarifa kama nilivyofahamu mimi basi Mhe. Spika nina wasi wasi kwamba sheria hii huenda isifanye kazi. Kwa sababu watu wataogopa kutoa taarifa kutokana na masharti magumu yaliyokuwemo humu ya mtoa taarifa.

Mhe. Spika, nafikiri kina Mhe. Ali Suleiman Ali wameshajiandaa hivi sasa.

Mhe. Spika, jengine ambalo nimeliona humu lakini sikujua kifungu gani kinachosema sheria kupitishwa na Bunge. Kwa mujibu wa mswada huu kwamba sheria ikishapitishwa na Bunge ina maana itatumika Zanzibar. Lakini sisi tunasema hapa sheria yoyote inayopitishwa na Bunge basi iridhiwe na Baraza la Wawakilishi. Mhe. Spika, hapa sikuona kwamb itaridhiwa na Baraza la Wawakilishi, ningeliomba kidogo Mhe .Waziri akimjibu Waziri Kivuli itakuwa amenijibu na mimi kwa sababu suala hilo Waziri Kivuli ameliuliza vile vile lakini yeye amelichambua vizuri sana. Mhe. Spika, kwa kuwa yeye amelichambua vizuri sana mimi naliuliza kwa ufupi kwa sababu kidogo kanuni zetu zinatukataza tusirudie yaliyozungumzwa tukayasema tena.

Mhe. Spika, jengine ambalo limenivutia katika mswada huu ni kwamba kutakuwa na kitengo maalum cha kushughulikia masuala haya. Mhe. Spika, kama nilivyozungumza katika mswada ule wa madawa ya kulevya, kama tunataka ufanisi wa shughuli zetu hizi kwenye hii pesa haramu na hata kwenye ule mswada wa kusafirisha madawa ya kulevya lazima tuwe na vitengo ambavyo wakati wowote watakuwa na kazi hii ya kushughulikia masuala haya.

Mhe. Spika, ikiwa hatukufanya hivyo inawezekana kwamba sheria hizi tutazipitisha, Mhe. Rais ataridhia, Waziri ataunda kanuni lakini zisifanye kazi vizuri. Ndio mimi nikasema lazima kila mmoja wetu ajifunge mkaja katika kusimamia na kuhakikisha kwamba haya matatizo ambayo yameingia katika dunia yetu, basi tunayasimamia vizuri na tunahakikisha kwamba katika nchi yetu ya Zanzibar tunaweza kuyadhibiti vizuri.

Mhe. Spika, kama nilivyotangulia kusema kwamba mswada wa mwanzo nilikuwa na mambo mengi lakini kamati imenifilisi kwa zile *point* ambazo nimeziona, kwa kweli zote zimefanyiwa marekebisho, nawapongeza sana na nawaomba Waheshimiwa Wajumbe tusikae kimya tuuchangie mswada huu na hatimae tuupitishe ili tuipe serikali nguvu ya kuweza kusimamia sheria hii. Mhe. Spika, naunga mkono mswada huu mia kwa mia na nakushukuru kwa kunipa nafasi hii wala hukunikamatia. Ahsante sana.

Mhe. Ali Suleman Ali: Mhe. Spika, ahsante sana, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha na mimi kusimama hapa mbele ya Baraza lako tukufu kuchangia Mswada huu wa Kufuta Sheria ya Usafirishaji Fedha Haramu.

Mhe. Spika, mimi kwanza naipongeza wizara inayohusika kuona pana haja hivi sasa katika nchi yetu kuleta mswada huu, na hasa tukizingatia kwamba wakati

huu tuliokuwa nao ni wakati wa ubabaishaji wa mambo mengi ambayo yanakwenda kinyume na taratibu za kisheria. Mhe. Spika, fedha haramu lina njia nyingi, na fedha haramu kama ulivyoeleza mswada huu, inapatikana kwa mipango mingi ambayo sio ya halali. Kwa mfano, tumesema mtu fulani anafanya shughuli zake ipasavyo kwa sheria zinazokubalika na nchi, lakini wakatokea wajanja wakafanya ubabaishaji wa kutumia hadaa yoyote wakamnyanganya mali ile na kuipata wao, hiyo kweli itakuwa ni fedha haramu. Mhe. Spika, fedha hiyo kwa kuwa mimi nilikuwa nimekaa tu sina kazi nayo nimetumia mbinu zangu za kimabavu nikaweza kuzipata fedha hizo inakuwa sina uchungu nazo hata matumizi yake yanakwenda haramu haramu, kwa sababu zinatumika kinyume na taratibu zetu za sheria ya nchi.

Mhe. Spika, kila linaloletwa hapa katika Baraza lako hili serikali inaangalia kwa asilimia mia moja kuwa na mwelekeo wa usalama huko mbele tunakokwenda. Vile vile inazingatia sana kwamba haya yanayokemewa yanafaa kufuatwa ili kuhakikisha kwamba mtu anapata fedha kwa njia ya halali inayokubalika bila ya kutokea kwenda kinyume na hali inavyotakiwa.

Mhe. Spika, kumekuwa na udanganyifu mwingi katika mbinu za kupata fedha, kama nilivyosema huko mwanzo. Kwa mfano, kuna magenge mengi yanajiingiza katika biashara isiyokuwa ya halali, na biashara hizo zina njia nyingi ambazo zinakwenda kinyume na taratibu za nchi na pia zinakwenda nje ya mtiririko wa kisheria ambao umewekwa. Mhe. Spika, kwa mfano tunapokaa katika shughuli fulani au serikali imelenga kufanya kitu fulani kwa maslahi ya jamii baadae kukatokea wajanja wachache wakapata fungu la pesa ambalo halimo katika kisheria. Hiyo pia ni haramu.

Kwa hivyo, mimi namuomba Mhe. Waziri hili aliangaliwe na ijulikane kwamba fedha haramu hazikiwi katika nchi yetu. Mhe. Spika, kwa mfano serikali imelenga kujenga mradi wa maji sehemu Fulani, au inaelekeza barabara sehemu fulani na mambo mengine ya jamii kwa mfano tumelenga kutumia bilioni tatu, lakini wakatokea wajanja katika mtiririko ule ule wakasema kwamba sisi tunakubaliana kuwa mkataba wetu ni bilioni na sisi tupate chetu milioni mia mbili. Hiyo ni fedha haramu namuomba sana Mhe. Waziri watu kama hawa wanaohusika na mambo kama hayo wakipatikana wachukulie hatua zinazofaa ili kuondoa hii kasoro ambayo tunaizungumza hapa leo.

Mhe. Spika, kuna wenzetu ambao wamejiandaa na mambo ya mbinu za udanganyifu. Na udanganyifu huu wanautumia kwa uwezo wao. Kwa sababu mtu au kikundi cha watu kinaweza kumuendea mtu fulani ana duka lake na amejiimarisha vizuri, lakini mtu yule kwa bahati mbaya akaingizwa katika mtego ambao hakuutegemea, ilimradi akubaliane na matakwa ya wale watu

halafu wao wafaidike na fedha waondoke bila ya kufahamika. Kwa hivyo, Mhe. Spika, fedha haramu haitumiki hapa tu, inatumika sehemu nyingi katika jamii yetu na ndio inayoleta utata.

Mhe. Spika, kudhulumu chochote pia ni fedha haramu. Kwa hivyo, tunapozungumza kusafirisha fedha haramu sio lazima fedha ile iwe inasafirishwa au inaingia nchini kwetu kutoka nje. Lakini ndani ya taasisi zetu ikiingia fedha yoyote kinyume na taratibu basi na hiyo ni fedha haramu. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri jambo hili liangaliwe ili kuhakikisha maeneo haya ya kupitisha fedha haramu yanaondoka katika sehemu zote ambazo zinajitokeza.

Mhe. Spika, hivi sasa kuna wataalamu wengi sana wa mambo ya fedha na wakati mwengine watu wanatengeneza fedha zao kwa njia ya haramu wakawatumia watu wetu humu mitaani na wengine wanajuulikana. Mimi ningeiomba sana serikali hili nalo liangaliwe, kwa mfano mimi siwezi kutoka na safari zangu akaja mtu akaniambia Mhe. Shihata kuna jambo hili na hili bila ya kumtambua mimi nitamwambia sio kweli.

Hili ni sawa sawa na muuza madawa ya kulevya anapoleta mzigo wake basi anam-*point* fulani kumpa dawa zile anakuwa ameshamjua kwamba huyu ndiye mtu wangu na atanisaidia katika kazi zangu. Kwa hivyo, fedha haramu inaanza na mimi niliyepewa mzigo mdogo lakini mletaji mkuu itakuwa nimemficha, basi itakuwa hatumpati. Kwa hivyo, mimi ningeomba sana kwamba mtu akigundulikana na fedha haramu basi achukulie hatua.

Kwa hivyo, mimi naiomba sana serikali huyu tusimpe mwanya na tusiridhike na maneno haya kwamba mimi nilipewa mtu sikumjua. Hapa pana mchezo ambao una maelewano, namuomba Mhe. Waziri hii ni katika njia moja wapo ya kuwasaka na kuwapata hawa waletaji na wasafirishaji na watengenezaji wa fedha haramu tunaweza tukawapata hapa.

Mhe. Spika, uhalifu umeenea kwa njia mbali mbali na uhalifu una mambo mengi, na watu wanapata fedha nyingi kwa uhalifu wanaotumia silaha, wanaotumia mapanga, wanaotumia marungu, wanaovunja nyumba za watu ndio moja katika uhalifu. Mhe. Spika, mimi nataka niseme kwamba asilimia kubwa ya nchi yetu ya Wazanzibari tunajuana na asilimia kubwa ya nchi yetu tuna bahati hata ule usemaji wetu unalingana. Kwa mfano, mtu wa Bwejuu, Jambiani, Makunduchi, Uroa lugha zetu zinakwenda sambamba, hata tukifika Tanga wakati mwengine kuna msemo huo nikifika pale shemeji zangu wanazungumza lugha utaondoka hapo hujapata kitu chochote. Kwa hivyo, kama hapo akitokea mgeni ni rahisi kujuulikana kwa sababu ya lugha.

Mhe. Spika, mimi nataka niseme kwamba hawa wahalifu wanaowatumia watu hawa kwenye maeneo tofauti, mtu hawezi kutoka Nungwi akenda Makunduchi moja kwa moja bila ya kumtumia fulani mpaka akafanikiwa uhalifu wake. Pia huwezi kutoka hapa ukasema nakwenda kwa baba mkwe wangu kule Mtambwe, ukifika tu hutakwenda kupata lolote bila ya kumpata yeye au anayehusika na ile Mtambwe wenyewe ndio utafanikiwa na ulilokusudia. Mimi naiomba serikali maeneo haya kwanza tuangalie huu uhalifu unatokea watu kunyanganywa fedha, kuibiwa mamilioni, kuvunjiwa majumba hasa uhalifu huu unaanza na nini.

Mhe. Spika, hilo nakuliabana kwamba ndio fedha haramu inamopatikana na fedha haramu ile ndio inaleta utata mwingi kumuona mtu siku mbili tatu unamshangaa kwa maisha yake yalivyokuwa mazuri. Kumbe ndio ana kazi ya uhalifu tu. Mhe. Spika, haiwezekani usikie pahala fulani pamevunjwa na zimeibiwa fedha nyingi, fedha hizo kuwa ziondoke tu hivi hivi bila ya kupatikana watu hao, lakini wanajua tu kwamba madhali tumefuatana na mwenyeji wetu, basi tutarudi pale salama, tutaingia ndani tulale asubuhi, tunatoka tunakwenda zetu na mashaka hakuna. Kwa hivyo, ningeiomba serikali itoe elimu juu ya kuhakikisha kuwa wizi wote au hatua yoyote ya kuhakikisha upatikanaji wa fedha haramu unaanzia mikononi mwetu tutoe taaluma ambayo wananchi wetu wataifahamu.

Mhe. Spika, huu mswada ni mzuri na hasa tukizingatia kwamba, kama taaluma itatolewa vizuri kwa wananchi wetu basi umuhimu na uzuri wake utafahamika. Lakini kama utaishia hapa tu katika Baraza na wananchi kupata dakika mbili tatu tunazozitangaza hapa utakuwa bado haujafika na hautokuwa na malengo ya kufikisha tulikokusudia.

Mhe. Spika, wenzetu nje kuna mitambo ya kutengeneza fedha na fedha hizo ndizo zile zinazopelekwa katika zile nchi changa kama yetu, fedha hizo nyingi sana. Mimi siku moja Mhe. Spika, nililetewa bunda la fedha nyingi tu, lakini sizijui. Sasa fedha zile nilipoletewa nikafikiri labda yule mwenyewe anataka nikambadilishie kumbe kaja kusikitika tena analia, nikamuuliza nini mwananchi wangu? Akanambia Mheshimiwa hizi pesa nimepewa katika vituo vinavyobadilishwa pesa kumbe pesa sizo. Hiyo sehemu siitaji lakini ipo, nikamwambia mimi nina mashaka na wewe haiwezekani hata siku moja upewe pesa zinazofika dola elfu kumi unambie kwamba ulipewa na *Bureau de change* fulani si kweli, labda kuna kitu wewe hutaki kukisema hebu nambie ukweli. Akanambia mheshimiwa niamini ni kweli.

Mhe. Spika, kidogo kilichonitia hofu yule kijana wangu ustadh tena ustadh kweli kweli. Sasa manung'uniko yake aliyonipa yale nikamwambia twende mimi na wewe, mimi ndiye kiongozi wake na mimi nikifika pale nitataka

ukweli kama ulivyonieleza wewe nay eye huyo nitataka aseme ukweli. Tukatoka tukenda, tulipofika pale mwenye *Bureau de change* ile tunafahamiana nikamwambia nimekuja huyu kijana wangu kanijia siyajui mwanzo wala mwisho, lakini nataka ukweli kwa sababu kuna mchezo ambao mimi siufahamu, ana dola zake elfu kumi hizi hapa anasema dola hizi kapewa katika *Bureau de change* yako na bahati nzuri kakukuta wewe kakutaja kwa jina.

Mhe. Spika, akanambia mheshimiwa mimi wewe tunaelewana toka enzi, tangu unauza kamba wakati huo sio sasa hivi, unakuja ukichukua mamilioni kwangu mimi kisheria lakini sio kwa njia ya haramu, nabadilisha. Kwa sababu *Bureau de change* zimekubalika zina leseni na kila kitu, na nikienda kubadilisha mpaka nipewe risiti ndio niridhike, kwa sababu ikitokea hitilafu yoyote najua namkamata yeye na ushihidi nitakuwa ninao na ndio utaratibu wa kisheria na fedha halali inavyokwenda.

Mhe. Spika, sisi tunafanya mambo ya mchezo sana wakati mwengine hatujifahamu, lakini kwa wenzetu ukiibadilisha dola moja unapewa risiti nchi za wenzetu za Kusini mwa Afrika, dola moja ile unapewa risiti ile ni msingi wako wa usalama wako, lakini kama unapewa dola elfu kumi wee unakwendazako useme ahsante nimeridhika huna maana, wala sheria ya fedha halali au haramu huijui inavyoingia na kutoka.

Kwa hivyo, nikamwambia yule mwenye *Bureau de change* nakuomba unipe ukweli tu, hii fedha mimi sikuelezi kwanza nitakueleza baadae nipe ukweli kwamba je, kweli umempa? Akanambia si kweli, huyu kaja na dola zake 200 nikamwambia dola hizi sizo akatoka akendazake, nikamwambia hii ndio faida ya kutumwa ukatekeleza utumwa mbele ya wewe mwenyewe. Kwa sababu ningekuja mimi ndio ungenambia nimezungumza vyengine lakini mwenyewe nikamhakikishia. Mimi nilimwambia mapema siamini kuna mchezo hapa hutaki kuutaja.

Sasa Mhe. Spika, mimi kutoka pale jamaa yule jamaa mwenye *Bureau de change* kwanza nikampongeza na nikamwambia mimi nina risiti nyingi tu ambazo hupewa nikichenjisha hizi hapa ikiwa dola moja au zaidi, wewe dola elfu kumi usichukue risiti? Si kweli. Nikamwambia kuna mchezo lakini leo utanieleza. Mhe. Spika, jamaa jasho lilimtoka mwisho akanambia ukweli wake kwamba hizi pesa nililetewa, sasa nikamwambia kama ulileteWa twende polisi ukazipeleke polisi na itafanya kazi yake na wewe itabidi uisaidie polisi. Mhe. Spika, jamaa alilia jasho linamtoka yumaji. Nikamwambia basi maamuzi yangu ya mwisho mimi uyachome mbele yangu, Mheshimiwa dola elfu kumi akazichoma hadharani na mashahidi wapo.

Sasa hii kujua kudhibiti na kusaidia fedha haramu inavyoingia katika nchi na jinsi gani ya kuisaidia serikali ili fedha ile isitapakae kwa wananchi wetu ambao hawaifahamu ikawaumiza.

Mhe. Spika, fedha hizi si fedha za kigeni tu kutoka nje, halkadhalika pesa zetu za Tanzania hivi sasa unaikuta shilingi elfu kumi mpya unaamini hasa hii ni elfu kumi, lakini pesa hiyo ukitoka dakia 10 au 20 mpaka nusu saa ishayayuka kwanza inakuwa si pesa tena, lakini pale ukipewa utaamini hii inatoka *BOT* sasa hivi. Sasa ningeiomba serikali na Wizara ya Fedha na Uchumi au benki zetu wakatoa taaluma za kutosha.

Wizara au benki zinajitahidi kuelimisha wananchi lakini mara nyingi wananchi wetu huwa hawafikii pahala wanasahau upesi. Mwananchi akija kushituka anakuja kusema aa, katika pesa zangu shilingi 50,000 mna shilingi 10,000 imepachikwa siijui au atapokwenda dukani. Wenye maduka wengi siku hizi wameamka anakwambia hiyo sio, kwa ghafla mimi na wengine hapa pamoja na wananchi wetu huwezi kuijua.

Kwa hivyo, niseme kwamba fedha haramui zimo katika nchi yetu na fedha haramu zinatengenezwa kwa wingi lakini serikali nafikiri na wananchi tuwe kitu kimoja ili kuhakikissha kwamba wananchi wanatoa taarifa wanapomuona mtu anakwenda kinyume na utaratibu au anatumia pesa isiyokuwa ya halali, tukiwaachia hapo basi mtiririko huu Mhe. Spika, utakuwa mkubwa na utaleta maafa katika nchi yetu.

Mhe. Spika, wananci wetu wanyonge sana na wanaitegemea serikali pamoja na sisi Wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi tuliomo humu ndio serikali yenyewe tuwasaidie angalau kuwaelekeza au kuwasemea kama hapa juu ya athari za pesa haramu. Tusifikirie pesa tu inayosha kwamba fedha haramu madhali nimekosa kwenye dola au pesa ya Tanzania ndio imekwisha, sivyo. Hata mali inayoingizwa nchini kinyume na taratibu hiyo ni fedha hafamu.

Kwa sababu serikali kwa upande mmoja inakosa mapato yake, yakiingizwa mafuta haramu haya naweza kusema mafuta yaliyonunuliwa nje yamapita hapa bila ya kulipiwa ushuru, serikali inakosa mapato yake kutokana na huo mdumo uliopo, lakini niishukuru serikali hivi sasa kwa asilimia kubwa mchezo huu umepungua kidogo, naweza kusema kidogo kwa sababu sasa hivi ushindani ya biashara ya mafuta au katika maeneo ya vituo vyetu vya mafuta basi mafuta yamekuwa mengi na huwa kwa wale wajanja wanaoweka mafuta ndani pia wanaogopa, niseme etu hivi sasa hiai *Alhamdulillah* wimbi hili kidogo ilimepungua na serikali kuweka mkakati mzuri kusema kwamba kila kinachopatikana kinyume na taratibu kikamatwe.

Mimi hapo naishukuru serikali na ninamuomba sana Mhe. Waziri wenzetu wanaohusika na masuala hayo waongeze bidii juu ya kuhakikisha kwamba pato letu la mafuta halendi nje ya wanaotumia unununzi haramu.

Lakini pia Mhe. Spika, bidhaa, serikali ijitahidi sana kuhakikisha kwamba bidhaa zetu zinazoingia katika nchi yetu zinakuja kisheria na zinaingia ndani kisheria na kulipiwa kodi kisheria. Ukilipia kodi kisheria ndio pato la nchi la halali linapatikana pale na muuza biashara yoyote anakuwa fedha yake anaipata kihalali.

Mhe. Spaika, kwa wale wengine ambao wanaingiza bidhaa kinyume na taratibu pia ni hao hao ambao wanaleta hatari katika maeneo yetu ya kueneza fedha haramu. Nitatoa mfano Mhe. Spika.

Kama mimi naleta nguo na vifaa mbali mbali vya matumizi katika majumba, lakini kule nilikovipata sikulipia chochote nimefanya mipango yangu ya juu juu tu, sasa atapokuja mfanyabiashara yule anauza anavyotaka hana hasara. Kwa sababu katoa kule kaingiza hapa bila ya kulipia chochote au katumia hadaa au njia ambayo si ya halali. Njia hiyo kusema bidhaa ile kule kaipata kwa njia za kienyeji, hapa katoa kienyeji, sasa na ile anayoitumia yeye ni fedha haramu. Inafaa serikali iangalie na wanaopatikana wachukuliwe hatua za kisheria ili kuhakikisha kwamba serikali inapata chake kwa maslahi ya wananchi wake, na mfanyabiashara anapata chake kwa mujibu wa taratibu ambazo wamejiwekea.

Mhe. Spika, ikiwa tutaweka mkakati mzuri na tutakuwa na msimamo naamini hakuna litaloshindikana, serikali imeitwa serikali kwa sababu siri yake ni siri kali. Mtu anayeifanyia masihara serikali mimi humshangaa sana, kwa sababu serikali ni serikali tu, serikali ndio sisi sote, sasa wewe una mambo yako ya kienyeji unayotaka kufanya mwenyewe kinyume na taratibu *Wallahi* itakukamata, kama tuna mwelekeo wa kweli.

Kwa hivyo, ndio nikasema katika mswada huu mna kitu ambacho nimekipenda sana, lazima pawe na zawadi kwa mtoa taarifa na zawadi ile iwe ni kielelezo tosha kwamba huyu mtu kafanya hili kwa siri na tumempa zawadi kwa siri. Naiomba serikali isimtangazie, itoe kwa siri lakini tu inaweza kuitangazia jamii kwamba, serikali leo imetoa shilingi milioni kumi mfano tu huo, kutoa zawadi kwa kudhibiti kukamata mali ya shilingi bilioni moja au bilioni mia tatu. Naamini Mhe. Spika, changamoto hiyo itatokea na wananchi watakuwa tayari kufika katika vituo ambavyo wataelekezwa kuhakikisha kuwa mtu akiliona hilo atoe siri pahala panapohusika.

Mhe. Spika, hayo yatawezekana, kuwezekana huko serikali kutoa taaluma ya kutosha na kuwaelekeza wananchi wake kuhakikisha kwamba haya yote tunayoyazungumza au kuyaelekeza yanafanyiwa kazi ipasavyo.

Mhe. Spika, kuna nchi za jirani za wenzetu wamepiga hatua kubwa sana za uchumi katika nchi zao. Tunaamini ukienda kubadilisha shilingi 500 ikiwa ya nchi ile ama ya nchi jirani mpaka mfano kama wenzetu wa Kenya, Uganda ndio jirani mwema hao, ukifika pale unabadilisha shilingi 500 unaambiwa kaa hapo kitako, *Bureau de change* anakwambia kaa kitako, hujui unakalia nini siku nyengine unapewa na kahawa kama unapenda au *juice* kunywa hii unawashiwa mtambo pale pale paa, pale pale unaijua kama pesa hii *fake* au si *fake*.

Kwa sababu katika nchi hatari kwa pesa za haramu wenzetu Uganda. Mhe. Spika, Uganda kuna hatari sana, lakini kila *Bureau de change* ina mtambo wake, fedha unaiona mpaka yale mambo yake ya ndani yote, anakuwekea ile uliyoipeleka na ile pesa haramu kisha anakwambia linganisha hii haramu hii sahihi. Kwa hivyo, ningeiomba serikali ili kuhakikisha haya nayo yanapatiwa nguvu pamoja na juhudi ya kuiangalia kwa macho tu, lakini mitambo midogo midogo iwepo. Niiombe serikali fedha zote zinazobadilishwa katika maeneo yetu ya ubadilishaji wa fedha hata wenye maduka makubwa pia si vibaya nao kuweka mitambo hiyo ambayo si ya gharama kubwa, ngarama yake ni ndogo na inasaidia kuingiza fedha haramu katika nchi ile au kutoa.

Mhe. Spika, jengine ambalo nimeligundua katika mswada huu, kuna maoni mbali mbali ambayo yametolewa. Kwa bahati nzuri au mbaya mimi nimeuza mzigo wangu lakini bahati mbaya mzigo ule sikutoa ushuru yaani nimeuuza sikuchukua risiti. Kwa mfano, nimepeleka karafuu zangu *ZSTC* kama gunia mia nne au mia mbili, nimechukua mamilioni yangu nimeondoka nimekwendazangu. Nimezungumza neno moja kubwa sana Mhe. Spika, nimechukua Shirika la Serikali makusudi kuonesha mfano kwa wengine. Sasa nikalipwa shilingi milioni 6 mpaka 7 nikatoka nikenda zangu, kumbe ndani ya fedha zile mna fedha haramu. Kwa sababu ukiwa pale unahesabiwa mbio mbio unakwenda zako hujui kitachokutokea mbele.

Kwa hivyo, mimi bado tatizo langu lipo pale pale Mhe. Spika, ikiwa katika vyombo vya serikali, mashirika ya umma, maidara, katika tasisi yoyote ya fedha, lakini ningependelea zaidi katika mashirika ya umma na wafanyabiashara wakubwa wakubwa, hata wa kati wakatumia uwezo wa kukabidhi stakabadhi ambazo baada ya kupata malipo unakuwa nayo inakuhalalishia kuwa likitokea tatizo unaweza kuja kusaidiwa kutokana na ile stakabadhi uliyokuwa nayo. Vyenginevyo Mhe. Spika, ni hatari.

Nimuombe Mhe. Waziri narudia ile ile ya mwanzo sio mbaya, lazima tuhakikishe kwamba taratibu zetu zinaendeshwa vizuri na zinalipiwa kutokana na utaratibu wa kisasa. Bila ya kulipa fedha kutumia risiti ni hatari, unaponunua unapewa risiti na unapouza pia upewe risiti ndio sawa sawa. Kununua kitu dukani na kuuzia duka lile lile kubwa upewe risiti, vyenginevyo italeta athari baadae.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nitalizungumza ni madhumuni. Kama ulivyoeleza mswada huu madhumuni ni mazuri na yameelezea mambo mengi. Kwa sababu kuna sehemu ambazo zimeeleza mambo ya faini, kuna sehemu ya mali kutaifishwa. Mimi niseme tu kwamba faini iliyowekwa kwa mambo haya si mabaya sana, lakini serikali ingeweka uwezo zaidi. Kwa sababu faini ni suala moja kubwa na ni suala ambalo litaleta vitisho kwa hawa wengine wanaoingiza fedha haramu katika nchi yetu.

Kutaifishwa sehemu ya kwanza na faini ni sehemu ya pili. Kwa sababu unaweza kutaifisha mali siku nyengine haina thamani yoyote lakini madhali haramu ni haramu, pamoja na kuitaifisha ile mali kidogo lakini ukimpa adhabu ikawa kubwa sana. Mhe. Spika, kwa sababu hakuna kosa dogo wala kubwa, kosa ni kosa tu. Tunaambiwa kwamba thawabu yoyote ni thawabu ukitoa shilingi mia moja utapata thawabu, ukitoa milioni moja utapata thawabu. Kwa hivyo, na adhabu yoyote ya kosa ni kosa tu, lakini na faini vile vile kusiwe na faini ndogo. Kuwe na faini ambayo itasaidia kuondoa kabisa tatizo hili katika nchi yetu na kuhakikisha kwamba mchezo huu unaondoka katika nchi yetu.

Mhe. Spika, niseme tu kwamba bado tumo katika mazingira magumu na bado taaluma yetu ni ndogo na naamini wenzetu watajitahidi mswada huu unapitishwa, lakini bado wananchi wetu wanafaa kupewa taaluma siku hadi siku kujua athari za uingizwaji wa fedha haramu. Usafirishaji unatoka ndani uletwaji unatoka nje.

Mhe. Spika, niseme tu kwamba mwananchi aelewe fedha ndio kitu tosha ambacho kinasema fedha hii ndio iliyopatikana kwa njia haramu, lakini bidhaa pia ikiingia kwa njia ya haramu nayo ijulikane fedha haramu zilizoingia katika nchi yetu.

Mhe. Spika, kuna chakula kinachoingizwa nchini au bidhaa mbali mbali za matumizi ya wananchi wetu ni kwamba zinaingizwa kinyume na taratibu. Kwa mfano, dawa wa meno, majani ya chai, vyakula vya makopo, tende zote zinaingizwa kwa njia haramu. Bidhaa hizi zikiingia hapa zinakuwa haramu kwa sababu kwanza zinakotoka zimeshaharibika. Kwa hivyo, madhali zimeshamaliza muda wake zikiingia hapa muuza biashara ile hana hasara tena. Mimi nitatoa mfano mwengine ambao ni wa halali kabisa.

Mhe. Spika, mimi mara nyingi nikitaka kununua kitu ikiwa nimemtuma mtoto au nimeshuhudia mimi mwenyewe basi yule mwenye duka huwa simuachii. Simuachii kwa njia mbili ambazo nitazieleza hapa, haiwezekani dawa kubwa ya meno, *colgate* unamtuma mtoto dukani anakwambia shilingi 1200, sasa wewe uliyemtuma yule mtoto uwe na tahadhari nae, kweli hii ndio bei yake? Yanatokea, yamo na yanatugusa.

Mimi kwa upande wangu huwakamata wenye maduka lakini huwa sitaki pesa haramu kwa kunipa kitu aa, mimi namwambia la mwanzo naweza kukupeleka panapohusika hutaki unaona utakwenda kupata adhabu na ni lazima adhabu upate basi nataka uziharibu hapa hapa mbele yangu. Pia ile ni kusaidia jamii yetu kuhakikisha isiingie katika maradhi ambayo yanahusiana na mambo ya tamaa zetu.

Hivi sasa kuna *kits* nyingi za *colgate*, unazikuta mpya, nafikiri zilikuwa *store* kwa muda mkubwa huko nyuma, lakini ukiangalia *expire date* inakwambia hii inamalizika mwaka 2020. Hee, mimi sijasikia lugha hiyo Mhe. Spika, utoke leo mwaka 2009 mpaka 2020 kiwanda gani kinachoweza ku-*control* mambo hayo kisilete uharibifu. Kwa hivyo, ukikuta mambo kama hayo tuhakikishe kuwa hili eneo si salama. Tunachotakiwa sisi kama wabunifu wa mambo yale tusaidie serikali kwa njia tunayoiweza na kuhakikisha kwamba hii ni haramu ambayo wanaitumia na kupata fedha kinyume na taratibu, lakini pia anawatia maradhi wananchi kwa jambo ambao halina msingi. Msingi wake kupata shilingi elfu 10 au 20 lakini anaharibu afya za watu na kuleta athari na uharibifu wa fedha za umma kwa matibabu ya mtu yule.

Kwa hivyo, niiombe serikali kupitia vitengo vyetu mbali mbali kwa sababu fedha haramu inaingizwa sana kwenye biashara, basi Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi aende sambamba sana na Mhe. Waziri wa Utalii, Biashara na Uwekezaji, kwa sababu huko ndiko chimbuko la mwanzo linakotokea suala hili. Naamini kama tutakuwa na mpango mzuri wa kufuatilia maduka, sio huku mjini tu, kwa sababu mjini kuna wajanja wengi, lakini tuelekee ng'ambo. Mimi mambo yangu mengi husema tuelekee huko ng'ambo.

Mhe. Spika, matatizo yako ng'ambo si mjini, huku watu wengi chuo kikuu kule kwetu *Form VI*. Wafanyabiashara wengi huku wanaogopa, lakini ng'ambo ndio wanakotumia ule mtiririko kauze huko, wape wale hata wakifa basi. Hayo yamo na nimuombe sana Mhe. Waziri lazima ziara zifanywe na kitengo chetu na si vibaya kupitia polisi. Kwa sababu ni vyema kama nilivyoeleza mwanzo aliyepewa pesa haramu ukikamatwa wewe ukimtaja aliyekupa ndio tunaanza kuuwa lile shina, tunalitafuta na tunalipata na tukiliuwa shina matawi yanatawanyika.

Halkadhalika na hawa wauza biashara wajanja maghala yao yote yako huku mjini, kwa sababu wafanyabiashara hao wako huku mjini. Lakini tukiwakamata wale wa ng'ambo wakasema mimi kanipa fulani kule mjini akija kushikwa basi tunahakikisha mtiririko mzima wa uendeshaji wa fedha haramu utatoka katika nchi yetu, vyenginevyo bado tutakuwa na kilio hiki hiki cha muda mrefu ambacho tunaamini kama haikutafutwa dawa madhubuti basi haipatikani.

Juzi tulizungumza katika mswada wa madawa ya kulevya tukasema kwamba katika watu wanaopata fedha haramu kwanza tuseme majambazi, lakini pili madawa ya kulevya. Mhe. Spika, narudia tena kauli yangu niliyokuwa nimeisoma katika taarifa yangu ya Mwenyekiti katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii juu ya hotuba yangu ya madawa ya kulevya. Nilisema kwamba wafanyabiashara wa madawa ya kulevya ni watu hatari. Kwa wenzetu wa nchi za nje ule uharamu wao ndio maana wanamiliki majeshi, silaha nzito, ndege kubwa kubwa, mashamba makubwa, hii yote kuhakikisha kwamba haramu ile inazaa haramu.

Mhe. Spika, bahati nzuri wewe ni jaji au ulikuwa jaji au hakimu. Mhe. Spika, maana nikisema daktari basi daktari, lakini unaweza kuwa jaji au hakimu, vyeo vyenu unavijua wewe nakuelekeza wewe. Unapotoa hukumu unasema namlenga fulani kwa kosa fulani, kwa hivyo, lile kosa ulilolifanya ile haramu yake ndio unapata hukumu. Kwa sababu kuna uharamu na uhalali, hakwenda kwenye makosa anapata halali, kafanya makosa anapata haramu ile ambayo kapewa kwa kosa lile ambalo limekubalika kisheria.

Mhe. Spika, hawa wenzetu wanavyofanya madhali fedha kaipata kiharamu ataitumia haramu kwa uwezo wake aliyokuwanao. Kwa mfano, mimi nina wafanyakazi wangu na sehemu ya kampuni au kampuni ya mtu fulani, nawalipa wafanyabiashara hawa shilingi laki tano kwa mwezi kila mfanyabiashara mmoja, ukimwambia hama hapa nakuhamisha njoo uchukue shilingi milioni tatu kwangu basi hapo ujue pana kitu. Kwa hivyo, ile haramu huzaa haramu. Sasa na yule akishapata ile haramu aliyoipata kinyume na utaratibu basi na yeye anatafuta haramu nyengine kuiendeleza. Kwa sababu atatumia vyengine na yeye keshakuwa na uwezo.

Sasa fedha hizi za madawa ya kulevya ndivyo zilivyo, hizi zinakwenda kutokana na msingi kwamba mtu kazipata huko hana wasi wasi anakutumikia.

Mhe. Spika, wengine juzi walisema hapa halafu mimi ikanijia ghadhabu na mimi nikasema baada ya wananchi wangu kuniuliza kuhusu mswada ule. Hii adhabu ya miaka 30 mbona ndogo, kwani si pana maisha hapa? Nikasema

tumefanya marekebisho. Basi tunakuomba kama Mwakilishi wetu wa jimbo iwe kifungo cha maisha ili kulikomesha au kuliondoa kabisa suala lile.

Kwa hivyo, niseme ikiwa mimi Ali Suleiman Ali nimezaliwa tarehe 6 Machi, 1955. Na ndivyo ilivyo, hiyo ndio tarehe wazee wangu wamenizaa na popote ilipo hii inajulikana hivyo, pia wanangu wanajua mimi baba yao nimezaliwa tarehe hiyo. Lakini nikafanya mimi nimefanya njia ya udannganyifu kwenda kutafuta hii tarehe 6 Machi nikaifanya mwaka 1965 badala ya 1955, natafuta nini, uharamu.

Mhe. Spika, hapa pana mchezo unachezwa mtu kutafuta kughushi, kuiba, kuongeza muda, alimradi tafrani. Mhe. Spika, ningeiomba serikali nyanja hii yote iangaliwe udanganyifu huu tuliokuwanao tuutazame kwa upeo wa mbali tusiuangalie karibu tu. Mhe. Spika, mimi nakuhakikishia kama kweli na ndivyo ilivyo maana usingeletwa mswada huu, serikali najua ina nia njema na naamini hilo. Lakini naiomba serikali yetu hii mswada unaoletwa hapa uwasaidie wananchi wetu na jamii kwa jumla na uwe na msimamo madhubuti kwa kuendeleza nchi yetu na kuondoa udanganyifu wa mambo mbali mbali ambayo yanakwenda kinyume na sheria ya nchi yetu. Ufanye kazi vizuri na kuhakikisha kwamba maslahi yanaonekana kwa faida ya wananchi wetu.

Mhe. Spika, hili linawezekana na kuwezekana itolewe taaluma kwa wananchi. Mhe. Spika, sioni tabu kurudia. Kwa sababu wananchi wetu hawapati muda wa kusoma hii sheria wala hawaipati, wala hawaioni, wala hawajui maana yake nini, sawa sawa na Katiba. Mhe. Spika, katika nchi yetu hapa wengi tunavunja Katiba kwa kutokujua wajibu. Kiongozi mfano mimi au mwengine anaweza kutumia uwezo wa cheo chake kwenda kinyume na taratibu zake, mchezo mchafu ule unaitwa haramu, kwa hiyo pia uangaliwe.

Mhe. Spika, nasema mswada huu ni muhimu sana na ninahakikisha kama Mwenyezi Mungu atatujaalia na *inshaallah* kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu atatujaalia mswada huu ufanye kazi, lakini usimamiwe vizuri kwa manufaa ya nchi yetu na vizazi vyetu, basi mabadiliko ya nchi yetu yataonekana. Tusiwe na mianya ya kupenyeza, tusiwe na mianya ya kutoa, tuhakikishe kwamba hapa tulipo tunadhibiti kisiingie wala kisitoke kwa njia yoyote, kuanzia fedha, bidhaa na mambo mengi ya kughushi. Kwa sababu kughushi kuna mambo mengi Mhe. Spika, haya nazungumza kama mengineyo lakini ndio hayo hayo.

Mhe. Spika, tuliambiwa zamani kuna mchezo mchafu unachezwa katika baadhi ya maeneo shilingi elfu kumi inafanywa laki moja, shilingi laki moja inafanywa milioni moja na milioni moja inafanywa milioni kumi. Mhe. Spika, wajanja hao wapo, kwa hiyo fedha haramu inaanzia humu humu, hata ikitapakaa humo tena

ndio watu wanaeneza kwa ujuzi wao na kuhatarisha usalama wa wananchi wetu na maisha yao.

Mhe. Spika, inapofikia hatua hii dunia inatuelewa na dunia itatuelewa vyema kwa sababu Tanzania au Zanzibar umewekwa mswada huu wa usafirishaji na uingizaji wa fedha haramu kuwa unapigwa marufuku katika nchi yetu. Kwa mfano, kifungo cha maisha kama kitakuwepo ni kizuri zaidi na faini ikaongezwa ikawa kubwa zaidi basi hilo litasaidia sana kuondoa.

Mhe. Spika, baada ya hayo niseme tu kwamba mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wote wa Jimbo la Kwahani, naamini kwa kuwa haya nimeyasema Wazanzibari wote watayapata, basi wawe tayari kuyaunga mkono na kuwa na hamu ya kutafuta haya mazingira ambayo tunayoyazungumza hapa kwa maslahi ya nchi yetu. Hapo ndipo tutafanikiwa na kuleta maendeleo na ufanisi katika utendaji wa serikali yetu na wananchi kupata haki ambayo ni sheria haiendi na haramu tunayoizungumza hapa.

Mhe. Spika, naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja na nawaomba wenzangu wote wa pande zote mbili tujitahidi tuuchangie kwa maslahi ya vizazi vyetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Spika, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima na kuhudhuria kikao cha Baraza ili kutekeleza majukumu ambayo tumepangiwa.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuchangia Mswada huu wa Sheria ya Kudhibiti Usafirishaji wa Fedha Haramu na Mapato ya Uhalifu na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, kwanza mimi mwenyewe binafsi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Chaani tunaunga mswada huu ili ukifanya kazi basi utasaidia kuleta maendeleo katika nchi yetu lakini pia kuondoa hii dhima ya usafirishaji wa fedha haramu.

Mhe. Spika, nikianza na mchango wangu katika mswada huu imezungumzwa humu suala zima la ufafanuzi kifungu cha 2 miongoni mwa fedha hizo haramu na zikawa zimetajwa. Kufanya biashara pengine ya dhahabu unapokea hundi ya fedha na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, jengine linazungumzia suala zima la kamari. Mhe. Spika, kwa bahati nzuri kamari imetajwa katika mswada huu lakini pia imetajwa katika

kitabu chetu kitukufu cha *Qur-an* kwamba ni jambo baya na linaleta madhara katika nchi yoyote ile ambayo huu mchezo unafanyika.

Mhe. Spika, kamari inachezwa katika nyanja nyingi. Kwa hivyo, ningeomba Mhe. Waziri akazingatia kuona kwamba katika kuzuia kucheza kamari basi tuzione hizo. Mhe. Spika, mfano mmoja wa kamari ni kwamba kamari inachezwa kwa kutumia karata, yaani wachezaji wanatumia karata aidha za mtu mmoja mmoja na nyengine inawakutanisha makundi ya watu, wanaweka mafungu ya fedha kila mmoja anaunganisha kwa mwengine badala yake anapatikana mshindi kutokana na zile karata wanavyozicheza. Pale wanapata fedha zile wachezaji, sasa fedha hizo nazo vile vile kwa mujibu wa sheria hii maana yake zimo katika mafungu ya fedha haramu. Sasa Mhe. Spika, mimi nataka niseme kwamba tuangalie nyanja hizo zote tuweze kuzidhibiti.

Mhe. Spika, jengine katika mchezo mwengine wa kamari kuna mchezo ambao washabiki wanachukua majogoo kwa mfano, wanakwenda wanayapiganisha yale, katika kuyapiganisha majogoo yale makuchi maana yake kila mmoja anasema jogoo wangu atashinda. Kwa hivyo, wale wanapata washabiki wa pande zote mbili kundi 'A' na kundi 'B'. Sasa pale mchezo unachezwa kwa wale majogoo kupigana hatima yake mpaka mmoja anashindwa aidha kwa kukimbia au anakufa kabisa.

Kwa hivyo, kwanza kama nilivyosema pale vile vile katika kitabu cha Qu-ran inakatazwa, lakini pia na hapa vile vile maana yake unamdhulumu yule jogoo, lakini pia kinachotokea pale kunapatikana fedha zile haramu kwa wale ambao wanashindana huo mchezo.

Mhe. Spika, jengine linalopatikana katika mchezo huu, mimi kuna mchezo nataka niulize kwa mfano huu mchezo wa bahati nasibu. Mhe. Spika, kwa mtazamo wa sheria hii unakuwa wapi? Bahati nasibu inachezeshwa pengine wewe unatoa kwa mfano shilingi laki moja lakini unaweza ukashinda, ukapata milioni mia moja. Je, hii haiingii katika fedha haramu kwa upande wa sheria zetu za kiserikali? Kwa sababu kwa sheria za kidini haikubaliki moja kwa moja.Lakini katika sheria hii tunayoizugnumza hii tunaiweka wapi?

Mhe. Spika, jengine lililotajwa katika sheria hii linazungumzia suala zima la rushwa, yaani mtoaji na mpokeaji rushwa nao vile vile wanaingia katika aidha kupatikana kwa fedha haramu (fedha chafu). Mhe. Spika, moja kwa moja mimi naunga mkono sheria hii na kipengele hiki kwamba hizo fedha ni haramu na tupige vita eneo hilo.

Mhe. Spika, jengine katika hilo hilo suala la rushwa upatikanaji wake na kuzuia kwake. Mhe. Spika, inabidi tujiandae kweli kweli katika kuzuia hizi rushwa.

Kwa sababu watu wanaoshughulika na mambo ya rushwa ni watu ambao wanakuwa na mbinu tofauti kila siku. Kwa hivyo, ili kuweza kumkamata kunahitaji kazi kubwa na kutumia fedha nyingi hadi kupatikana yule ambaye anapokea zile rushwa. Mhe. Spika, njia rahisi zaidi ya kupatikana kwa huyu mtu anayepokea rushwa, basi ni kupata muumini mzuri ambaye aidha ana shida ya kupata jambo lakini jambo lile halipatikani, ila kwamba yule ambaye anahusika moja kwa moja ni mtu ambaye hawezi kutoa haki ila apate rushwa.

Sasa tukipata watu wa aina hiyo au pengine mtu ambaye ni mfanyakazi wa kitengo hicho kama wenzetu kule Bara walivyoanzisha mara nyingi wanawatia hatiani wale wanaopokea rushwa. Kwa sababu kwa vyovyote yule mpokeaji wa rushwa anakuwa na mbinu zake anazozitoa ili wewe uweze kuzitekeleza.
Nafikiri hata katika michezo ya TV unaweza kuona. Mhe. Spika, ile si michezo inayoonesha mfano, lakini ni mambo yanayotokea kweli kweli. Kwa hivyo, kama tutakuwa tunafanya kazi hiyo basi tunaweza tukafanya kazi nzuri ya kuondoa hiyo rushwa na pengine fedha haramu hizo zikakosekana.

Mhe. Spika, jengine ninalotaka kulizungumza na hili, si kwa maana nyengine yoyote isipokuwa kuunga mkono tu kwamba upatikanaji wa Mkurugenzi katika taasisi hii. Mhe. Spika, upatikanaji wa Mkurugenzi imetajwa hapa kwamba lazima huyu Mkurugenzi ambaye atahusiana na mambo haya kwa sababu yanahusiana zaidi na mambo ya fedha basi awe mwenye taaluma ya fani hii ya fedha. Hii sina mashaka nayo na naunga mkono moja kwa moja katika vielelezo vyote ambavyo vimetolewa mpaka anapatikana huyu Mkurugenzi.

Mhe. Spika, jengine linahusiana na suala zima la ugaidi. Mhe. Spika, ugaidi ukiwemo uharamia ni jambo baya sana na linaweza kuiingiza nchi katika umaskini mkubwa sana. Mhe. Spika, tukichukulia mfano ugaidi ule uliotokea tarehe 11 Septemba, laitani kama ingekuwa ugaidi ule umefanyika katika nchi maskini kama zetu basi ungechukua muda mrefu kurejesha hali halisi ya gharama ile iliyopatikana.

Mhe. Spika, si hapo tu, niliona vile vile katika TV India nafikiri ile wamefanya ugaidi. Mhe. Spika, ugaidi una nyanja nyingi maana yake huu ni uhalifu ambao unafanywa aidha mtendaji anatumia kubomoa majumba ama kuyachoma moto, ili kuiingiza nchi ama taasisi fulani katika hasara kubwa. Lakini pia Mhe. Spika, ugaidi unatumika katika kuwateka nyara wasafiri wanaosafiri katika vyombo mbali mbali kwa mfano meli na ndege.

Kwa hivyo, sheria hii maana yake tunapoipitisha pia na sisi kama watu tuliomo katika ulimwengu huu ama Jumuiya ya Kimataifa, basi tutakuwa tumeunga mkono kuzuia matendo hayo. Mhe. Spika, mimi naunga mkono eneo hili kwa

misingi kwamba, tutakapoweza basi tunaweza tukaona tumefanikisha azma ya dunia kuona kwamba inakwenda kwa amani na kuondoa mambo haya maovu.

Mhe. Spika, jengine linahusiana na usafirishaji wa silaha haramu nao pia tunaupiga vita. Kwa sababu silaha haramu ni silaha ambazo zikiingia nchini zinakwenda moja kwa moja kwa magaidi pengine majambazi na watu wengine wanaohusiana na mambo hayo. Kwa hivyo, hawa majambazi wanapozitumia hizi silaha maana yake wanaweza wakenda pengine kwenye mabenki au taasisi nyengine za fedha. Lakini pia Mhe. Spika, hawa wanaweza kwenda katika maeneo ya watu binafsi na kuweza kufanya uhalifu wa kupora fedha nyingi, fedha hizo zinapopatikana maana yake tayari zitakuwa zinaingia katika fedha haramu. Sasa tutakapozuia hili maana yake sambamba na hilo, basi tutakuwa tunaingia moja kwa moja katika kuzuia kupatikana kwa fedha haramu na matumizi yake.

Mhe. Spika, jengine ambalo limezungumzwa ni pamoja na usafirishaji haramu wa binadamu pamoja na uhamiaji haramu. Mhe. Spika, kitendo cha kumsafirisha mtu bila ya ridhaa yake, kutoka eneo moja kwenda eneo jengine ni jambo lisilokubalika. Kwa sababu unamnyima uhuru wake na haki yake kama binadamu ambaye anatakiwa awe na uhuru kwa jambo ambalo analifanya. Sasa kupiga vita haya Mhe. Spika, ambayo yamezungumzwa na sheria hii, mimi naunga mkono kwa asilimia mia moja kuona kwamba tumo katika kutekeleza yale makubaliano ya Kimataifa.

Mhe. Spika, jengine lililojitokeza katika miaka hii ya karibuni sijafanya utafiti wa moja kwa moja lakini inasadikiwa pengine hapa kwetu Zanzibar pia lipo kwamba hivi sasa kumekuwa na usafirishaji wa watu kutoka katika visiwa vyetu hivi. Pia katika Tanzania na mwambao wa Afrika Mashariki hasa kwenda kufanya kazi katika nchi za Arabuni na mara nyingi wanatakiwa wanawake.

Mhe. Spika, wanaondoka hapa kwa azma ya kwamba wanakwenda kule kufanya kazi za majumbani. Unajua kazi za majumbani pengine ni kazi za kupika, kuosha vyombo na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Lakini badala yake Mhe. Spika, wakifika kule kunakuwa na mabadiliko ambayo pengine aliyechukuliwa kwenda kufanya kazi hiyo hakuwa tayari kuyafanya. Analazimishwa pengine kufanya kazi ambazo hakuziridhia. Sasa haya nayo pia ni mambo ambayo yapo na kuna haja kama ilivyotajwa katika sheria hii kupigwa vita kwa sababu si tu kwamba ni mambo maovu kwa mambo ya dunia, lakini mambo maovu pia katika mambo ya dini ya Mwenyezi Mungu inakataza mtu kuyafanya katika hatua ambayo haipo kisheria.

Mhe. Spika, jengine ni kuhusu udanganyifu nao pia umetajwa katika mswada huu. Mhe. Spika, udanganyifu ni mbinu zinazotumiwa na watu wengi duniani.

Sasa katika kupiga vita biashara hii ya udanganyifu basi mimi naunga mkono mswada huu na umekuja wakati muafaka.

Mhe. Spika, katika suala zima la udanganyifu, pengine udanganyifu unakuja aidha mtu anafanyiwa kwa kuolewa kwa sababu ya mahitaji tu lakini pia kwa kutokuelewa. Anaweza kuja mtu akakueleza kwamba ana dhahabu, na dhahabu hii anataka kwamba mshirikiane pamoja ili muweze kwenda kuiuza pahala. Aidha, mambo yanayohusiana na hayo kwa mfano ya dhahabu kuna mambo kama almasi, lakini kumbe hana dhahabu wala hana almasi, ana mambo tu ya udanganyifu ambayo wewe kwa sababu huelewi nini dhahabu na nini almasi anakuingiza katika tamaa na kukufanya kwamba wewe labda akutoze fedha.

Kwa hivyo, anakutoza fedha nyingi na fedha zile ukishamkabidhi basi anaweza akakuachia ule mzigo wewe kwa kujenga tamaa kuona kwamba kwa vyovyote kwa sababu mimi nimetoa fedha na nimekabidhiwa mzigo ule wote, basi unajenga imani kwamba tayari mimi sasa naelekea kwenye utajiri. Lakini baada ya muda mchache mtu yule anakutoroka na humuoni tena, anakubakisha pale katika njia panda ukibakia na mambo ambayo sio dhahabu, wala sio almasi, pengine ni chupa tu zilizosagwa. Matokeo yake unapata hasara kubwa na kuingia katika umaskini!

Pengine ulikuwa tayari umeshakuwa mfanyabiashara mzuri na unaweza kujiendesha pamoja na kuendesha familia yako, lakini pia kutoa mchango kwa serikali kwa sababu mfanyabiashara nae anachangia mapato ya serikali kutokana na kodi mbali mbali anazozitoa. Lakini unapofikishwa pahala ukafilisika maana yake tayari wewe utakuwa huna uwezo wa kujiendesha wala kukusaidia familia yako, lakini hata serikali yenyewe itakosa mapato kwa sababu tayari mteja wake huna kitu.

Mhe. Spika, jengine limezungumzwa hapa kuna fedha bandia. Mhe. Spika, fedha bandia zipo na zinatumika. Sasa pamoja na mswada huu kuzuia lakini pia Mhe. Spika, ningeomba sana Wizara ya Fedha pamoja na taasisi zake wakasaidia kwa wananchi kuweza kuzitambua fedha bandia ni zipi? Pamoja na taarifa zinazotolewa na wenzetu hawa wa baadhi ya vitengo kwamba fedha bandia inakuwa hivi na hivi, mimi ningeomba taaluma zaidi zitolewe ili kudhibiti hizi fedha bandia.

Mhe. Spika, fedha bandia kwa hapa Zanzibar zinatumika lakini kidogo nashukuru na naomba Mwenyezi Mungu atujaalie tuendelee kuwa hivi, kwamba mtandao wake sio mkubwa sana. Mara nyingi mtandao wa fedha bandia unakuja na wageni wanaokuja kutoka eneo moja na kuja katika eneo letu. Mhe. Spika, hii mara nyingi inapatikana kwamba ili mtu aweze

kutengeneza fedha bandia kwanza anatakiwa mtu yule awe tayari ameshaasi kwa maana ya kwamba ameshajiepusha kuwa karibu na Mwenyezi Mungu.

Mhe. Spika, mtu ambaye anaamini sana dini yetu ya Kiislam na akawa ni mtu mwenye *taqua* hawezi kuitengeneza au kuitumia fedha haramu na akaweza kumpa mwenzake kuitumia. Lakini pia kupokea kutoka kwa mtu mwengine ambazo pengine ataletewa labda azitumie kwa niaba ya kwenda kuzibadilisha pahala hatokubali kwa sababu anajua kwamba lile ni kosa na linaweza kumpelekea kupata majanga mengi.

Lakini kwa mujibu wa utandawazi tulionao fedha bandia zinaweza zikaingia. Kwa hivyo, mimi ningeomba serikali kupitia vyombo vyake ikazidisha mtandao ule wa kuzuia hizi fedha.

Mhe. Spika, mikoa mikubwa kwa mfano kama vile ya Tanzania Bara katika miji mikubwa kama vile Mwanza kuna kipindi fulani kulikuwa na fedha nyingi za bandia na mpaka serikali ikafikia pahala imeshindwa kuzizuia wakaamua sasa zitumike, zikawa zinatumika. Sasa hii inaonesha athari ya mambo haya yanavyoweza kujitokeza. Wameruhusu kwa muda fulani zitumike ili na wao waweze kuzikusanya na zikiingia benki maana yake tena hazitoki. Sasa Mhe. Spika, mpaka tunafika hapo ujue kwamba ni tatizo. Kwa hivyo, hii sheria imekuja pahala pazuri na inaweza kusaidia tatizo hilo.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo limetajwa katika sheria hii katika mlolongo mrefu wa mambo yale kuna suala limezungumzia wizi. Mhe. Spika, wizi ni jambo ovu maana yake ukifanywa katika taasisi zetu za serikali, lakini pia ukifanywa na mtu binafsi wizi ni jambo ovu kwa hiyo kulizuia kwa njia yoyote ile ni jambo jema.

Lakini Mhe. Spika, vipi tutazuia wizi? Mhe. Spika, wenzetu wametaja hapa kipindi fulani katika Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira kupitia eneo la Misitu, pale serikali katika kipindi hicho ilipoteza fedha nyingi sana. Ilipoteza fedha kwa sababu ya kwamba maafisa wao wale wa kati na kwa vyovyote walikuwa na mtandao na maafisa wakubwa. Kwa sababu haiwezekani ufanye kazi hizi bila ya kuwashirikisha wafanyakazi wakubwa. Waliweza kufanya kazi hizi za wizi kwa maana ya kwamba mfanyakazi mmoja anaweza akapatiwa vipande vya majina ya watu kama kumi na pesa hizo zote akapokea mshahara yeye mtu mmoja.

Sasa fedha hizo akizipata maana yake kunakuwa na mtandao wa kugawana baina yake yeye ambaye amechukua hizo fedha lakini na wale ambao wametoa. Sasa zoezi hilo likawa limekwenda na *voucher* hizo zikawa zinafanywa lakini nashukuru Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika awamu

tofauti imekuwa ikishughulikia suala hili na kuona kwamba hakutakuwa na mtu ambaye anapokea fedha bila ya kuifanyia kazi. Kwanza kwa kutengeneza vitambulisho vyetu hivi vya Mzanzibari Mkaazi ambavyo hivi sasa katika taasisi za fedha sidhani kama kuna taasisi ya fedha ambayo unaweza kwenda kupokea fedha bila ya kuwa na kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi.

Kwa hivyo, hili ni moja katika zoezi ambalo limefanywa na Wizara yetu ya Fedha la kuweza kudhibiti hizi fedha haramu upatikanaji wake na kutoa kwake.

Mhe. Spika, jengine ambalo pia linahusiana na hili ni la wafanyakazi hewa. Mhe. Spika, wafanyakazi hewa nao pia ni fedha haramu na fedha chafu kwa sababu ni mtu ambaye si mfanyakazi lakini anapata fedha kutoka serikalini na kusaini vocha ya serikali kwamba yeye ni mfanyakazi katika taasisi fulani.

Mhe. Spika, serikali imeanza kulifanyia kazi ninategemea kwamba tutafika pahala tuone kuwa nalo limekatika.

Sambamba na hilo Mhe. Spika, pia taratibu ambazo zimetolewa na Wizara ya Fedha kwamba , wafanyakazi sasa badala ya kupokea fedha katika taasisi zao au katika wizara zao, basi moja kwa moja fedha zile zinakwenda benki. Kwa hivyo, benki nayo inasaidia kuhifadhi hizo fedha.

Lakini Mhe. Spika, watendaji hawa waovu wa taasisi za fedha ambao kwa njia moja au nyengine nao wanapelekea kupoteza fedha, nazo ni fedha haramu. Watu hawa wanashirikiana na watu wa nje, Mhe. Spika, imetajwa hapa fedha zilizoibiwa Bank ya Watu wa Zanzibar, ni fedha nyingi.

Nchi kama hii yetu maskini Mhe. Spika, inapofika mahala tukaibiwa fedha kama zile basi tuone kwamba tunaingia katika unyonge mkubwa. Kwa hivyo, mimi nafikiria sheria hii itakuwa imeweka mkazo kuona kwamba nayo hayo yatapatikana ufumbuzi kwa makosa hayo ya fedha katika taasisi za fedha.

Mhe. Spika, jengine ni magendo. Magendo nayo yanasababisha kupatikana kwa fedha haramu. Kwa sababu mtu ambaye anachukua magendo, kwanza anapita katika maeneo ambayo hakuna vizuizi vitakavyomfanya yeye aweze kulipa kodi. Kwa hivyo, moja kwa moja yeye anakwepa kodi, maana yake mtu wa magendo moja kwa moja ni mtu ambaye anakwepa kodi.

Kwa hivyo, kwa sababu imetajwa hapa Mhe. Spika, anapofanikiwa mtu huyu wa magendo kwa njia moja ama nyengine kusafirisha magendo yale, tayari atakuwa ameshaingiza fedha haramu kule alikokwenda, lakini na yeye amekwenda kuuza kile alichokiuza na hatimaye kupata fedha. Mhe. Spika,

serikali inajitahidi katika hili, lakini bado tunahaja ya kuongeza nguvu, ili kuona kwamba tunakomesha masuala haya ya magendo.

Mhe. Spika, jengine ambalo limetajwa katika sheria hii na imezihusisha taasisi za kifedha. Sijui kama nimeelewa vizuri, lakini kama nimeelewa vizuri basi itakuwe nimekwenda sawa. Ni kwamba zimemtaja hapa mtoa taarifa kwa maana ya kwamba atakayetoa taarifa pengine za mtu ambaye anajishughulisha na mambo haya.

Mhe. Spika, hata tulipokuwa kwenye semina hii, tuliitaja na ilitajwa kwamba inawezekana akaonekana mtu nyendo zake. Mhe. Spika mfano mtu anakwenda benki kwa kila wiki, ama wiki mara tatu na anawekeza fedha nyingi, lakini nyendo zake za huku nje haonekani biashara yake kuwa ana biashara ambayo ingemuwezesha kuweza kuweka fedha zile benki. Maana yake ni kwamba benki hapa ikigundua hivyo, wale wafanyakazi wa benki wanatoa taarifa kwa taasisi husika, yaani kwenye vyombo hivi vya serikali.

Mfano polisi na vyombo vyengine ambavyo vitaweza kumfanyia kazi mtu yule, kuona kwamba ana biashara gani ambayo inamuwezesha yeye kuwa na fedha hizo katika kipindi hicho kifupi na akaweza kujijengea wigo mpana katika kuweka fedha nyingi katika vipindi hivyo vifupi?

Mhe. Spika, hapa panahitaji hawa wanaotoa taarifa walindwe, kwa maana ya kwamba Mhe. Spika, ukikosa kuwalinda hawa maana yake watashindwa kufanya kazi zao vizuri.

Jengine ambalo ningetaka kulizungumza katika mswada huu ni kuunga mkono kwa maeneo yale yote ambayo yamependekezwa hasa ya adhabu kwa watu ambao wanapatikana na makosa ambayo yanahusiana na mambo hayo. Kuna makosa mengi ambayo yametajwa yanapatikana katika makosa hayo.

Mfano Mhe. Spika, mtu ambaye anapatikana na fedha haramu, basi aidha kwa kusafirisha au kuwa nazo tu basi atapewa adhabu ya shilingi milioni 100, ama kifungo kisichopungua miaka saba.

Mhe. Spika, hii inaonesha dhahiri kwamba ni kuweka mkazo, ili kuona kwamba hayo makosa hayafanyiki, ndio maana adhabu hii kali imetolewa kwa yule mkosaji ambaye amefanya hilo kosa.

Mhe. Spika, katika mswada huu kama nilivyosema kwamba umetaja maeneo mengi ambayo yanahusisha kuzuia kwa fedha haramu, ama kuingia au upatikanaji wake. Sasa Mhe. Spika, ningewaomba basi Waheshimiwa Wajumbe wakaangalia mswada wao kwa makini kila mmoja, na baadae

akapata fursa ya kuchangia, kwa sababu ni mswada muhimu ambao utekelezaji wake utasaidia nchi yetu kutokana na makosa haya, vile vile kuifanya nchi yetu kujijenga kiuchumi.

Kwa sababu Mhe. Spika, haya yote makosa ambayo yakifanyika moja kwa moja yanapelekea nchi kuwa na uchumi dhaifu, kwa sababu tayari watakuwa wanakosa fedha nyingi ambazo zingeingia moja kwa moja katika mfuko mkuu wa serikali, basi zitakuwa haziingii humo na zitaingia kwenye mifuko ya wachache.

Jengine Mhe. Spika, ambalo ningependa nilizungumze kwa kumalizia mchango wangu huu, vile vile nimehusisha na wale ambao wanafanya biashara haramu ya madawa ya kulevya, pia fedha zao zikipatikana maana yake moja kwa moja si fedha halali, kwa hivyo ni fedha haramu. Kwa hivyo, kwa njia moja ama nyengine wanapokwenda katika hatua ya mwisho ya kwenda kuzisafisha hizi fedha ambazo wamezipata katika makosa hayo ambayo ni ya madawa ya kulevya, maana yake tayari watakuwa wanaingia katika mtandao huu, nayo tungeomba kuona nyendo za watu hawa zingekuwa zinafuatiliwa kwa makini na waonekane moja kwa moja hawajiingizi katika kuziingiza fedha hizo haramu hapa nchini. Pia hayo madawa ambayo yatapelekea upatikanaji wa fedha zenyewe ambazo hatima yake zinakuwa ni fedha haramu na badala yake kutaka kuzisafisha katika kufanya kazi nyengine ambazo hazihusiani na mambo haya.

Mhe. Spika, tumesema pale kwamba mtu anaweza kufanya kazi hii pengine katika kipindi cha miaka 10 mpaka 15, lakini baada ya kupata fedha nyingi, basi akaamua sasa kuondokana na biashara ile ya madawa ya kulevya, na akaanzisha vitega uchumi. Kwa mfano mahoteli, majumba ya starehe na mambo mengine. Sasa itakapobainika kwamba chanzo chake kabla ya hapo ni fedha hizi, basi fedha hizi kwa mchango wangu Mhe. Spika, ni kuona kwamba mali hizo zinataifishwa. Sasa ili kuweza kufanya kazi hiyo kunahitaji kazi pevu kwa sababu si mambo ambayo yako dhahiri sana, kwa hivyo kuna kazi kubwa.

Zaidi Mhe. Spika, mimi ningesema kwamba tungetizama fedha hizi au tungetizama sheria hii kutizama hapa tulipo, kwamba huko nyuma kumepita mfano, lakini kwa sasa tungetilia mkazo zaidi ili kuona kwamba hayatokei hayo ambayo yameoneshwa katika sheria hii kuwa yanaonesha kuingia katika fedha haramu na fedha chafu.

Baada ya hayo Mhe. Spika, mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Chaani, kama nilivyosema mapema kwamba tunaunga mkono kwa asilimia mia moja, ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ndogo ya kuchangia sehemu fulani ya mswada huu.

Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuweka hai na wazima na kuwepo katika Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, mswada huu unanitia wasi wasi mimi kwa hapa Zanzibar. Kwa sababu juzi tulipokuwa tukipitia mswada wa madawa ya kulevya, ambapo kwa mujibu wa mswada huu madawa ya kulevya ni sehemu tu ya mswada huu ikiitwa kwamba ni *Predicate Offence* ambapo inapelekea kupatikana kwa hizo fedha haramu. Tumeona jinsi serikali ilivyo legelege katika kushughulikia ile *Predicate Offence* ya madawa ya kulevya. Sasa tukiingia katika mswada huu ambao ni *secondary* unahitaji kujua kwamba kumepita lile kosa la awali halafu ndio zikapatikana hizi fedha. Kwa hivyo, huu mswada ulikuwa unataka tuwe-*highly developed* katika kushughulikia zile *Predicate Offence* halafu tuingie katika mswada huu.

Sasa mimi unanitia wasi wasi kwamba, huwenda ikawa tumefuatana kama alivyosema Mhe. Waziri Kivuli, tumefuata mkumbo wa kukubaliana tu, lakini bado hatujakuwa tayari katika kushughulikia haya. Kwa hivyo, ili yaweze kupatikana masahihisho, kwa sababu biashara kubwa ambayo fedha zake husafishwa ni biashara ya madawa ya kulevya, kwa sababu ni biashara ulimwengu mzima ni haramu. Na *volume* yake ndogo tu inatoa mafedha mengi.

Kwa hivyo, hii miswada kwa kuwa imekuja mmoja baada ya mwengine, mimi nadhani tungekuwa wna hadhari sana katika kuona kwamba ule wa mwanzo unashughulikiwa mwanzo halafu ndio uje huu. Fedha haipatikani mpaka yauzwe hayo madawa. Wako wanaolima wakatengeneza fedha, wewe unataka kuishughulikia ile fedha, lakini madawa yanasambaa. Kwa hivyo, kama amabvyo nilichangia katika mswada wa madawa ya kulevya kwamba ubinafsi ukitawala, rushwa inatawala katika ushughulikiaji wa madawa ya kulevya. Sasa mambo haya ambayo vile vile ni moja katika kosa la mwanzo katika hayo, ina maana na hayo pia yaende sambamba katika kushughulikiwa.

Mhe. Spika, ndipo niliposema kwamba mimi nina wasi wasi katika utekelezaji wa mswada huu kwa hali tuliyokuwa nayo hapa Zanzibar, hatujajiweza. Ndio kwanza tuko katika *infant stage* ya *implementation* au tunaita *enforcement* za sheria. Ilivyokuwa tuko katika *infant stage* tuipitishe, labda kwa ku-*please* watu wengine, au kwa kuridhia hiyo mikataba ya kimataifa. Lakini kiukweli hasa utekelezaji wake bado kabisa hatujafikia. Hilo la mwanzo Mhe. Spika.

La pili, imeonekana katika mtazamo mzima wa ushughulikiaji wa upigaji marufuku madawa ya kulevya kwamba, wanaokamatwa ni vidagaa, nyavu yetu

ni ile iliyopigwa marufuku. Mhe. Spika, ziko nyavu zimepigwa mafuruku zile za kukokoa kokoa mule baharini, ya kukokota na zile zenye macho madogo. Lakini hii ndio nyavu iliyokamatwa na SMZ, sasa wanataka na wao waipige marufuku nyavu hii kama walivyoipiga marufuku ile nyavu ya baharini, na hii nyavu waliyokamata wawanyang'anye hawa na waweke zile nyavu zenye macho mapana, ili na hawa nguru na papa wavuliwe, kwa sababu hapa ndio kwenye kiini.

Mhe. Spika, juzi kuna mheshimiwa mmoja hapa katika kuchangia alisema kwamba inasikitisha hata wawekezaji na wao wameingia. Wamekuja wakaitizama hii hali wakaona aah! hapa panaingilia, na wao wakaingia tele. Mhe. Mjumbe mwenzangu yule wa Matemwe yeye anakwenda na kurudi na gari kumbe ndani ya gari yake siku nyengine wanaweza wakapachika dawa la kulevya. Huyu ni rafiki yangu sana kwa hivyo namtaja.

Mhe. Spika, tunabadilishana fulana mimi na Mhe. Ame Mati Wadi. Nikipata blue nampa na yeye akipata kijani ananipa, kwa hivyo ni rafiki yangu sana. Sasa Mhe. Spika, ni lazima tubadilishe mienendo ili tufikie pahali ambapo tunaweza sisi kutekeleza hizi sheria zetu kama tunavyozizungumza humu.

Mhe. Spika, kesi zote zilizokamatwa hapa nasikia moja tu ndio iliyo-*involve* zaidi ya shilingi milioni 20 au 30 ya madawa ya kulevya, lakini zote wanakamatwa kwa kete. Sasa hawa hawatusaidii kitu. Hilo ni la pili.

La tatu, Mhe. Spika, sisi tumebahatika kupata matokeo mbali mbali kuanzia mwaka 1964, kwa bahati nzuri kukaja kipindi ambacho dunia ikachangamka, watu wetu wamesafiri na wako katika maeneo mbali mbali, kuanzia Tanzania Bara na ulimwengu mzima.

Kuna mtu mmoja Mhe. Spika, aliniambia kwamba kuna jamaa alikwenda *Antacti*c sijui huko. Akamuuliza jamaa kwamba natafuta hoteli, akamjibu kuwa kwa unavyozungumza wewe basi unatokea Zanzibar, hakuna hoteli twende ukakae nyumbani, ni kwamba watu wetu wameshafika huko, yaani wametambaa ulimwengu mzima, mashariki na magharibi. Sasa kwa bahaati nzuri wengi wao wana ule ule utamaduni wa mjomba na shangazi wa kusaidiana. Utamaduni huu hauko kwa wazungu, hawa wazungu wanaotupa mikoba hii baadhi yao hawana utamaduni wa kusaidiana. Kwa hivyo, wao wataliona ni jambo geni kwamba mimi nimpelekee bibi yangu, nimpelekee shangazi yangu. Mmehusiana na nini, wewe shangazi yako na mjomba wako mmehusiana nini. Lakini hawa vijana wetu wamechukua utamaduni wetu wanawaletea jamaa zao fedha mbali mbali.

Sasa katika ufuatiliaji wa sheria hii tuchukuwe hadhari kubwa, ili wale ambao wanaletewa misaada ya kupata vijio vyao na serikali ikapata nafuu ikawa hakuna watu wanaookota ndani ya madebe ya mataka, basi tusije tukaikata kwa kutumia sheria hii, tukaja tukawatilia mashaka hizi sijui za walioko wapi, sijui hizi zinatoka wapi na hizi zinatoka wapi, tuingie kwenye uchunguzi wa kina mpaka pale itakapoonekana dalili ya kweli sio kwa tuhuma tu.

Mhe. Spika, baadhi ya wenzetu yameshawafika haya. Kwa mfano katika Africa, Egypt na Somalia ni watu ambao wanapokea sana misaada kutokana na familia zao. Bagladesh ni sehemu moja ambayo inatoa wafanyakazi wengi kwenda pale Middle East. Kwa hivyo, ilipoanza kuja mtindo huu, hasa kwenye suala la kupinga ugaidi waliathirika, kwa sababu zile sehemu ambazo walikuwa wanawapelekea jamaa zao, wale ambao walikuwa wakipokea pesa kutoka kwa wale wafanyakazi wakiwapelekea jamaa zao walipata shutuma kali na wengine wakafungiwa. Kwa hivyo, na sisi tutafute njia ambayo itaondoa tatizo hili.Vyenginevyo mzigo huu mwisho utakuja kwenye serikali.

Mhe. Spika, kwa nini utakuja kwenye serikali. Mhe. Spika, kwa mujibu wa pato la taifa la Zanzibar lilivyo, tunaambiwa kwamba ni shilingi isiyozidi 1500/= *per capital*. Mhe. Spika, hebu sasa hivi mpangie mtu kwa Shs.1500/= hiyo ni *average* ya kila mtu. Sikwambii kwamba kuna watu tayari kwa nafasi zao wameshachukua Shs.6,000/= au Shs.10,000/= wanabakishiwa Shs. 500/= hebu mpangie atazitumia vipi. Lakini fedha zinazoletwa na jamaa zetu, zikiwemo *material*, kwa sababu ni aina ya fedha. Kwa sababu mtu akikuletea nguo, ina maana kakuletea fedha, kwa sababu wewe ulikuwa ukainunuwe dukani, lakini kakuletea ni *substitute*, kwa hivyo kakusaidia *financial*, lakini kakuletea *in material* tu, *in candy* wanaita wazungu.

Mhe. Spika, zile zitakuja kuathirika vibaya na hasa katika kifungu cha 10, kwa sababu kimeunganishwa baina ya Tanzania Bara na hapa kuhusu FIU na mambo mengine yale ya kamati ya tume ya pamoja, wenzetu hawana sana hii, Tanzania Bara hawataathirika na hili, kwa sababu si wengi walioko nje. Wao wanataka wachukuwe pale mirija waipeleke nje sikwambii atoke huko nje alete Bara. Wale wenye vipesa kidogo, vijisenti wanachukua wakapeleka nje, sikwambii wale ambao walioko nje tena kama wataleta huku ndani. Kwa hivyo hii haitawaathiri wao. Itatuathiri sisi ambao jamaa zetu mbali mbali kwa Uislamu wao, kwa utamaduni wao waliochukuana nao wanatusaidia.

Mhe. Spika, hata taasisi za kidini, kwa kutumia hii nembo ya kushughulikia ugaidi. Mimi Mhe. Spika, katika Jimbo langu la Ziwani walitaka kujenga jengo la skuli ya ufundi, na walianzisha jengo lile, lakini waliita Ziwani Islamic, kuita hivyo tu ikawa hoja . Ziara walizozipata kipindi hiki cha yule bwana Bush sijui ni ziara za mara ngapi walizokuwa wakiulizwa, wala jengo lenyewe

halijasimama ni nguzo tu, yaani ni msingi na nguzo tu. Lakini pesa hizi mmezipata wapi ni kwa kuita Islamic tu. Kwa hivyo, na hili suala la ugaidi ndio maana Waziri Kivuli akasema kwamba tuwe na maana halisi ni nani gaidi. Ikiwa mimi najenga madrasa au sekondari, skuli ya ufundi, kwa hivyo ni gaidi na pesa naulizwa nazipata wapi na ananiletea nani ,ziara ya kwenda na kurudi. Kwa hivyo, ni lazima hapa tupatizame.

Mhe. Spika, kuna jambo jengine ambalo lingehitaji ufuatiliaji mkubwa. Mimi Mhe. Spika, nilikuwemo katika Kamati ya Fedha na Uchumi, sitaki niingie katika *details* kubwa ya kifungu kwa kifungu, kwa sababu tumewaeleza na ndio maana kama ulivyoambiwa na Mwenyekiti. Lakini bahati mbaya, waswahili husema 'abebwaye hujikaza'. Sisi tulijitahidi kumbeba Mhe.Waziri lakini leo katuangusha, maelezo yake yamekuwa mafupi sana kiasi cha kwamba hayakufahamika kwa wengi, hii pesa haramu isiyosafishwa. Kwa sababu katika mswada wa mwanzo kulikuwa na neno kusafirisha, sasa sisi katika kupitia ikaonekana kwamba limekosewa, kwa hivyo ni kusafisha.

Mhe. Spika, hata ukichukua povu, pengine pesa imeingia vumba, basi ukichukua povu ukaiosha ni kuisafisha. Kwa hivyo, ilikuwa Waheshimiwa Wajumbe wafahamu vizuri zaidi kutokana na maelezo yako, nini maana hasa ya kusafisha? Lakini maelezo ya Mhe. Waziri alotoa na watu wanasema yali-*fall short* ya kuelezea hasa maana na ukubwa wa hili suala, kwa hivyo, pengine ndio maana hata Mhe. Waziri Kivuli akamwelezea zaidi Mwenyekiti kwamba alielezea zaidi kuliko Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, usafishaji huu wa fedha, kwa sababu ni fedha ndio inayotizamwa, ina maana kunahitajika watu ambao watakuwa ni waangalifu katika *system* mzima. Ndio maana tunaitaka hii FIU kilikuwa kiambatanishwe ili tuone kwa hapa Zanzibar kitatoa watu kutoka wapi. Katika mambo ya kitaalamu kama haya hatungetegemea tena kupata vifungu, ndio tukasema kwa hekima ya Rais na kwa hekima ya waziri, kwa vile anavyoitwa Rais na vile anavyoitwa waziri basi anaonesha kwamba ana hekima. Kwa sababu wako wengi hawajaitwa cheo kile. Lakini haya mambo yanataka utaalamu, kwa hivyo tukitaka tukione kile kitengo cha FIU kwa hapa Zanzibar ni nani ata-*qualify* kuingia katika kitengo kile, kabla ya kupitishwa hii sheria, lakini haikuambatanishwa. Sisi katika kamati tuliona kwamba kuna mapungufu hayo. Hakikuwa *defined* FIU. Sasa tusijetukakubali jambo halafu tukawa *imposed*.

Juzi hapa tulikuwa tunajadili kuhusu *TPDC*, tokea siku iliyoundwa inaitwa Tanzania, lakini sisi tumekuja kushtuka kwamba si ya Tanzania, kumbe tumeiachia kwa sababu inaitwa Tanzania na wala haikuitwa Tanganyika. Mhe. Spika, jambo lilikuwa halikubadilika kule ni Lake Tanganyika, kwa sababu

haliwezi kuhamishwa na kuletwa huku Zanzibar na *Tanganyika Packers*, kwa sababu ng'ombe hatuna sisi.

Kwa hivyo, jambo lolote ambalo lingeweza kuchukuliwa na kutumika sehemu zote basi linaitwa Tanzania. Kwa maana hiyo, tokea mwanzo tuangalie katika *wide post* ya haya mambo na wala tusiyavamie tu, halafu tena tukajatukasema kwamba sisi hatukuwemo na wala hatukushirikishwa. Kutokana na hali hiyo, lazima tuangalie tokea mwanzo, hii *FIU* nani *members* na Zanzibar itatoa nani *(Makofi)*.

Mhe. Spika, kama nilivyosema kwamba ukenda *Western Union* zile sehemu kama vile Benki zenye *Western Union* utaona ni jinsi gani jamaa zetu wanavyopata *subsidy* kutoka kwa jamaa zao nchi mbali mbali, hizi ndizo zinazosaidia.

Kwa sababu mimi mara moja tulikuwa na *Workshop* wakati nilipokuwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, alikuja katika wale wataalam waliokuja kufanya ile *Workshop*. Kwa kweli aliuliza huu umasikini uliopo hapa watu wanapata wapi fedha za kujenga nyumba hizi zote, mbona haionekani kwamba *ecomonic* yenu na nyumba zinazojengwa vinalingana.

Mhe. Spika, nilimwambia kuna mambo mawili na wala sikumficha kwamba wengine wanatoboa mfuko wa serikali na kwenda kujenda, lakini wengine wanao jamaa zao mbali mbali nje tena ndio wengi wanawaletea fedha na wala hazitokani na uchumi wa humu ndani *(Makofi)*.

Sasa hii kusema kwamba kila mtu anayo simu ni moja katika maendeleo. Je, simu hizo zinapatikana kutoka wapi, ingelikuwa ni hizi shilingi 1,500/- ambazo ndizo tunazopata kutoka serikalini, yaani chumo la taifa ni shilingi 1,500/- nani angelinunua simu hapa. Kwa kweli tungeziona hivi hivi, isipokuwa wakubwa tu.

Kwa sababu suala hili linahitaji *research* mtu ambaye mwenye wasi wasi na maneno yangu, basi akafanye utafiti na mimi niko tayari baada ya kumaliza utafiti wake aniite nika-*defend* haya niliyosema. Mhe. Spika, kama kweli mtu katika nchi *per capital* ni 1,500/- akamiliki kununua simu *(Makofi)*.

Kwa kweli mimi binafsi Mhe. Spika, nimeanza kupata simu kwa kusaidiwa. Kwa hivyo, najitizama kama mimi wakati huo ni mwalimu nimeanza kupata simu kwa kusaidiwa, leo mtu hana chochote aweze kumiliki simu kama si hii misaada ambayo tunapata kutoka kwa ndugu zetu.

Mhe. Spika, nikimalizia mchango wangu kwa sababu nilisema kwamba mimi na Mhe. waziri ni shahidi kwamba tulifanyakazi ya kuweza kuuchangia huu mswada katika kamati na ukafikia hapa.

Lakini suala la usimamizi wa sheria hii unahitaji mambo matatu. Kwanza tunahitaji kupata elimu ya kutosha. Kwa sababu sisi tunavyo vyuo vikuu hapa na hivi sasa vyuo vikuu ndio *immediate output* ya kwenda kazi (*field*). Kwa mfano, mambo kama haya yanayohusu madawa ya kulevya, masuala ya kusafisha fedha pamoja na mambo mengine.

Kwa hivyo, kuna haja ya wale wanafunzi walioko vyuo vikuu wapatiwe *first hand information*, kwani wale ndio *doors* inayoingia kwenye jamii hivi sasa, lakini hakuna anayeshughulika. Kwa mfano, semina zote utaona wanafanyiwa wale wale.

Mhe. Spika, napendekeza wale wanafunzi wa vyuo vikuu wapatiwe dose kuhusu mambo haya, yaani kuwe na *special request* wapatiwe utaalamu mambo haya kuweza kujuilishwa.

Jambo la pili katika kusimamia sheria hii tuwe waadilifu. Mhe. Spika, usipokuwa waadilifu, basi litakwenda kama lile gurudumu la madawa ya kulevya kwa sababu ndicho kinachopeleka mbele suala hili, yaani tuwe wakweli na waadilifu. Nadhani hili uadilifu linaweza kuwa gumu kidogo, lakini tukianza kuwa wakweli, basi hakuna tena haja ya *memoirs* kwamba huyo muachie namjua nyendo zake. Mhe. Spika, tukianza huyo muachie basi suala la sheria hii limekwisha kama ilivyokuwa Sheria ya Madawa ya Kulevya.

Vile vile katika suala hili la ukweli na uadilifu nataka kuongezea. Mhe. Spika, sisi tupo mataifa mawili, yaani tupo wa upande wa kulia na kushoto. Mimi nasema kwamba anapofanya kosa wa upande wa kulia achukuliwe kwa kosa alilolifanya na anapofanya kosa wa upande wa kushoto achukuliwe kwa kosa alilolifanya. Lakini anapofanya kosa wa upande wa kulia kusema huyu mwenzetu lazima tumlinde na akifanya wa kushoto ndio wote tena.

Mhe. Spika, siku moja kuna mtu mmoja alikamatwa kwa masuala haya ya kisiasa, lakini waliokwenda kumkamata ni askari 6 tena wote wanazo bunduki. Kwa kweli aliwageukia na kusema kwamba huyo mmoja atakapofyetua risasi mimi sifi mpaka zote zinielekee mimi, basi wale askari walicheka *(Kicheko)*.

Kwa hivyo, iwe kwamba akifanya huyu ni kosa na yule si kosa, kwa sababu hayo masuala ya madawa ya kulevya wapo watu wanaowajua, yaani wanajulikana hasa lakini wanaachiwa, kwa sababu ama yuko mrengo anaoutaka au anampa maslahi *(Makofi)*.

Suala la mwisho ambalo ni la tatu katika utekelezaji wa sheria hii lazima tulingane na utekelezaji wa kimataifa. Kwa hivyo, vyema kuwa na *training* maalum iliyokubalika. Kwa sababu hivi sasa Mhe. Spika, kuna baadhi ya taasisi na siku itakayofika wakati wake tutakuja kusema tukijaaliwa, zinazuia watu kwenda kusoma, yaani nafasi zinakuja na wala si za kulipia kwa ajili ya tunayoita *capacity building* ya ile taasisi, watu wanazuia nafasi zile kwa ubinafsi tu mpaka nafasi zile zinamaliza muda wake.

Sasa inawezekana hiyo *FIU* ikaleta taarifa kwamba tunataka watu wawili waende kusoma, basi akitajiwa Marekani au Ujerumani loo! Hapa ndipo pahala pa kupachika jamaa yangu hapa na yule *qualified* hapelekwi na yule anasubiri hajampata mpaka muda unamaliza na halafu sisi tena tunakuwa na matatizo mengi, kwa kweli hatuko *serious.*

Mhe. Spika, tutakuja kutoa ushahidi hapa wa hiyo taasisi siku yake ikifika. Kwa sababu taasisi inahitaji wasomi watu wazuia nafasi za masomo kibinafsi kabisa na wala hazilipiwi, kwa kweli jambo hili ni la kusikitisha *(Makofi).*

Mhe. Spika, kwa kumalizia naomba sana kwa sababu hii inahitaji utaalamu, tena utaalamu wa kimataifa katika kufuatilia zile nyendo pamoja na harakati zake. Kwa hivyo, lazima tukubali kwamba watu wakasome na wale wenye *qualification* zao *(Makofi).*

Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, ahsante sana nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia Mswada wa Sheria ya Usafishaji wa Fedha Haramu na Mapato na Uhalifu na Mambo Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Spika, kwanza ninamuomba Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho kuhusu hili neno usafishaji au usafirishaji, hapa naomba anisaide mantiki yake kwa sababu maneno mengine huwa yanatamkwa, lakini yanakuwa ya kisheria.

TAARIFA

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Spika, naomba kutoa taarifa kwamba labda Mhe. Mjumbe wakati nilipotoa hotuba yangu alikuwa nje ya ukumbi. Naomba sana azingatie ile *version* mpya tuliyoisambaza na ile ya zamani aiache, kwa sababu kwenye ule mpya utaona usafirishaji halipo, isipokuwa ni usafishaji. Sasa ukilikuta usafirishaji ndani ya *version* mpya basi ujue kweli hapo imekusudiwa usafirishaji.

Lakini neno hasa usafishaji. Kwa hivyo, naomba sana utumie hii mpya, ambayo kwa kweli tumejikita katika makosa mengi sana tunayaondoa kwa kushirikiana na kamati *(Makofi)*.

Mhe. Spika, ahsante.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, nikiendea kwenye ukusara wa 60 hapa kuna Wakala wa Usimamizi wa Sheria, maana yake ni Jeshi la Polisi, na inajumuisha mtu wa aina yeyote aliyeruhusiwa kufanya upelelezi au kufuatilia majukumu chini ya sheria hii.

Mhe. Spika, kwanza nianze kusema kwamba Jeshi letu la Polisi pamoja na kufanyakazi zao nzuri za uadilifu, lakini mambo mengine yanaupungufu na hususan kutokana na vitendea kazi. Kwa mfano, upatikanaji wa magari, *radio call* pamoja na mambo mengine.

Kwa kweli haya Mhe. Spika, ningeomba ili usimamizi huu uwe mzuri na halafu kutokana na kama kuna kifungu angalau maposho yale ya usiku kama hayapo, basi naomba hawa ndugu zetu polisi wapewe, kwa ajili ya kuweza kusimamia vizuri katika utekelezaji wao huu ambao ndio utakaotupa moyo mzuri wa kuweza kusimamia vizuri masuala haya yetu ya haramu.

Mhe. Spika, pamoja na haya yote labda niseme juzi niliipokuwa nikichangia mswada unaohusu madawa ya kulevya, nilijaribu kusema sehemu ambayo niliyoiona yenye kuhatarisha maisha kwa vijana na kueleza. Lakini kwa bahati nzuri kilifanyika kipindi maalum katika Televisheni ya Zanzibar kinachoitwa Sema na Polisi. Kwa kweli watu wengi walinipigia simu na kusema Mhe. mwakilishi mbona tunaona maswali na majibu moja kwa moja kwenye televisheni na wanasema suala hili si kweli.

Mhe. Spika, naomba nirejee *statement* yangu, suala hili ni kweli na mimi Mhe. Spika nimekuja hapa na nimekula kiapo cha utiifu kabisa na nilisema kwamba sitosema uongo. Kwa sababu mimi ninaakili timamu na wala sio mwendawazimu, mimi sifanyi jambo pasipokuwa na wananchi wenyewe kutupa taarifa kama ni viongozi wao, sasa wanapotupa taarifa zile huwa tunazifuatilia kwa kina na wala haturipuki tu, kwa kuwa ni mwananchi wako na wewe uifanye ile kazi tu. Kwa hivyo, lazima lile suala unalifanyia kazi kwa ajili ya kupata uhakika mzuri *(Makofi)*.

Kwa kweli tukio hili nilipigiwa simu na sheha wangu wa Kiwengwa na kuniambia Mhe. mwakilishi njoo haraka sana, kuna nini, njoo uone mwenyewe, basi nilipofika pale nilimkuta yeye wakati naingia mimi mkewe anaondoka.

Kwa hivyo, alinipa taarifa kwamba Mhe. mwakilishi hapa kuna tatizo mwanamke amekamatwa na madawa ya kulevya.

Sasa mimi nilimwambia kama ni hivyo je, tunaruhusika kuona, alisema tunaweza subiri tumwite askari, basi tulimwita askari na kusema hurusa twende mkazione. Mhe. Spika, tulikwenda kuoneshwa kete zimo kwenye *packet* kama za njugu za *plastic* nimeona mwenyewe kwa macho yangu. Mhe. Spika, pamoja na kuona nilisema hii *packet* haiwezekani ikawa *packet* tu, hebu na ndani nione huo unga wenyewe niuone wa aina gani. Kwa hivyo, nilifunguliwa na askari yule na tuliuona ule unga rangi yeupe. Mhe. Spika, nilisema kama ni hivyo sawa mtaendelea na sheria zenu.

Kwa hivyo, wakati tunatoka nje pamoja na sheha wangu tunamkuta muhusika yupo nje anatwita pembeni waheshimiwa ninakuombeni yule mama amekuja kwa ajili ya kulea mtoto tu, hali ile imetokea ni bahati mbaya. Hivyo, ninachoomba mimi ndiye mwenye mali, Mhe. Spika mimi si mwendawazi nina akili zangu timamu, yaani anatuambia mimi ndiye mwenye mali, kwa hivyo nakuombeni yule atolewe niingizwe mimi.

Mhe. Spika, tulirudi ndani na sheha wangu na kumueleza polisi kuna kaka kule anasema kwamba yeye ndiye tajiri, ambaye anasema huyu mama anusurike aingizwe yeye. Sasa je, kuna sheria au kifungu hicho nilimuuliza.

Kwa hivyo, aliniambia ngojea nipige simu niulize wakubwa wangu, wakati alipopiga simu tupo mimi na sheha tumekaa kikato, basi jibu alilopewa ni kwamba mkamatwa na ngozi ndiye mwizi. Kwa maana hiyo, huyo aliyekamatwa tu ndiye anayehusika na wala sio mtu mwengine. Mhe. Spika, basi sawa hakuna tatizo lolote sisi tulitoka na kwenda zetu.

Baada ya hapo Mkuu wa Wilaya wangu alinipigia simu na kuniuliza umeona na nilimwambia nimeona hali halisi mwenyewe, basi nilitaka na wewe ushuhudie. Mhe. Spika, nilitoka na kwenda zangu.

Sasa baada ya muda sheha wangu alinipigia simu kwa masikitiko na kunieleza kwamba ile kesi imekuwa *dismiss* na ule unga wa kaki, kwa kweli nilizimia Mhe. Spika. Kwa hivyo, ule unga wa rangi ya kaki, ina maana ule sio tena halisi umeshabadilishwa, nadhani kuna aina maalum na ikiwa rangi fulani ndio unga uliokuwa halisi, lakini ukiingia kwenye rangi nyengine sio unga. Mhe. Spika, nilimuuliza amekwambia nani, aliniambia kwamba nimeambiwa, ndio mpaka leo kimya.

Kwa kweli wenzetu hatuna nia mbaya na wao, isipokuwa tunachozungumza hawa askari wetu watufahamu kuwa uzembe wa aina kama hiyo usitokezee

tena. Kwa sababu lengo ni kuzuia na ndio maana tukasema hapa kwamba mswada huu unaohusiana na fedha haramu, sasa fedha haramu ndio hizo kwa njia hiyo na hiyo mantiki yetu.

Kwa hivyo, kama tutaachia tusiseme, basi madawa yataendelea na kuwaua watoto wetu pamoja na kuendelea kuwepo fedha za haramu. Mhe. Spika, hatuwezi kukaa tusiseme lazima tutasema kwa mujibu wa utaratibu na hasa sisi tunazirekebisha hizi sheria, basi lazima tuzieleze.

Mhe. Spika, tulizungumza suala wawekezaji. Hivi sasa tukiangalia kuna hawa *managers*, yaani mtu ukimuona tu utajua kuwa huyu mtu anakula unga na hawa wapo. Kwa kweli zile ndio njia za kuleta huo unga na wameona ile njia ya urahisi, yaani ndio haramu yenyewe hiyo Mhe. Spika, wanajilimbikizia fedha kwa misingi hiyo.

Kwa maana hiyo, wawekezaji wanaleta unga, wakati wanapoajiri hawafuati ile sheria yetu ya Serikali ya Zanzibar masuala ya mishahara pamoja na haki za wafanyakazi, yaani wanatoa mishahara vile wanavyotaka wenyewe na kile cha juu wanakichukua wao na hiyo ndiyo haramu yenyewe. Lakini kwenye sheria hii sikuiona.

Mhe. Spika, wanafanya hivyo, kuwa Sheria ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeweka kiwango cha fedha mtu alipwe shilingi 60,000/- na wao wanalipa chini ya shilingi 60,000/- kilichowekwa na serikali. Kwa hivyo, kile kinachobakia wanakipeleka wapi, ina maana yule *manager* ambaye anakuwepo pale ndiye mwenyewe kuchukua kile cha juu, hiyo ndiyo haramu yenyewe. Kwa kweli mambo hayo yapo, lazima serikali ikae pamoja na kujipanga vizuri katika kuyashughulikia masuala haya *(Makofi)*.

Kwa sababu mimi Mhe. Spika, ninajiuliza tunasema pamoja na kufuatilia vizuri viongozi, lakini hatimaye tunasubiri wakati tumalize hapa, basi tunatoka na kwenda zetu. Kwa kweli hali hii sisi wengine inatupa shida, hali hii inatupa shida kwa sababu kiapo ndicho kitakachotudhuru, yaani kile kiapo tulichokifanya pale ni halali ndani ya kiapo kile tunataja jina la Mwenyezi Mungu kwamba naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu. Kwa hivyo, tunaposema tuchangie basi tunaomba serikali itukubalie yale tunayochangia, kwa sababu yapo kweli na tunayaona yanatendeka.

Mhe. Spika, inapofika pahala na kusema mwekezaji analeta madawa Mhe. Spika tusikatae tayari hayo mambo yapo. Vile vile hao *managers* hao wengine wanakula unga, yaani ukiwao leo ni tofauti na zamani sasa mdomo umemzidi, yaani unaning'inia na wala sio maradhi isipokuwa ni unga. Kwa hivyo, hiyo ndiyo hali ambayo inabidi hivi sasa kila Mheshimiwa Mjumbe anayesimama

hapa anakuwa mkali, kwa sababu hizi sheria tunazozitunga hapa zifuate mkondo wake.

Kutokana na hali hiyo, ndio maana juzi nilisema hapa hawa watumiaji wadogo wadogo tusipande sheria ya kuwakamata na nilisema hivyo kwa fikra zangu Mhe. Spika. Kwa sababu hawa masikini wa Mungu ndio wanaopewa, kama hawa hawapati basi Mhe. Spika tusingekuwa na matatizo haya. Kwa mfano, narudia tena kwa Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii anachato kitengo kizuri sana, ambapo hivi sasa hawatumii tena kwa sababu wameshajihamasisha, kwa wale waliokuwa wamekonda basi wamerudi hali zao hivi sasa.

Mhe. Spika, hivi sasa kuna wimbi la ajira za watoto. Kwa kweli suala hili hapa tulipiga kelele sana kwamba jamani watoto wanaajiriwa wakati umri wao bado haujafika. Suala hili kwa kulifikiria lengo lao nini, Mhe. Spika, ndio ile dhana ya kusema wanajipatia fedha za haramu. Kwa sababu yule mtoto wanapomuajiri anajua umri wake ni mdogo kwa hiyo hajui chochote, kwa maana hiyo watakachompa yeye atakuwa ameridhika tu.

Kwa hivyo, lile pato la katikati bado anajilimbikizia yeye kwa kummaliza yule mtoto. Kwa sababu kwanza muda wake haustahiki na wala hamuenzi kwa mujibu wa sheria inavyosema kima cha chini kwa mshahara apewe kiasi fulani hakitimizi, nadhani na hilo tulione.

Mhe. Spika, ni vyema tukajipanga kwa ajili ya kuyaondosha mambo haya, kwa sababu kila siku zinavyokwenda tukasema bado ndivyo yanavyolimbikizana. Kutokana na hali hii ndio tumeona makosa yetu na sasa tunajirekebisha.

Kwa maana hiyo, kama tunajirekebisha Mhe. Spika naomba serikali kuu tujidhatiti kabisa na tuamue kama tulivyosema sehemu ya kifungu hapa madonge manene. Kwa hivyo, hili donge nene litoke kwa ajili ya kuonesha mfano, kwamba mtu akitoa siri ile apewe kwa kuwajibika kabisa na wala usitangaze kwa jina la mtu, lakini useme wazadi imeweza kutekelezeka, nadhani nalo linaweza kutusaidia.

Mhe. Spika, tukisema tukae tu na kuisema kwenye karatasi na tuseme muda wa kuondoka umefika. Kwa hali hiyo, nafikiria tutaendelea na vijana wetu watapukutika na sisi tupo hapa Mhe. Spika.

Nikiendelea na mchango wangu niende kwenye ukurasa wa 68 kwenye kifungu kinachozungumzia kwamba mtu yeyote anayevunja sheria kama kinavyojieleza kifungu chenyewe. Mhe. Spika, kuhusiana na adhabu hapa nasema bado ni ndogo, kwa sababu lengo letu ni kukomesha.

Kwa sababu nakumbuka kuna sheria ambapo bado sijazawali wakati wa Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, basi ilipitishwa sheria mtu atakapoua na yeye anyongwe, yaani mimi bado sijawa mwanasiasa. Lakini baadaye sheria hiyo ikawa haitekelezeki kwa yule mtia saini wa mwisho kuona ile hali ilivyo.

Sasa nafikiri kuna haja kwa sheria kama hiyo kurekebishwa tena na kuweza kutekelezeka, kwa sababu muuaji ni muuaji kama tunavyojua tukimuacha ataendelea na huku tayari ameshawaathiri wenzake, yaani wameshapoteza maisha.

Mhe. Spika, nina maana kwamba sheria hii pamoja na kuwa tayari ipo hapa, lakini bado ndogo haikidhi haja nyepesi. Kwa sababu kufumba na kufumbua miaka saba haiko mbali na hususan sisi tunavyo vyuo vya mafunzo na wala hatuna magereza ndio kabisa. Kwa kweli mtu anajifahamu kwamba kule anakwenda kupata mafunzo, lakini kama tungekuwa na Magereza angelifahamu nini anachokwenda kufanyiwa huko. Mhe. Spika, tumekwenda pamoja na hao wanafunzi wetu lakini ukiangalia hali ya kule, Mwenyezi Mungu atunusuru tusiende kwani hali ni ngumu kule, lakini bado wenzetu wao wanataka kuelekea huko lakini kama wakiamua hivyo tayari muelekeo huo tuione hii sheria. Sheria hii pamoja na hizi fedha zenyewe milioni mia moja, milioni mia moja sasa hivi ni sawa sawa na shilingi hamsini elfu.

Mhe. Spika, hapap tungeona ile hali halisi na tungejua zile *grams* ambazo mtu anaziingiza kwenye tumbo akaja nazo hapa zinafika kiasi gani? Mimi nafikiria tungefanya mara mbili zaidi. Kwa sababu pengine zile *grams* zinazokuja hapa ukiziuza thamani yake ni ndogo sana. Mhe. Spika, tukiangalia kuwa kontena la tumbo linalobeba sijui ni *gram* ngapi? Na kila *gram* ni kiasi gani? Mhe. Spika, sheria hii tungeipandisha nalo lingekuwa onyo kali kabisa na ingekuwa tayari mtu kutishika.

Lakini milioni mia moja, ni kwamba bado tumesimama pale sheria ingali bado haijaonesha makeke yake. Kwa hivyo, tungeomba Mhe. Waziri atizame zaidi kama upo wakati tuiangalie tena kwa undani zaidi, si vibaya kwani sasa hivi tunataka kukomesha masuala kama haya yasitokezee katika nchi yetu angalau hilo janga lililokuwa limeshapita basi tuliokowe na hili. Mhe. Spika, ni kwamba mitaa yetu yote imeathirika, watoto wanavyokula unga hata Matemwe nao unga upo unauzwa!

Mhe. Spika, ni kwamba Kempiski wana siku maalum ya kufanya sherehe zao, *Wallahi* mkitaka muende mkaone unga unavyouza kama njugu basi ni siku hiyo. Mhe. Spika, namwambia Mhe. Waziri siku hiyo ukisikia kule kuna siku maalum basi wewe jigeuze uvae vazi jengine ukatizame ile hali halisi ya huko. Mhe. Spika, kwa kweli hali ni ngumu na vijiji vyetu vinateketea kwa matatizo

haya. Mhe. Spika, ndio maana nikasema kuwa sheria hii ikiwa kali basi vijiji vyetu angalau tutaweza kuvinusuru.

Mhe. Spika, mimi leo sikutaka kwenda mbali sana, kwa sababu mimi ni mjumbe wa kamati hii na nilisaidia sana katika marekebisho, lakini nimeona yale yaliyokuwa mapungufu hayamo, nikaona bora nidondowe na kuweza kuyaeleza ili tufahamu vizuri. Kwa hivyo, Mhe. Spika, pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Kitope na mimi naunga mkono mswada huu asilimia kwa mia.

Mhe. Ali Denge Makame: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi leo kuchangia Mswada huu wa Sheria ya Usafirishaji wa Fedha Haramu na Mapato yanayohusiana na mambo haya.

Mhe. Spika, mswada huu kwa kweli umeletwa pahali pake ili kupata kuuchangia na kuupa baraka na inaonesha dhahiri kuwa itawapa nafuu wale wenye kipato cha chini. Pindipo tukishaupitisha utaondoa baadhi ya makero mengi ambayo yalikuwa yanawakabili wale wenye kipato cha chini.

Mhe. Spika, nije katika ukurasa wa 65 kifungu cha 4(i) mtu atafakari kabla ya amri ya kukamatwa haijatolewa. Mhe. Spika, hapa kitengo hiki kiwe na uangalifu wa kutosha kwa suala hili la kuwa mtu ameshafanya ovu na kama mada hii iliyozungumzwa humu kama kusafirisha pesa haramu, magendo au uhalifu mwengine wowote unaohusika kupata pesa kwa njia iliyokuwa ya haramu. Halafu mtu huyu asiwe na kesi kwamba amefariki na kufariki kwenyewe amejidhuru au kujiathiri sio kama amefariki kwa homa tu au ahadi ya Mwenyezi Mungu.

Kwa hivyo, hapa nataka paangaliwe sana sio kama inavyoeleweka kama kuna baadhi ya wengine utakuta ameshafanya kitendo cha kujipatia fedha haramu kwa hivyo mtu kama huyu inakuwa hajali kupoteza maisha, anategemea sana kwamba fedha yake itawaendesha watoto wake kimaisha. Mhe. Spika, mtu kama huyu kama ndio ameshafanya uhalifu huo wa kujipatia fedha chungunzima kwa njia haramu, na wakamataji walikuwa wameshapata picha kama fedha hizi kashiriki fulani kuzichukua na ziko mikononi kwake. Mhe. Spika, kusema amefariki iwe ndio basi lengo lake kubwa litakuwa wale aliokuwa nao watakuja kuitumia fedha ile na hapo hapo serikali itakuwa imeshaipunguzia fedha kubwa ya kujiletea maendeleo.

Mhe. Spika, mimi ningeshauri watu kama hawa wachunguzwe na waangaliwe kwa kina kama imesibitisha kuwa fedha ile ameipata kiharamu basi wanaohusika waliokuwa nao wafilisiwe. Kwa sababu masuala kama haya kama tutayaachia itakuwa upotevu wa fedha utakuwa unaendelea. Kwa mfano, kuna

baadhi ya nchi kama tunavyozisikia kunakuwa na magaidi wanatumwa kwa makusudi kufanya ugaidi ili kujipatia fedha. Mhe. Spika, mtu kama huyo akishakuahidiwa kufanya suala fulani na atapatiwa fedha matokeo yake yule anakwenda kujivalisha mabomu mwili mzima, hapo yeye hajali wala hahisi kama mimi nikipoteza maisha watoto wangu watapata shida. Mhe. Spika, anakuwa hajali kwa sababu fedha anakuwa ameshaidhibiti na yeye hata akiripuka na mabomu anakuwa hajali chochote. Kwa hivyo, ningeomba Mhe. Waziri akaangalia sana kipengele cha sheria hii.

Mhe. Spika, mimi ningependekeza kuwe na taratibu ya kufilisi baada ya kuwa mtu ameshaonekana akafanye kitendo kile ili kuchukua mali ya umma au kufanya biashara ya haramu inayothibitisha mambo haya. Kwa hivyo, ni bora afilisiwe kama kuna mali zake alizozipata kwa njia ya udanganyifu ili fedha hiyo iwanusu na baadhi ya wananchi wengine ambao waliokuwa hawana makosa hayo.

Mhe. Spika, katika sheria ya upekuzi tunatakiwa tuwe na uangalifu sana kwa sababu hapa tuna sheria ambazo zimepita hapa nyuma tulitangaza biashara huria na kila atakaye aje. Kwa hivyo, utakuta baadhi ya wafanyabiashara wetu wengi katika suala hili la upekuzi kama ilivyozungumzwa kuwa kwenye bandari zetu mtu akipita na mkoba mkubwa uliokuwa na fedha nyingi apekuliwe na aangaliwe fedha hizo amezitoa wapi na amezipata kwa njia gani.

Kwa hivyo, mimi nilikuwa nataka pawe na uangalizi wa kutosha kwa sababu tumeweka biashara huria, utakuta baadhi ya wafanyabiashara wengi huwa wanakwenda nje ya nchi kwenda kufanya biashara na kukopeshwa mali wengine huwa na mabilioni ya fedha. Baada ya kukopeshwa mali hizo wanavyotakiwa akishauza arejeshe fedha ya kigeni. Kwa hivyo, mara nyingi mtu akishauza mali hiyo anatafuta fedha za kigeni kurejesha fedha za watu.
Mhe. Spika, pindipo mtu kama huyo anapopita kwenye bandari zake akionekana na fedha hizo basi ni lazima aangaliwe, ameipata kivipi kwa biashara au ndio ameipata kwa njia haramu. Mimi jambo hili naogopa lisije likatuletea madhara ya sheria ile tuliyoipita ya biashara huria halafu watu wetu ambao wanafanya biashara kihalali wakaja wakashtuka na kupunguza nguvu kasi ya kufanya biashara. Mhe. Spika, ningewaomba wakaguzi waangalie kwa kina na kumtizama mtu mienendo yake.

Mhe. Spika, yule aliyekuwa na taratibu za kupitisha fedha haramu au kufanya biashara ya madawa ya kulevya kwa kweli huwa anatambulikana mwanzo wake anavyoanza, na shughuli zake anazozifanya. Kwa hivyo, kama utamuangalia kwa kina basi tunaweza tukamgundua tu bila ya wasi wasi ili kuondosha usumbufu kwa wale waliokuwa hawahusiki na kuwasaidia wananchi.

Mhe. Spika, kama inavyoeleweka sasa hivi kuwa nchi yetu ina vijana wengi wadogo wadogo ambao ni wafanyabiashara wazuri tu na wanamiliki fedha nyingi sana za kufanyia biashara. Kwa hivyo, hapa mimi ningeomba tupaangalie vizuri sana ili yale malengo mazuri ya sheria ile tuliyoiruhusu mwanzo isije ikabadilika na kwa kuwa faida yake tumeiona tumekuwa na wawekezaji wengi na wafanyabiashara wakubwa wakubwa, wanaomiliki bidhaa za kutupatia nafuu wananchi wetu. Hapa katika upekuzi ningeomba pawe na uangalizi wa kutosha, tuwapekuwe wale tuliokuwa tumeshawazoea na wale wanaojuulikana vitendo vyao wanavyovifanya.

Mhe. Spika, nakuja katika ukurasa wa 69 kifungu cha 15(i) kutoa taarifa ya uwekaji fedha wenye mashaka. Mhe. Spika, hii kama inavyoeleweka baadhi ya watendaji wetu wamekuwa na utaalamu wa kufoji risiti mbali mbali wa kutaka kujinufaisha wao wenyewe binafsi. Kwa hivyo, kama kitengo hiki kitakuwa na watendaji ambao watakuwa waangalifu sana kwa kuyaangalia haya naamini wazi masuala yetu yatakwenda vizuri. Mhe. Spika, ni vyema katika hawa ambao watakuwa wakaguzi na wapepelezi ambao watawafuma itakuwa ni vizuri kuwapatia zawadi, ili mtu atakayefichua siri na akatoa ushahidi ni vyema kufikiriwa na kuzawadiwa.

Mhe. Spika, pindipo kama tutafanya mfumo huu basi yale maovu mengi yatapungua. Mhe. Spika, haiwezekani mtu alifume suala la bilioni tatu ambazo zilikuwa zinasafirishwa kiharamu halafu leo uje umwambie kama hatuna cha kukupa isipokuwa ahsante. Kwa kweli hivyo itakuwa hatufanikiwi kufanya mambo yetu.

Mhe. Spika, vile vile ningelimtaka Mhe. Waziri baada ya kupitisha mswada huu ni vyema ikatolewa taaluma zaidi kwa wananchi ili wanapoyaona masuala kama haya basi wao wawe karibu kuyafichua. Kwa sababu madhara, shida na tatizo linawakabili wao ile hali ya kuwa maisha magumu kunasababishwa na watu hawa. Kwa hivyo, nawaomba wananchi na wao wawe tayari kutoa ushahidi wakati utakapoona masuala haya unapoyaona katika nchi yako.

Mhe. Spika, kama inavyoeleweka sasa hivi wimbi kubwa la upandaji wa maisha limekuwa linaripuka, hapa kila kukicha dola zinapanda bei tu. Kwa hivyo, jambo hili linasababishwa sana na hawa watendaji wa biashara hii ya usafirishaji wa fedha haramu. Wao huwa wanajipatia fedha kirahisi kwa mipango yao hii, lakini mwananchi huwa anapata tabu maisha yanakuwa mazito kulingana na ukali wa maisha unavyopanda wao wachache huwa wanafaidika. Mhe. Spika, hili naona limefika wakati wake sasa hivi kufanyiwa kazi ili kuhakikisha limepungua au limeondoka kabisa.

Mhe. Spika, nakuja katika ukurasa wa 63(g) usafirishaji haramu wa bidhaa za wizi au bidhaa nyengine. Hapa mara nyingi huwa baadhi ya wafanyabiashara wengi huwa wanasafirisha biashara haramu kwa kutumia njia mbali mbali ikiwemo kutia kwenye makontena ili iwe tabu kwa wale wapelelezi wanaokagua kupata kujua kilichotiwa mwisho kwenye kontena ni nini. Mara nyingi huwa wanafanya biashara hizo kwa kutaka kujipatia fedha ambazo zilizokuwa sio halali.

Vile vile kuna biashara ambayo inafanywa kwa siri kubwa tu, mtu atakuja kufanya biashara ya kuwatafuta wasichana au watoto chini ya umri wa miaka 10 na kuwachukua kwenda kuwafanyisha kazi nje ya nchi. Mhe. Spika, hili linaleta usumbufu mkubwa na uzalilishaji mkubwa sana. Mtu kama hakufahamu na mapema anamtoa mtoto wake baada ya muda akishachukuliwa hapati habari zozote, na hatimae anakuja kupata habari mtoto huyo ameshaharibika. Mhe. Spika, biashara hiyo mara nyingi ilikuwa inafanyika na hilo nalo likemewe ili wale waliokuwa wanafanya wasifanye tena au kama lipo liondoke kabisa. Pia ningemuomba Mhe. Waziri ukawa karibu na baadhi ya nchi hizi ili kuyatatua haya masuala kama yapo watu hao wahifadhiwe na kurejeshwa kwa usalama wa maisha yao.

Mhe. Spika, nakuja katika ukurasa wa 67 kifungu cha 10(i) kutakuwa na idara zaidi ya wizara itakayojulikana kama Kitengo cha Taarifa za Fedha au kwa ufupisho FIU. Mhe. Spika, kwa taratibu hizi kuwepo kitengo hiki ni vizuri sana, lakini nilichokuwa sikukiona humu ni kwamba kitengo hiki cha FIU hakikutoa taratibu zake kama mtu awe na sifa gani ili aweze kuwemo ndani ya kitengo hiki. Kwa hivyo, hilo nilitaka Mhe. Waziri akija hapa atufafanulie kwa undani zaidi.

Mhe. Spika katika hawa watakaotengwa ndani ya kitengo hiki wawe watu waadilifu, na ambao ni wakweli kwani kazi hii ni ya fedha, wasiwe watu wepesi kurubuniwa. Mhe. Spika, kama tutakuwa na watu wepesi katika kitengo hiki basi tutakuwa hatujafanya lolote, na lile lengo la kuondosha maovu haya yatakuwa yapo pale pale. Mhe. Spika, nitawaomba wale wanaohusika na kuunda kikundi hiki wawe waangalifu sana, isijekuwa tunaunda kuyaondoa yale maovu ikawa hawa wengine wanayakusanya na kuyarekebisha. Mhe. Spika, kwa hivyo mimi katika kitengo hiki naunga mkono kiundwe, lakini kiundwe kwa taratibu kama hizo ili kuepusha mambo haya yasije yakajitokeza.

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza mwanzo katika mswada huu kama tutashirikiana sote na tukiupitisha kwa kweli utatupeleka hatua nyengine serikali yetu hii. Kama inavyoeleweka muda mrefu sana wameachiwa baadhi ya wakorofi kama hawa, mtu anatulia, anajitafutia madawa yake kwa mbinu

anazozijua yeye, anajitengenezea fedha zilizokuwa sio halali. Kwa kweli sasa hivi inaonekana izidishwe kasi masuala haya yasiwepo.

Mhe. Spika, kwa kuwa tuna vyombo vyetu vya ulinzi na usalama kama vitapewa ruhusa ya kulisimamia hili na kuliangalia kwa kina naamini mambo kama haya hayatofanyika. Lakini ninachoomba cha muhimu ni kwamba watu wawe waadilifu katika kufanya kazi zao. Mhe. Spika, la muhimu ni kuwekwa mkakati wa nguvu tusiogopane, tukiogopana hatufanyi kazi. Mhe. Spika, ni kwamba mswada umeletwa ukishapitishwa watendaji wa kazi wafanye kazi hapo ndio tutafanikiwa na wananchi wetu ndio wataishi kwa raha na kujipatia mapato mazuri katika maisha yao. Mhe. Spika, suala hili mimi naliunga mkono.

Mhe. Spika, kwa kumalizia ni kwamba humo wanamopita na matatizo haya ya fedha haramu na mambo mbali mbali yanayohusiana na haya yakiwemo madawa ya kulevya sehemu hizo zinajulikana. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri na taasisi husika wakawaekea vifaa vya kutosha vya uchunguzi ili kuyazuia masuala haya au kuyaondoa kabisa. Mhe. Spika, kama bandarini au uwanja wa ndege kama kutakuwa hakuna vifaa vya kutosha vya uchunguzi askari waliokuwepo watafanya nini? Lakini tukikubali gharama ya kuwatafutia vifaa basi kuhusu suala hili halitotokea na hata sehemu zetu za bandari ikiwa tumejiandaa vizuri basi ukorofi huu utaondoka.

Mhe. Spika, kama inavyoeleweka, mtu haramia anakuwa ni mtu matatizo sana, anakuwa hajali maisha ya mtu, hajali kitu cha mtu. Kipindi cha nyuma kilichopita tumeshuhudia wenzetu Tanzania Bara majanga yaliyokuwa yametokezea, mtu baada ya kufanya biashara za kusafirisha maharage, kunde na mchele, amefikia kufanya biashara ya binadamu. Wale ndugu zetu waliopata ulemavu wa ngozi sasa hivi wamefanywa ni biashara ya kujipatia fedha. Kama tutakuwa tuko makini na sote tunaamini kiapo tulichokula basi mambo kama haya hayatofanyika.

Mhe. Spika, mimi mswada huu naipoongeza sana wizara kwa kutuletea mswada huu ili kupata kuujadili. Kwa hivyo, kwa hapa nilipofikia Mhe. Spika mimi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Amani nauunga mkono mia kwa mia. Ahsante sana.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Ame Mati Wadi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwana nimshukuru Mwenyezi Mungu kunipatia pumzi na nguvu za kuja hapa kusimama na kutoa mawazo yangu juu ya Mswada huu ambao unahusiana na Usafishaji wa Fedha Haramu pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Mwenyekiti, pili nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii mwanzo kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu ni mswada mpya kabisa, mswada huu inavyoonekana kama hatuuelewi katika mazingira ambayo tumo. Lakini kwa bahati au inaweza kuwa ndani ya mazingira ambayo tunayo ziko pesa chafu nyingi mno, lakini hatujui ipi pesa chafu ipi safi, ingekuwa kidini tungelisema ni zile pesa ambazo zinaingia ndani ya riba basi tungeseme hizo ndio pesa haramu. Lakini katika mazingira ya kawaida basi pana ufundi mkubwa kutafuta mpaka ukaelewa ipi pesa chafu.

Mhe. Mwenyekiti, ziko nchi zilizoendelea na nchi hizi tayari zimejijenga kiuchumi na pia hazina matatizo kwa wananchi wake wa pato kwa siku. Lakini katika nchi yetu hasa Tanzania ikiwemo Zanzibar bado tuna tatizo kubwa sana la kiuchumi. Kukua kwa uchumi Mhe. Mwenyekiti, ni jitihada ya uzalishaji ambayo inaweza ikapelekea taifa likajijenga. Baada ya kujijenga ndio mnaweza mkatafsiri zipi pesa chafu na zipi pesa ambazo zinafaa.

Lakini kwa nchi kama yetu ipo haja sana ya kutafakari na kuelewa na kufundisha watu kujua ipi pesa safi na ipi chafu. Lakini ukitizama kwa haraka haraka na mswada unavyokwenda, nina hofu kwamba inaweza kuwa sheria ya magendo na mambo mengine wakati wa kesi sheria hii inapofanya kazi ikawaingiza watu wao bila ya wao wenyewe kujijua kwamba wao sasa hivi wanaingia kwenye pesa chafu.

Kwa mfano, mtu amekamatwa na karafuu baharini karafuu zake zikachukuliwa, zitakapochukuliwa karafuu zile kama hakuna sheria ambayo inahusiana na magendo wazi wazi ya kutaifisha mali, basi inaonekana kwamba sheria hii inaweza kumtia mtu hatiani.

Kwa sababu katika nchi yetu ingekuwa pesa chafu ni ile pesa ambayo inatokana na madawa ya kulevya tu, basi ingekuwa si muda mkubwa kubidhiti hali hii. Lakini katika semina tulipopata mafunzo tuliambiwa pesa chafu ni zile pesa zinazotokana na miradi michafu. Sasa pesa zinazotokana na miradi

michafu ni nyingi na zina aina nyingi sana. Kwa hivyo, ipo haja ya kutafakari kwa vizuri nakuona kwamba tunakwendaje ili tusiuwe uchumi.

Mhe. Mwenyekiti, nilichotaka kukizungumza ni kwamba ndani ya nchi kama pesa zina ujazo mkubwa yaani bila ya kudhibitika basi hupelekea mfumko mkubwa sana wa bei. Sasa mfumko wa bei katika nchi nalo tatizo, maana yake wengi watakuwa wanamiliki na wengine watakuwa hawawezi kumiliki na hawana mradi au mpango ambao unaweza kuwakomboa kiuchumi.

Lakini juzi hapa nilipata neno jengine kwambana ule mtetereko mkubwa wa uchumi nao husababisha shughuli za jamii hata za serikali kutetereka. Kwa hivyo, katika mambo mawili haya tuangalie na pia Mhe. Mwenyekiti, atapokuja Mhe. Waziri anifahamishe, madhumuni hasa ya mswada huu ukitoa yale ambayo yameandikwa kule nyuma kwenye madhumuni na sababu basi tuje tupate maelezo, tumelenga nini kuona kwamba sasa hivi tupitishe sheria ya kuzuia pesa haramu? Kwa sababu isije ikawa tunazungumza lakini maana yake hatuijui vizuri.

Kwa sababu nahisi kwamba tukiacha pesa zikiingia sana husababisha mfumko wa bei (*inflation*), lakini na tukabana mpaka zikashuka sana litatokea tatizo jengine la *deflation*. Sasa ningeomba Mhe. Waziri atakapokuja anifahamishe kwa sababu yeye bilashaka mtaalamu wa uchumi.

Chengine nikitoka hapo wa jumla jumla niingie katika ukurasa wa 66. ukurasa huu kifungu cha 7 kina tafsiri ya kuzuia usafishaji wa fedha haramu. Mhe. Mwenyekiti, fedha haramu ni kweli tuwe na utaratibu wa kudhibiti fedha chafu, kwa sababu mbali na zile ambazo zunaziona lakini siku moja nakumbuka katika *briefing* tulitahadharishwa namna zinavyoingia fedha haramu, na walikuwa tayari wajanya washaingia katika nchi yetu kipindi cha kati na walishakuwa wengi.

Hawa wao walikuwa wanapata pesa haramu sana, kwa sababu mtu anakupigia simu anakwambia mimi jinni na wewe nakujua una matatizo kwa hivyo, nisikilize upate kukomboka usiwe na tatizo. Anakwambia hebu niwekee pesa shilingi milioni 10 pahala fulani halafu wewe unatajirika. Binadamu kaumbwa na tama, wengi ndani ya Baraza walipatikana kumbe ujanja ule nao ni jumla ya pesa haramu lakini bila ya sisi wenyewe kujua.

Hapa nakusudia kwamba katika zile adhabu inaweza kumkumba mtu japo humu Baraza la Wawakilishi, kwa sababu siku ile baada ya kufanya *briefing* yake Mhe. Spika, walijitokeza kama watu 10 kwamba wamepambana na mambo hayo. Sasa utakapokamatwa na pesa ile basi umejiingiza katika mtindo wa pesa chafu. Wengi wetu tulisikia wakati Spika anazungumza, na hata

mchangiaji na yeye alikosema kupatikana lakini bahati nzuri aligundua mapema.

Sasa vitendo kama hivi kama yupo mtu anakusudia kukutia hatiani basi anakutia hatiani, na bahati mbaya basi kama kwa mtu binafsi basi faini yake ni shilingi milioni 100, sasa humu ukimtoa Mwenyekiti na Mhe. Waziri anayehusika na mambo ya fedha sijui nani kama ana hakiba ya shilingi milioni mia moja. hapa nakusudia tuwe na hadhari sana ya kujua, kwamba mswada huu hatuwategi mapapa tu kama vile alivyozungumza Mhe. Rashid Seif, lakini na sisi visamaki tulio chini ya nchi mbili ya wao tunaweza tukapatikana. Hivyo nakusudia kwamba Waheshimiwa Wajumbe tuwe na tahadhari na huu mswada hatumkingii mtu, tuwe makini sana katika kuona kwamba tuutunge, tuujadili, lakini tuwe makini sana.

Mswada huu hauhusishi pesa tu, lakini hata zile rasilimali na mali chafu. Tukiingia kwenye mali chafu hee, mswada huu ukifanya kazi haraka unaweza ukawafilisi watu wengi. Lakini pia naomba sheria hii ianze pale mara tu baada ya kutiwa saini, tusije tukaitumia sheria hii kuwa mpaka wale ambao wako nyuma ya sheria hii, watafilisiwa wengi kwa sababu tunajuana, mshahara wake mdogo lakini *asset* anakubwa. Sasa hapa lazima tuone kwamba sheria hii ianze kutumika kwa pale ambapo rais atakuwa ameitia saini.

Mhe. Mwenyekiti, katika sheria hii baada ya kuondoka hapo basi niingie katika ukurasa wa 67, lakini mwenzangu Mhe. Rashid Seif aliuzungumza vizuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, kitengo cha taarifa za fedha na kamati ya kitaifa. Kamati ya kitaifa hii bahari mbaya sijaisoma muundo wake itakuwa kuwaje lakini nahisi hii kamati inaonekana kama itakuwa ya kimuungano muungano. Na zaidi inanidhihirishia kwamba itakuwa ya kimuungano baada ya tafsiri ya ukurasa wa 67 kifungu 12(1). Inaonesha wazi kwamba kuna vipengele ambavyo vinaonesha kuwa sheria hii itatumika kama ni sheria ya Jamhuri ya Muungano. Kwa sababu inagusia kwamba baada ya sheria ile kuonekana kipengele fulani kuridhiwa na Bunge, basi sheria hii inaweza ikatumika pande zote.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kunukuu ili kuweka sawa *hansard*.

Kifungu cha 12(1)

> “Masharti ya sheria iliyoelezwa chini ya kifungu 1 cha kifungu hiki ambacho ni jadweli, sheria hii italazimika kwa matumizi yake hapa Zanzibar kutokuwa yamerekebishwa moja kwa moja endapo yatafanywa marekebisho na Bunge”.

Mhe. Mwenyekiti, tunapotunga sheria ya Zanzibar basi hatuhusishi na sheria ya Bunge, lakini Mhe. Waziri atakuja kunieleza kwa sababu kuna marekebisho yamepatikana lakini mimi niliambiwa jina langu halionekani kwa hivyo, marekebisho yale sijayapata. Sasa Mhe. Waziri naomba unitakie kwa wagawaji kuwa yale marekebisho sikuyapata na natumia hii hii baadae wewe utajua wapi utanipatia.

Sheria ambayo tunaitunga sisi Zanzibar tunapendelea itumike Zanzibar, na kama sheria tunaona inafaa kwa kutumia kwa Tanzania basi sisi ndio tunaotoa ridhaa kwa sheria ile ambayo inatungwa na Bunge. Sasa sijui sheria hii kwa madhumuni gani ionekane kwamba inahusisha baina ya sisi na Bunge. Kwa hivyo, inanitia wasi wasi sheria hii inaweza kuwa ni sheria ambayo itatumika Kijamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Mwenyekiti, maeneo niliyotaka kuchangia kwa wingi tayari yamekwishachangiwa na naona kurudia rudia ni tatizo.

Chengine nilichotaka kuchangia ambacho wenzangu wameshakigusa kidogo ni ukurasa wa 85. katika ukurasa huu kifungu cha 41 maelezo yake ya pembeni yanasema, “Mtu mwenye hisa kwenye mali iliyotaifishwa anaweza kuinunua tena” katika maelezo haya sikuelewa kwa sababu taratibu za kufilisi mali ambayo chafu zitakuwa tayari zimekamilika na mali tayari imechukuliwa, lakini kinachonitia wasi wasi kwamba anaweza akainunua tena, atakapoinunua tena ndio tayari ule utaratibu ambao tunataka wa kuwa keshaisafisha ile mali au vipi. Kwa sababu tunazungumzia pesa chafu au mali ambayo ni chafu.

Sasa kifungu hiki kitakapoeleza hivyo nina wasi wasi kwamba ule utaratibu hasa wa mwenye mali kuamini kuwa pesa yake ilikuwa chafu inaweza kumuondokea hiyo imani. Kwa sababu atakuwa na nafasi ya kuinunua tena mali ile iwe yake tena. Na sijui kwa maelezo au maandiko gani itakuja kumuhalalikia ile mali ionekane kwamba sio mali ya pesa chafu, ile kupewa nafasi ya kununua tena itakuwa ndio tayari nafasi ya kusafisha imekamilika au vipi.

Tunapotunga sheria lazima tuijue, mtu kumnyang’anya mali yake halafu ukaja ukamuuzia haileti maana. Kwa hivyo, nahisi kipengele hiki kingebadilika, ikawa mtu ambaye amekamatwa na mali chafu asiruhusike kuinunua tena, hapo ingekuwa angalau panaonesha mantiki kwa sababu ananyang’anywa yeye anapewa mtu mwengine. Lakini umnyang’anye yeye halafu umruhusu anunue yeye haileti maana, itaonekana kwamba serikali ina nia ya kuwanyang’anya watu mali zao halafu iwauzie. Kwa hivyo, bora kipengele hiki kingefanyiwa mabadiliko ili kuona kwamba tunatunga sheria ambayo inaweza kumtia imani mtu.

Chengine ukurasa wa 83 sehemu ya nane ni usimamizi wa mali inayotakiwa kufilisiwa, uwezo wa kupekua na kukamata. Hapa Mhe. Mwenyekiti, inaonekana kwamba sheria iko wazi moja kwa moja. Kwa sababu mtu kumruhusu kupekua moja kwa moja bila ya taratibu ya ripoti kukamilika na alama ya mpekuzi ni kumgombanisha baina ya yeye na askari. Kwa kifungu hiki inaonekana kwamba patakuwa na mzozo baina ya mtu anayepekuliwa na kufilisiwa mali na askari.

Mhe. Waziri hapa angetengeneza utaratibu maalum ambao ungempa fursa moja kwa moja mpekuzi kuliko hivi ambavyo kuwa askari atakuwa na uwezo wa kupekuwa moja kwa moja. Kwa sababu askari nao watu, na sio askari ambao wana imani ile tunayoiamini kwa asilimia mia moja, tunajua kwamba siku hizi askari wanawaharas wageni, wanawapekuwa, wanawataka rushwa, kwa hivyo lazima tuwe na utaratibu ambao unamuepusha mtu au mtuhumiwa, au mshakiwa kusumbuka. Kwa sababu anaweza akapekuliwa hapa hana, akafika kituo chengine kwa mfano sehemu nyengine yoyote akapekuliwa tena hana, ilimradi ile shaka ikawa imesambazwa kila pahala yule mtu atahisi kwamba hafanyiwi haki anafanyiwa usumbufu.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri kifungu hiki kama kina marekebisho tutakuja kuyapata baadae. Basi ningeomba kwamba pasiwe wazi moja kwaa moja kama ilivyo katika kifungu cha 44(1), lazima tuone kwamba tunakiwekea utaratibu wa mtu kupekuliwa.

Bahati nzuri ukurasa wa 44 kifungu cha 45(1) katika maelezo ya pembeni huu unazungumza moja kwa moja hati ya upekuzi wa mali haramu. Hapa Mhe. Mwenyekiti, angalau kimeweka utaratibu wa namna ya mtu kumpekuwa ambaye anatuhumiwa na mali chafu. Mali chafu Mhe. Mwenyekiti, kwa nilivyoona tafsiri yake inaweza ikapatikana maeneo yoyote, inaweza kuwa garini, inaweza kuwa mtu anatembea kwa miguu, lakini anaweza kuwa hata katika hali ya kawaida mtu akakamatwa na mali chafu.

Lakini kwa mfano, sheria hii kama utailinganisha na sheria ambayo tumeipitisha juzi ya madawa ya kulevya, zinaweza zikawa zinakwenda pamoja kwa kuangalia kifungu hiki. Kwamba mali hata inaweza kuwa ni sehemu ya ardhi ambayo nayo uhalali wake haupo basi pia inaonekana inaweza ikaingiza, maana yake mali chafu inaweza kuwa hata ardhi kwamba kuna mtu kaichukua ardhi lakini katika kufuatiliwa hana waraka, hana chochote na anahesabu ardhi ile ni mali yake au ni sehemu yake. Lakini bahati nzuri katika ufuatiliaji ikaonekana kwamba haimiliki. Sasa nahisi Mhe. Mwenyekiti, kwa kifungu hiki sijakipitia vizuri kwamba nayo inaweza kujumuisha na yale ambayo yamekusudiwa hapa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo mimi mwenyewe binafsi baada ya kupata ufafanuzi mzuri basi pamoja na wananchi wangu tunaiunga mkono sheria hii kwa asilimia mia moja. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nakushukuru kunipa nafasi ya kuchangia mswada huu wa sheria ambao umepewa jina la Kudhibiti na Usafishaji wa Fedha Haramu na Mapato ya Uhalifu na mambo mengine yanayotokana na hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka kusema *almagendo hakku riba tartib*, hiyo ni aya imo kwenye kitabu kinachoitwa kitabu *l-wakti.* Naomba nirudie inasema, *almagendo hakku riba tartib.* Huu ndio mtiririko wa maisha ya dunia, huo ndio mtiririko wa maisha yetu ya kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, kazi ya benki ni moja tu, benki zote katika dunia hazinunui nguo, benki hainunui gari, kazi ya benki ni kununua fedha na kuuza fedha si kitu chengine. Sifa moja ya mfanyabiashara yoyote yule kununua rahisi kuuza ghali, hiyo ndio *formula* ya mfanyabiashara yoyote ikiwa benki, ikiwa mwenye duka, yeyote yule ni lazima anunue kwa bei ndogo auze kwa bei kubwa.

Zanzibar ni sehemu ya dunia nayo inapaswa kwenda kusimamia, kutekeleza mambo yale dunia inayoyataka. Mhe. Mwenyekiti sheria hii ya kusafisha fedha haramu pamoja na sheria ya madawa ya kulevya hizi ni sheria ambazo dunia nzima zipo sasa hivi, zinapigana vita na mambo hayo. Lakini hakuna njia ya mkato katika jambo hili. Nisije nikasahau naunga mkono kwanza mswada huu nisije nikasahau huko mwisho.

Mhe. Mwenyekiti, lazima tujipe wasi wasi, hawa wakubwa wa dunia wao ndio waanzilishi wa hawa na mpaka hivi sasa imekuwa vigumu wao kuweza kufanikiwa katika mambo haya. Sasa yamekuja kwetu nadhani tuwe waangalifu.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nitoe mfano, sijui kama itakuwa ni haramu au ni halali au vipi. Hivi sasa Somali kuna wale magaidi wanaoteka meli sijui kwa lugha ya kigeni wanaitaje, hawa wanaziteka nyara meli na wanadai walipwe fedha nyingi sana.

Mhe. Mwenyekiti, cha kusikitisha ni kuona kwamba wanalipwa fedha, fedha zinalipwa na wanaolipwa si malaika, wao wanasema tu tulipe shilingi milioni kadhaa na fedha hizo ziingie kwenye *account* ya Mhe. Ali Mzee, fedha hizo zinaingizwa kwenye *account* ya Mhe. Ali Mzee, sio Ali Mzee wewe Mhe. Mwenyekiti, huo mfano tu. Fedha zile zinaingizwa kwenye *account* ile.

Mimi nataka ufafanuzi, kitendo wanachokifanya wale ni kitendo cha uharamia, fedha watazozipata wale ni fedha ambazo zitakuwa haramu, lakini kampuni ya meli ambayo meli yake imetekwa nyara inakubali kulipa fedha zile ambazo wanajuwa wanampa mtu anayeeleweka. Wakubwa hao hao ndio wasimamizi wakubwa wa mambo haya, hatuoni wanachukua hatua gani dhidi ya yule ambaye amepewa zile fedha kwenye *account* yake. Sasa hili ni jambo gumu kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, si jambo rahisi ku-*prove* kwamba ni fedha ipi haramu. Bahati nzuri Mhe. Ame Mati Wadi hapa amesema hata sisi tuwe waangalifu. Nitoe mfano Mhe. Mwenyekiti, inaaminika hakuna hakika lakini, inaaminika wawekezaji wengi ambao wamekuja hapa Unguja hasa katika Sekta ya Utalii. Baadhi yao walikuwa wamo kwenye utaratibu wa kupata ule uhalali wa fedha zao, ama walikuwa wameuza unga au wamefanya mambo yoyote mengine lakini hatimaye wakaweza kuingia hapa wakawekeza kwenye mambo ya mahoteli.

Mahoteli yale yametusaidia tumepata ajira, vijana wetu wanafanya kazi, wanalipa kodi mbali mbali. Je, ikitokea mwekezaji mmoja wakaanza kuchokozana huko baadae wakafika mpaka huku wakathibitisha kwamba mwekezaji huyu ambaye ana hoteli hii chanzo cha fedha yake haikuwa fedha halali na hapa kuna mambo tumezungumza kutaifisha, kufunga, kufilisi, ikitokea hiyo hatuoni kwamba inawezekana ikaleta athari kwa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiri haramu ni vile vitendo. Kwa mfano mtu hui mwinzi mpaka ukamatwe upate hatia, ukipata hatia ndio utaitwa mwinzi, lakini kama yeye amefanya mambo yake huko amekuja kuwekeza hapa kwetu sijui kama kuna tatizo, madhali hakukamatwa. Sasa mimi nina wasi wasi nayo kidogo Mhe. Mwenyekiti. nasema tuwe waangalifu sana na jambo hili.

Jambo jengine kuna suala hili la biashara mbali mbali. Nataka niseme kwa mfano, hapa kwetu kamari ni haramu, kimazingira na maadili yetu kamari ni haramu. kamari ni sehemu ya maisha yao. Inawezekana mtu akawa amecheza kamari kule akafanikiwa akataka kutumia fedha zile kuja kuwekeza hapa kwetu. Sijui nini hukumu yake?

Kwa sababu hapa tunaikataa kamari lakini kule wanaikubali na akafanikiwa, akataka kuja kuwekeza huku tutamruhusu baada ya kubaini kwamba alipata fedha zile kwa njia hiyo ambayo sisi hapa hatuikubali.

Mhe. Mwenyekiti, hivyo akitokea mtu mmoja labda amemsaidia madawa Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, katika kipindi ambacho kuna tatizo, lakini madawa yale yameshafika hapa ikaja kugundulikana baadae kwamba yule

ambaye amesaidia madawa yale fedha alizotumia kununulia madawa yale zilikuwa ni fedha haramu. Tunafanyaje Mhe. Mwenyekiti, yale madawa sasa yatakuwa hayafai tena au Waziri anayehusika na Wizara ya Afya afanye nini?

Mhe. Mwenyekiti, wenzangu wameshazungumza hapa Mhe. Ame Mati Wadi, lakini ni kweli lazima tuangalie kama mtu amebainika mali aliyokuwanayo ni ya haramu, haikuwa ya halali imetokana na fedha chafu nasema itafilisiwa lakini anayo fursa tena ya kuinunua.

Mhe. Mwenyekiti, hili ni jambo la kuchekesha sana kwa sababu unahalalisha ile haramu, unaihalalisha hii haiwezekani tukubali tu, ama ibaki kuwa si haramu au kama inafilisiwa asiinunue tena anunue mtu mwengine. Lakini hata akinunua mtu mwengine bado inabaki chanzo chake ni ule uharamu, uharamu.

Sasa nasema hapa ndio tuwe waangalifu sana, kama ni ndoa ndio wanasema pengine labda mtu anatolewa mhalili (utaratibu) ambao haukubaliki.Lakini wengine wanakubali kwa sababu kitu ukiwa unakipenda wakati mwengine kinakuwa halali, hukipendi kinakuwa haramu. Maana yake huu uharamu na uhalali umo kwenye kupenda.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano kuna mwekezaji nina ardhi yangu nimepata m-bia katika kujenga hoteli, mimi nina ardhi, yeye ana fedha. Kuna sababu gani ya kutaka kumuuliza fedha hizi kazipata wapi? Chanzo chake nini? Mimi sihitaji hayo. Yeye anazo fedha, mimi ninayo ardhi tunaingia ubia sina haja ya kutaka kujua yote hayo. Mhe. Mwenyekiti, hivi ni vitu ambavyo tunatakiwa tuviangalie sana.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nitoe mfano mwengine, nasema haya mabenki ya dunia wanatudanganya na sisi tunadanganyika. Kwa sababu yenyewe ndio washiriki wakubwa katika kuhalalisha fedha hizi haramu.

Kwa mfano, Marehemu *Rais Mabutu Seseseko* wa Zaire alipokuwa Rais pale, aliweka fedha nyingi nje ya Zaire. Wakati wa utawala wake, fedha zile zilipokelewa na mabenki kule na zilikuwa fedha halali. Walizipokea mabenki yale tena wanamsisitiza kuweka kule hawakusema wanazifanyia biashara kwa sababu fedha ikikaa pale haikai tu wanaifanyia biashara.

Lakini ilipotokezea baada ya kuwa hayumo tena kwenye madaraka wakaona na wao hawana *advantage* nyengine. Ndipo walipoanza kugeuka sasa kwamba kuna fedha huku uliweka na fedha hizi si halali tunazirudisha. Jana zilikuwa halali mkamshawishi akazileta kwenu, mkazipokea, mkazifanyia biashara, mkapata faida, lakini baadae mnarudi mabenki haya yanasema fedha hizo si

halali. Kama hazikuwa halali, ni pale pale mwanzo walikuwa wakatae wasizipokee.

Sasa nasema jambo hili lina utata sana na ni moja ya sheria ngumu sana. Sheria hii ya fedha hizi haramu kuzifanya ziwe halali kuzisafisha ili zionekane kuwa sasa zinafaa, lakini wakati huo huo watendaji wakuu wa dunia wao ndio chanzo kikubwa cha kuhalalisha haya.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, nataka Mhe. Waziri anitoe wasi wasi. Mtu anaweza akaingia hatiani kwa namna moja au nyengine pindipo atashiriki katika kupatikana kwa fedha zile. Mhe. Mwenyekiti, sote tunaelewa mawakili. Mawakili wana wajibu wa kumtetea mtu wa aina yoyote yule. Mhalifu yeyote kwake yeye ni mtu mzuri. Watu kama hawa wanakuwa na mawakili wao kabla, anakuwa anamlipa fedha nyingi, siku anapokamatwa yeye anakuwepo pale kumtetea.

Je, ikitokezea bahati mbaya baada ya utetezi wake wakili akashindwa yule mtuhumiwa akapatikana na hatia, wakati huo huo wakili alikuwa anamtetea kwamba huyu ni mtu safi hana dhambi. Hatuoni kwamba wakili nae amechukua mchango wake mkubwa katika kujaribu kuhalalisha biashara ile ya fedha haramu. Kwa sababu kama angeshinda yule angeonekana hana dhambi na fedha zile ingekuwa ni halali kabisa, fedha safi. Sasa ni mambo ambayo yana ugumu wake.

Mhe. Mwenyekiti, nani kati yetu hapa anaweza kuzikataa fedha hizi, sio kitu rahisi. Sifikiri kama kuna mlokole akatokea miongoni mwetu, kama fedha ipo anasema anamuomba Mungu, amefanikiwa sawa kwa sababu sio rahisi.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, tuna vijana humu wanaweza kutengeneza pesa kwa muda mfupi tu, wakiwemo kina Babu Pesa, wapo na wengine, ingawa fedha hizo yeye mwenyewe anasema hawezi kuzitumia. Hebu watu kama wale tunawahukumu vipi? Yeye yupo kwenye mchezo tu kwa sababu ni fedha ambayo inakaa kwa muda mfupi baadae inapotea.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwa hakika mimi sikuwa na mchango mkubwa, lakini nataka niseme tu mswada huu wa sheria ni mgumu, si mgumu kwa maana ya kuueleza, kuutafsiri aaa, kusimamia sheria hii ni ngumu. Kwa sababu mtandao huu umeenea dunia nzima na kwa kweli una nguvu sana. Inasemekana magaidi hawa ambao ni makundi haya ya kina *Al-qaeda,* wana nguvu za kifedha ambapo sehemu kubwa ya fedha zao zinatokana na mtiririko huu. Tumekuwa tukisikia hapa na pale vitendo walivyokuwa wakivifanya hawashindwi, kwa hiyo ni jambo gumu kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema mimi sina mchango mkubwa, narudia tena kusema tu kwamba naunga mkono mswada huu, lakini tukubali kwamba utekelezaji wa sheria hii ni mgumu.Sambamba na ugumu wa kutekeleza Mswada wa Sheria ya Madawa ya Kulevya. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ambapo jambo moja tu nataka nilizungumze katika mswada huu, namna gani mswada huu unavyotilia mkazo sheria ya madawa ya kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza natoa pongezi kwa Wizara ya Fedha na Uchumi kwa kuleta mswada huu. Mswada ambao ni mzuri sana bila ya kiasi. Mswada huu una mambo mengi mazuri katika kupiga vita mambo haramu.

Kwanza umekuja wakati mzuri, Baraza la Wawakilishi limeupangia mswada huu mara tu baada ya Mswada wa Madawa ya Kulevya. Mswada wa zamani ulikuwa na matatizo ya upekuzi. Zamani Mswada wa Madawa ya Kulevya ulikuwa unahitaji umpate shahidi kama Sheha, ikawa ni tatizo. Hata upate shahidi Sheha au upate watu wengine mashahidi ndio aweze kuthibitisha kwamba haya ni madawa ya kulevya inachukua muda.

Katika mabadiliko tuliyoyafanya tukamuondosha shahidi Sheha, tukamuweka Sajenti wa Kituo. Sisi si wataalam wa Polisi, lakini tulipokwenda kwenye Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, alikuja mtaalam mmoja kutoka Polisi. Akasema mmemuondosha shahidi Sheha sasa mmeweka Sajeti wa Kituo, na Wilaya ya Mjini Sajenti wa Kituo wenyewe wapo watatu, badala ya kurahisisha upekuzi wa madawa ya kulevya, sasa mmefanya kwamba upekuzi uwe mgumu sana na ambayo sheria hii haiwezi kutekelezeka.

Lakini kwa busara ya Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo na Ustawi wa Jamii, pamoja na wewe Mhe. Mwenyekiti, ni Mjumbe, tukakubaliana tuondoshe neno kituo kwa hiyo tukabakisha sajenti, mbali suala la *ambush*. Kwa hivyo, ule mswada tukautengeneza ukawa mzuri sana ambao unaowezekana kutekelezeka.

Lakini ukifuata mswada huu unaoletwa wa Sheria ya Kudhibiti Usafishaji wa Fedha Haramu na Mapato ya Uhalifu na mambo mengineyo yanayohusiana na hayo, imezidi kuupa nguvu ule Mswada wa Madawa ya Kulevya. Kwa nini? Upekuzi wake humu umeonesha hata askari polisi wa kawaida anaweza kumpekua mtu mwenye madawa ya kulevya na anaweza kupata ithibati au kuruhusiwa akipiga simu tu anapewa ruhusa ya kumpekua mtu yeyote na kuangalia madawa ya kulevya.

Utakuta huu mswada umeipa nguvu sana bila ya kiasi na ukiusoma upekuzi, utaona anaweza kutiwa mtu hatiani mwenye madawa ya kulevya kwa kutumia mswada huu bila ya kutumia Mswada wa Madawa ya Kulevya. Ingawa Mswada wa Madawa ya Kulevya unatia nguvu pia suala la *ambush*, unaweza kupiga pahala popote *ambush* ukavunja mlango, ukaingia, ukakamata. Kwa hivyo, utakuta miswada hii miwili inafanya kuwa na nguvu kupiga vita mambo yote haramu hususan masuala ya madawa ya kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja bila ya matatizo yoyote.

Mhe. Asha Moh'd Hilal: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na mimi kupata nafasi ya kuchangia mswada huu. Mhe. Mwenyekiti, mimi nitaanza ukurasa wa 69 kifungu cha 10 (1) "Kitengo cha Upelelezi wa Taarifa za Fedha na Kamati ya Kitaifa *(Finance Investigation Unit - FIU)"*. Hapa tumeambiwa itakuwepo idara hii ya kupokea, kuchambua, kusambaza habari kutoka ndani na nje ya Zanzibar. Lakini Mhe. Mwenyekiti, hii ni kazi ngumu sana lazima tujitahidi kuifanya kwa pamoja. Si kweli kama hii idara tupu itaweza kufanikisha suala hili. Hili suala ni zito, gumu na sio la mchezo.

Mhe. Mwenyekiti, pia kwenye ukurasa huu huu pamoja na kazi za hizi idara, hapa namuomba Mhe. Waziri atuainishie. Kwa sababu hakutuainishia hii idara itakuwa na watu wangapi watakaounda hiyo idara yenyewe, na itafanya kazi gani kwa mujibu wa watu wao.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 76 sehemu ya tano kutaifisha pamoja na masharti, mtiririko, upelelezi, uchunguzi wote tayari umekamilika ikathibitika huyu mtu ndio yumo kwenye hii *issue* tunayoizungumza. Sasa huyu mtu ameshatiwa hatiani, kwa kawaida kunakuwa na rushwa kama huyu mwendesha hii shughuli kapokea rushwa, ili ile kesi ife, asiwe na hatia yule aliyetiwa hatiani. Je, huyu Mwendesha Mashtaka hukumu yake nini? Kwa sababu na yeye atakuwa pia kapokea fedha haramu. Kwa hivyo, hapa ningeomba ufafanuzi kwa Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 84 – 85 amri za kulipa faini za fedha. Tayari ameshaingizwa hatiani huyu mtu, fedha ameshalipa kuhusu hili tatizo ambalo limetokea, lakini sasa yule yule akarudia tena kufanya yale mashaka kama mwanzo. Je, huyu adhabu yake itakuwa nini? Itakuwa mara mbili zaidi kwa sababu hatukuona hapa. Maana yake wengine wataona kama ndio wamelipa kodi pale halafu atarudia tena kufanya yale yale kama mwanzo alivyofanya. Ametoleshwa faini hiyo ya milioni mia moja halafu akaendelea na mchezo wake.

Kwa sababu milioni mia moja Mhe. Mwenyekiti, kama madawa unabeba *trip* moja tu! Haya unakuja na kontena lako mwenyewe unasema la futi 20 *full* mtungi, hiyo tayari milioni mia moja mtu kishabeba, anakuja hapa anakwenda zake trip nyengine tatu kishajiunga tayari anaendelea. Je, huyu hukumu yake nini kwa sababu yeye anaona ni mchezo tu? Kafanya, kafanikiwa wenyewe wanaita *deal* kidogo imekwenda upande, anaanza tena, kama anaondokea hapa, au Nairobi halafu anaendelea na shughuli zake kama kawaida.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 108 sehemu ya tisa "Uwezo wa kukusanya taarifa". Taarifa tayari zimekusanywa lakini kwa kawaida ukusanyaji wetu wa taarifa isiwe unachukua muda mrefu. Taarifa zile zinakusanywa muda mrefu pengine kesi imepelekwa mwaka huu mpaka miaka mitano mbele haijesha. Kwa hivyo, taarifa zile zinaanza kupotea potea kila siku ushahidi haukamiliki, mashahidi wale wanachoka wanakimbia hawendi tena. Sasa kesi pale inapotea kwenye mazingira ya kutatanisha.

Je, kama hili tuko makusudi kulishughulikia, Mhe. Waziri atajipanga vipi ili hii kesi iende haraka? Kupoteza ule ushahidi ili kupata ushahidi wa haraka haraka na kutoa *suggestion* kwa vile kesi nyingi zinakimbia huku tunakotokea ushahidi wake ndio hivyo hivyo hazikufikia mwisho. Hata juzi tuliambiwa pale na Mwanasheria kwa hivyo sijui kwa hili wamejipanga vipi ili kufanikisha hizi kesi ziende haraka.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo nakushukuru na naunga mkono mswada huu mia kwa mia mimi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Magogoni.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza naomba nimshukuru *Allah Subhanahu Wataala* aliyeweza kunisimamisha katika Baraza lako tukufu na kuweza kutoa mchango mdogo utakaoonesha dhahiri hali ya kuunga mkono mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, nikianza kuzungumzia Mswada wa Sheria ya Kudhibiti Usafishaji wa Fedha Haramu na Mapato ya Uhalifu na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Kwanza nasema kwa niaba ya Mkoa wa Kusini Pemba naukubali mswada huu mia juu ya mia.

Mhe. Mwenyekiti, nianze na mchango wangu katika ukurasa wa 63. Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme kwamba mswada huu umekuja kwa wakati wake na umefika katika kutuonesha dhahiri kwamba vitendo na visa hivi vinavyofanyika vipo hapa Zanzibar tena mia juu ya mia.

Kwa mfano, ukurasa wa 63 kuna makosa yaliyoorodheshwa (a) mpaka (z). Nasema makosa haya yapo sasa hivi na kuna haja kweli ya kushughulikiwa.

Kwa mfano, nikiacha la (a) niingie katika (b) ugaidi, ikiwemo kugharamia ugaidi. Yapo haya tena makubwa. (c) usafirishaji haramu wa silaha upo. (d) kushiriki kwenye vikundi vya ugaidi. Mambo haya yapo watu wanashiriki katika vikundi vya ugaidi hawana wasi wasi. (e) usafirishaji haramu wa binadamu na kufanya magendo ya kusafirisha wahamiaji. Haya yapo yameenea. (f) udhalilishaji wa kijinsia ikiwemo makosa ya udhalilishaji wa watoto.

Mhe. Mwenyekiti, hili siku zote tunalizungumzia lakini tunaona bado watu hawajapata adabu. Kwa hivyo, mswada huu inaweza ikawa ni kigezo cha kutusaidia katika kuwa angalau wenzetu wakome juu ya mambo haya. Mhe. Mwenyekiti, kwa hapa nachukua nafasi hii kuupongeza sana mswada kwa kuliweka jambo hili.

Usafirishaji haramu wa bidhaa za wizi au bidhaa nyengine, rushwa au hongo, fedha bandia zipo. Mimi binafsi yangu siku moja nilikutana nazo nikapewa manoti siyajui nawapelekea wenye maduka wanasema aaaa bibi wewe ilikuwaje? Wizi wa silaha upo tena mkubwa, wizi mwengine pia upo wa majumbani watu wanaingiliwa kwa silaha wanawake wanatishwa wananyang'anywa vitu vyao vya dhahabu, nguo zao, mali zao na kadhalika. Kwa kweli jambo hili ni la hatari kwa nchi yetu, kwa hivyo mimi nasema naunga mkono sana mambo haya yaliyoorodheshwa hapa na nadhani zipo adhabu zao wamewekewa hapa.

Kuteka nyara, kuzuia kinyume cha sheria mateka, magendo. Magendo yapo makubwa. Ukandamizi, kughushi, uharamia, utekaji nyara, ubadhirifu wa fedha, udanganyifu na hadaa katika biashara ya soko la ndani. Watu wanachukua vipolo vyeupe vipya vizuri wanavishona wanatia Michele halafu wakatuuzia kwa bei kama tunanunua chakula kipya kumbe ndani yake kuna michele mibovu. Kwa hivyo, mimi haya yote nayapongeza na nayakubali.

Makosa makubwa ya madawa ya *nakotiki* na *saikotropiki*. Usafishaji wa fedha haramu kinyume na kifungu cha 7 cha sheria hii. Kupanga, kutenda au kusaidia kushiriki kwenye kutenda kosa lililoelezwa kwenye aya (a), (b), (c) na kifungu hiki. Kumsaidia mtu mwengine kuangamiza mapato yaliyotokana na kosa chini ya aya (a) au kujaribu kutenda kosa lililotajwa kwenye aya (a), (b) au (c). Mhe. Mwenyekiti, yote haya yapo tena makubwa kuna haja ya kushughulikiwa.

Kosa jengine lolote ambalo Waziri ataliona. Makosa yapo mengi Mhe. Waziri tusifanye muhali, kuna watu wanafanya magendo ya hali ya juu, kuna watu wanafanya ubaya kuwapiga watu wetu, kuwaumiza watu wetu bila ya kisa chochote. Leo utasikia mawio yanasema sijui nani kakamatwa huko keshachinjwa, yaani watu wanauliwa ovyo ovyo, mambo kama haya hatari!

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea naingia katika ukurasa wa 68 “Katazo la usafishaji wa fedha”. Kuna makatazo hapa yamewekwa katika mswada huu nayo ni muhimu sana. Mhe. Mwenyekiti, naomba uniruhusu niyasome.

La kwanza mtu atakuwa amefanya kosa la usafishaji wa fedha haramu akiwa anajihusisha moja kwa moja au vyenginevyo kwenye uhaulishaji unaohusisha rasilimali inayotokana na mapato ya uhalifu wakati akijua, au angeweza kufahamu, au angetakiwa kutambua kuwa rasilimali hiyo ni kutokana na mapato ya uhalifu.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani mimi makosa haya tuchukue hatua ya kuwaeleza wenzetu kabla mswada huu haujafanya kazi, tuwaeleze na mapema wasije wakaona kama tumewafanyia vibaya.

Lakini (b) anabadilisha, anahaulisha, anasafirisha rasilimali wakati akitambua angeweza kutambua, au angetakiwa kutambua kuwa rasilimali hiyo imetokana na mapato haramu na yeye akaisimamia, akaisafirisha binadamu huyo, na yeye anajua kwamba mambo haya ni haramu. Kwa mtu yeyote ambaye anashiriki katika kutenda kosa ili kuepuka adhabu za kisheria kwa vitendo vyake.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu © mtu atakuwa anakatazwa usafirishaji wa fedha haramu ikiwa anaficha au anavuruga uhalali wa asili chanzo, eneo, umiliki wa haki iliyotokana na kuwepo kwa rasilimali wakati anatambua, au angeweza kutambua kwamba rasilimali hiyo inatokana na mapato ya uhalifu.

Mhe. Mwenyekiti, makatazo haya yote mpaka (d) yanakuwa na adhabu zake. Kwa hivyo, kama sisi viongozi tunawajibika tumetoka huko kama Wawakilishi tuyachukulie hatua haya kuwafahamisha wenzetu.

Mhe. Mwenyekiti, kubwa mimi ninalotaka kulisema tusije tukapitisha sheria hii halafu tukafanya mambo ya muhali. Muhali haya jamani, lakini jambo hili fulani ndio aliyefanya mwenzangu, ndugu yangu, mhisani wangu itakuwaje mimi nimpelekee ripoti au nimshtaki. Muhali tuuondoe wenzetu wanatupitia kinyume nyume, wanataka mapato ya haraka haraka. Unaweza ukamuona mtu anakwenda benki ana mshahara wa laki moja, anakwenda kuchukua laki moja akitimiza siku mbili anapeleka shilingi milioni 20 kazipata wapi kama si za kuiba hizi, kama si za kunyang’anya kwenye serikali yetu. Nchi hii ya watu wanyonge maskini za Mungu hawana kitu, leo mtu mmoja unamkuta ana magari 20, matano ya kutembelea, mengine ya kwendea shambani.

Mhe. Mwenyekiti, watu wanaiba sana kwenye serikali yetu, hatuna haja ya kuficha kwa hilo. Ndio maana tunakatazwa mambo haya tusiyafanye, ukiyafanya sasa mswada huu ukianza kazi maana yake unafanya kwa makusudi

sheria zilizokwishapangwa inabidi zitumike usije ukasikitika ukasema aaaa naonewa, jamani mimi itakuwaje. Ukenda serikalini tena mbio kwa waziri nisaidie. Hapana kusaidiwa kwa mambo haya.

Mhe. Mwenyekiti, namalizia kwa kusema nashukuru kwa kunipa nafasi na naunga mkono tena mswada huu.

Mhe. Hasnuu Moh'd Haji: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nikaweza kuchangia Mswada huu wa Usafirishaji wa Fedha Haramu na mambo mengineyo.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba mswada huu umekuja wakati muafaka.

Mhe. Mwenyekiti, katika miswada yote tuliyopitisha na tutakayoendelea kupitisha, kwa muono wangu basi miswada miwili hii, swada mmoja huu na mmoja uliyopita punde hivi wa madawa ya kulevya ni miswada muhimu sana katika nchi yetu, iwapo itatekelezwa ipasavyo.

Nasema hivyo Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu katika nchi yetu sasa hivi masuala ya hizi fedha haramu , au miradi ya fedha haramu kwa wafanyabiashara , au kwa watu wote waliomo katika nchi hii kwa sasa hivi yamepamba moto. Katika kipindi kilichopita tulikuwa tunaishi kwa hali ya tahadhari sana, ukilinganisha na wimbi la watu walioingia hapa nchini kujitafutia fedha kwa njia ya udanganyifu.

Katika pembe zote za nchi yetu Unguja na Pemba, basi ulikuwa ukifanya kazi zako za mchana mzima basi katika kujipumzisha unaweza ukaiona simu inapigwa ukipokea simu ukakuta maneno ya ajabu ajabu. Pengine uliyokuwa hujapatapo kuyasikia na kama hukuwa muangalifu basi maneno yale yanaweza yakakuchukua na moja kwa moja ukajishtukia kama una shilingi milioni 100 au milioni 3 au hata kama una vitu vya dhahabu, basi utajikuta vitu vile vimekutoka na wala hujui vimekutokatokaje.

Mhe. Mwenyekiti, kuna rafiki yangu mmoja alikuwa amekaa nyumbani kwake, akapigiwa simu na akaambiwa kuwa wewe una matatizo jimboni kwako kuna matatizo, kwa hivyo tunakuomba njoo katika Uwanja wa Amani. Utakapofika katika Uwanja wa Amani basi zunguka nyuma ya uwanja huko utatukuta na wewe unastahiki kufanyiwa dawa. Lakini kwa alivyo mjanja na yeye akatumia mbinu, akachukua vijana wake wakenda pamoja ile safari, walipofika karibu wakasikia sauti, mtwana tunakuona, tunakuona unasogea karibu, sogea, sogea. Basi yule bwana akasogea zake mpaka mbele, kwanza aliambiwa atowe shilingi milioni 5 ili mambo yake yakae sawa. Yule bwana alichukua karatasi akazibana bana hivi akaziweka, alipofika mbele pale akaambiwa haya, angalia

hapo chini kuna kijungu cheupe basi huo mzigo uweke ndani yake. Alikwenda lakini kuna vijana ambao kawapanga pale, baada ya kufika akaweka ule mzigo na akaambiwa usitizame nyuma, ukitizama nyuma basi utaungua na gari yako. Kisha akapiga mbio akaondoka.

Mhe. Mwenyekiti, sasa wale vijana wake aliokwenda nao walikuwa wamebakia pale, wakenda wakambana yule mtu. Kitu kilichotokea pale Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba walimchukua wakampeleka polisi, na polisi wakamkamata, lakini kulikuwa na maneno yalizungumzwa pale pale polisi ikiwa na mwenyewe yupo akayasikia, matokeo yake kijana yule aliachiwa na kesi ile hapana ilipokwenda.

Kwa maana hiyo Mhe. Mwenyekiti, mswada huu kuja kwake, basi nina uhakika mambo kama hayo yaliyompata rafiki yangu huyo, basi yanaweza yakatokea kwa namna mmoja au nyengine. Kuna kitengo hiki cha upelelezaji, badala ya kupewa taarifa sasa kitakuwa kina msimamo gani? Kwa sababu hii pesa chafu ina nyanja nyingi, akikupa mtu rushwa tayari ni pesa chafu. Lakini vile vile wewe mwenye pesa chafu ni sawa sawa na mwenye kuuza unga. Mwenye kuuza unga tayari keshakamilika kuwa ni tajiri mkubwa. Sasa unapomkamata muuza unga, basi anaweza kutoa kiasi chochote cha pesa kumuhonga yule ambaye anashughulikia suala lile kama ni askari au muhusika yoyote, badala ya kupatikana ushahidi basi yule mwenye kuchukua ushahidi anaweza akapoteza ushahidi.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mswada huu tunaokwenda nao, wasi wasi wangu mkubwa yanaweza yakatokea mambo kama hayo. Sasa na hiki kitengo tulichoambiwa cha upelelezi sijui hawa watu ni wa aina gani? Ambapo Mhe. Waziri labda atatuambia, kwa sababu alituambia tu kutakuwa na kitengo. Kisije kikawekwa kitengo, kisha wakawekwa watu ambao kumbe ndio miongoni mwa wanaofanya hiyo shughuli ya mapesa haramu kama hayo.

Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba Mhe. Waziri watafutwe watu waadilifu, watu waliokuwa hawana hamu ya pesa sana, na wawekwe katika kitengo hicho, ili waweze kusaidia. Kinyume na hayo hapa patakuwa hapana muelekeo wowote. Nazungumza hivyo Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu kwenye mswada uliopita wa madawa ya kulevya, wengi tu walisema hapa, kuna watu wengi wamekamatwa na tokea ianze shughuli ya kushughulikia madawa ya kulevya mpaka leo hakuna aliyetiwa hatiani.

Kwa hivyo, na suala hili la usafishaji basi nina uhakika kama hawakuwekwa watu wazuri, basi watakamatwa watu halafu yule mtoa taarifa ndiye atakayeingia hatiani, na ataingia hatiani. Anaweza mtu kuingia hatiani kwa kupoteza roho yake kwa hao majasusi ambao tayari wako katika mtandao huu.

Unaweza kumuona mtu na masuala mabaya, ukenda kutoa taarifa, badala ya kuchukuliwa hatua basi moja kwa moja anapelekewa taarifa kwanza yule mwenye mtandao ule mchafu. Bwana mkubwa kuna taarifa, mtu fulani kaja kutoa taarifa hapa kwamba siku fulani utasafirisha fedha hizo chafu, au unasafirisha fedha pengine unampelekea mtu kwenda kufanya miradi nchi fulani na aliyetoa taarifa hiyo ni mtu fulani.

Kwa hivyo, mwenye kutoa taarifa ndiye atakayepata adhabu na yule mwenye kufanya suala lile akatokana na adhabu hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea nije katika ukurasa wa 70 sehemu ya 4, usimamizi na udhibiti wa usafirishaji wa fedha haramu. Vile vile Mhe. Mwenyekiti, kuna siku moja nilipata hadithi kwamba fedha zikitumiwa na zikimalizika muda wake huchukuliwa zikaenda kuchomwa. Kuna mtu mmoja alienda katika shughuli hiyo ya kuchomwa fedha, lakini baada ya kufika pale wanapochoma fedha akaanza kuzungumza na wenzake, wanakwenda kitengo kwa kitengo, jamani tunachoma fedha lakini kuna nyengine humu nzima. Sasa mmoja akageuka akasema tuzifanye nini? Wakamwambia tuzichaguwe zilizo nzima tuzirejeshe na zilizokuwa sio nzima basi tuzichome. Wakaendelea kuzongana pale kiasi ambacho alibakia mmoja huyu alikataa suala lile na wakafika pahala fedha ile wakaichoma.

Sasa namuomba Mhe. Waziri kwamba hawa watu wanaosimamia mambo haya basi wawe waadilifu sana, kwa sababu kama hawatakuwa waadilifu basi watapewa rushwa na kutakuwa hapana hata moja litakalokuwa.

Katika nchi yetu Mhe. Mwenyekiti, nina uhakika ukitembea katika vijiji au mitaa, basi ukiwatafuta hao wasafishaji wa hizo fedha haramu, basi mtoto wa miaka 10 anawajua. Nasema hivyo kwa sababu Mhe. Mjumbe mwenzangu aliyekaa sasa hivi kasema kwamba ukweli usiofichika, kuna watu wa aina zote, kuna wafanyakazi walioko serikalini, kuna wafanyakazi wa mahotelini, kuna madaktari, waganga wa kienyeji, kuna wafanyabiashara na wako aina kwa aina ambao tayari wako katika vitengi hivi ambavyo vimezungumzwa.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mtu utamkuta ana mahoteli, ana magesti na ana majumba kumi. Lakini mtu huyo ukizunguka nyuma ukiangalia mshahara wake, amini usiamini utakuta hamruhusu kufanya mambo yale. Lakini katika mambo yake ya vitega uchumi, pengine anamshinda waziri au anamsinda Rais. Sasa jiulize, pesa ile anaipata wapi, kama si biashara hizi zinazozungumzwa zilizokuwa haramu?

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri wasimamiaji wa kitengo hiki wawe waadilifu sana. Katika kuwatafuta watu hao hapa katika nchi yetu wapo na wanajulikana.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo machache, naunga mkono mswada huu mia juu ya mia, ahsante.

Mhe. Bihindi Hamad Khamis: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuchangia mswada huu, unaohusu usafishaji wa fedha haramu na mambo mengineyo. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mchango wangu hautakuwa mkubwa, nitakuwa na machache kwa sababu hali yangu sijaweza kuzungumza sana. Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu utakuwepo kwenye fedha haramu. Kwa kweli mimi naiomba serikali iwe na msimamo dhabiti wa kuweza kufuatilia sheria hii, kwa sababu mambo haya ni mtihani kwa sisi tuliokuwa Waislamu, kwa sababu tunatakiwa tufuate sheria za Kiislamu. Mhe. Mwenyekiti, serikali itakapofuata mkondo wake isiwe inarudi nyuma, iendelee mbele, kwa sababu mambo haya kwa kweli ni mtihani.

Mhe. Mwenyekiti, waganga wa kienyeji shughuli hizi na wao huwa wanazifanya sana na watu wengi wameshapatikana, lakini sio mimi, ni wenzetu mbali mbali. Katika bajeti iliyopita Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo alisema kwamba watafanyiwa sheria ya kuthibitishwa hawa waganga wa kienyeji, lakini na kwa upande wa masuala haya na wao wanahusika.

Mhe. Mwenyekiti, nitowe historia moja ndogo iliyotokea kwenye mkoa wangu, lakini siwezi nikataja lile eneo. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, hizi fedha haramu huwa zinatumika kwenye vijiji vyetu. Siku moja mtoto mmoja alipewa pesa ya Shs. 10,000/= kwenda kutumia dukani, basi yule mwenye duka baada ya kufanya majumuisho yake akaiona ile pesa ni haramu. Siku ya pili yule mwenye duka akamtega yule mtoto, alipokwenda siku ya pili akakamatwa yule mtoto na pesa. Kwa hivyo kwa pale walipokuwa ni maeneo ambayo kipo kituo cha polisi akaitwa polisi pale, wakaulizana. Kumbe ilikuwa ni yeye yule mtoto aliyeleta zile pesa lakini alikuwa ametumwa, kisha akapelekwa polisi yule mtoto ni mdogo sana na anahudhunisha. Kisha walikwenda wazee wake pale kuomba msamaha lakini hawakukubaliwa na mtoto yule akapelekwa mahakamani na akawekwa rumande. Lakini mpaka sasa hivi sijui kama kesi ile imeshamaliza. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli hali hii inatudhohofisha sisi pamoja na jamii nzima.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia kama nilivyosema mchango wangu utakuwa ni mdogo kutokana na hali yangu, basi naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia kwa mia, mimi pamoja na wananchi wangu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba hususan wanawake. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba: Mhe. Mwenyekiti, na mimi namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia tukapata nafasi ya kukutana hapa jioni hii, ni rehema zake *Subhanahu Wataalah* na hakuna mtu ambaye amemshawishi Mwenyezi Mungu ama amempa chochote ili tuweze kupata uhai. Wajibu wetu sisi ni kusema *Alhamdulillah Rabil Alamina.*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, naomba nichangie maneno kidogo sana, lakini nadhani yanaweza yakasaidia. Katika kifungu cha 7(2)(c), naomba kunukuu.

Kifungu cha 7(2)

"Mtu atakuwa amefanya kosa la usafishaji wa fedha haramu akiwa".

Kifungu cha 7(2)(c)

"Anaficha au anavuruga uhalali wa asili,….."

Mhe. Mwenyekiti, mimi kidogo hapa nina matatizo ya tafsiri, uhalali wa asili. Ametenda kosa, kosa sio jambo la halali, sasa neno halali hapa kidogo sijafahamu kimsingi mantiki yake imekusudiwaje, anaficha au anavuruga uhalali wa asili. Asili hii ya lile kosa au asili ya namna gani, huu uhalali hapa ndio kwangu unanipa wasi wasi kidogo. Kwa hivyo, naomba hapa kidogo kwa faida ya wananchi ambao utawafikia mswada huu basi ingefafanuliwa kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu cha 9(1) naomba kunukuu.

Kifungu cha 9(1)

"Endapo kosa chini ya masharti ya kifungu hiki limetendwa na kampuni au kundi la watu, kila mtu ambaye, wakati wa utendwaji wa kosa alikuwa"

Kifungu cha 9(1)(a)

"Mkurugenzi, Meneja, au Mwenye mamlaka ya kuongoza au Mbia'

Mhe. Mwenyekiti, sijafahamu kampuni hii wakati wa kutengeneza hizi fedha haramu zilitengenezwa kwa ma-*bandal*, baadae zikatiwa *label* za kampuni fulani. Kimsingi sijafahamu kitu gani ambacho kimezungumzwa hapa, au

kampuni hii iliruhusiwa kufanya shughuli nyengine, halafu ikatenda shughuli nyengine ya usafishaji wa fedha haramu. Kwa hivyo, na hapa kidogo nataka ufafanuzi.

Mhe. Mwenyekiti, halafu kifungu cha 11 mswada umesema kwamba naomba kunukuu,

Kifungu cha 11

> "Kutakuwa na kamati ya kitaifa ya udhibiti wa usafishaji wa fedha haramu".

Lakini Mhe. Mwenyekiti, mswada uko kimya. Jana tulipitisha Mswada wa madawa ya kulevya. Kamati zilitajwa na wajumbe wako Mhe. Mwenyekiti, wakapata hofu wakasema kamati hii ni kubwa, mawaziri wamekuwa wengi. Serikali ikasikia na mara ya pili waziri alipokuja alitoa kitu safi kabisa.

Sasa hii Mhe. Mwenyekiti, ni kitu ambacho kimejibana bana sijaelewa, inawezekana yapo maelezo ambayo sijamaliza kuyasoma. Kwani kulikuwa kuna tatizo gani kutaja hii kamati hapa ikajulikana, kuwa kamati yenyewe ni ipi? Maana hili ni jambo liko hewani na hzi zinawezekana sasa hivi ziko kwenye mitandao na serikali hii ni serikali ya uwazi. Sasa labda hakuna sheria nyengine hapa ambayo mimi sijaisoma. Kwa hivyo, ni vyema tukayaingiza ndani ya sheria hakuna tatizo kutaja hasa kwamba kamati hii itakuwa na fulani na fulani.

Mhe. Mwenyekiti, kitu chenyewe tunachokizungumza ni haramu, kwa hivyo inawezekana bila shaka kutaingia vyeo na majina ya watu hapa. Vile vile tunampa nafasi yule ambaye anawateuwa watu katika nafasi fulani kwamba kuna kitu fulani. Kwa hivyo, utakapofanya uteuzi basi ni vyema ukazingatia kwamba kuna mtu ambaye akiingia pale basi watu watasema ni kesi ya ndegere kenda kupewa nyani. Kwa hivyo ni vyema kama kuna sheria nyengine ambayo mimi sijaiona basi tungetaja wazi wazi kwamba kamati itakuwa na huyu na huyu.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 12 cha sheria hii hii kinasema kwamba naomba kunukuu,

Kifungu cha 12(1)

> "Masharti ya sheria iliyopitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa yanahusu kuwepo kwa *FIU* na kamati ya kitaifa ya kushughulikia udhibiti wa usafishaji wa fedha haramu yatatumika na kufanya kazi Zanzibar kama kwamba masharti hayo yamepitishwa chini ya sheria hii"

Mhe. Mwenyekiti, kuna kitu na kifahamu hapa kwa mbali kidogo, kuna sheria ambayo tunataka tuiunganishe hapa ambayo imepitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Au nikitafsiri neno kwamba yatatumika kwa kufanya kazi Zanzibar kana kwamba masharti hayo yamepitishwa na sheria hii. Akili yangu inaniambia kwamba kuna kifungu ambacho kimepitishwa na Bunge. Kwa maneno haya *implementation* yake sasa itatumika hapa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naona tulikuwa tuwe wazi, tutaje hicho chetu kama kwamba hatuja-*copy* kitu chochote, tutaje kabisa wazi wazi. Mhe. Mwenyekiti, halafu kuna maneno yanasema, sheria ya kuhifadhi usafishaji wa fedha haramu na mapato ya uhalifu na mambo mengine.

Tafsiri ya maneno ya kisheria huku mwanzo sikuona neno fedha haramu tafsiri yake ni nini. Inawezekana pia sijasoma vizuri. Kwa hivyo, ikiwa lipo basi Mhe. Waziri atatuambia kuwa fedha haramu iliyokusudiwa hapa ni hii na hii.

Mhe. Mwenyekiti, ipo haja pamoja na sheria hii tufikirie kutengeneza sheria nyengine ya wahujumu uchumi. Maana Mhe. Hasnuu alizungumza maneno hapa kwamba unamuona mtu, na mimi nasema kwamba mtu yuko serikalini, yupo katikati hapa, lakini utajiri alionao utashangaa! Mfano kama wewe ni Waziri katika familia ukaambiwa kuna shughuli ya kifamilia ulete Shs.300,000/=, basi unaweza ukaingia mvunguni mara 15, ukawaambia naomba mnistahamilie mpaka mwisho wa mwezi. Sasa watu wa kawaida wanaangalia huyu Waziri ama Mkuu wa Mkoa laki tatu tu! Lakini mtu mwengine ana mapato makubwa kweli kweli.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nashauri kwamba iko haja Wizara ya Fedha sasa au serikali kwa ujumla itengeneze Sheria ya Wahujumu uchumi na hapa tutawapata wote.

Kwa mfano, ukiangalia mafao ambayo tunapewa sisi Waheshimiwa Wajumbe kwa visiwa hivi ndio *high level*, lakini namna tunavyokwenda mbio mabenki kwa kukopa huko, wewe mwenyewe utachanganyikiwa. Lakini watu wa kati hawana habari tena wanayo nafasi ya kukukopesha wewe, yaani anazo gari kama 10, ukimtizama ni mfanyakazi na mswada wake umepitishwa hapa hapa. Sasa kwa kuangalia hivi na kuoneana aibu tunaweza kufika pahala taifa hili haki za watu wanyonge zitaangamia *(Makofi).*

Mhe. Spika, napenda kuishauri Wizara ya Fedha au serikali kwa jumla hivi sasa umefika wakati tutengeneze Sheria ya Wahujumu Uchumi tena tufanya *identification*. Kwa kweli itakapotungwa tu tutaona matokeo yake, nadhani imefika karibu miaka minne sasa tunapiga kelele kwa suala la mapato ya

Airport Charge ya shilingi 5,000/-. Lakini ilipofika pahala serikali ikatoa maamuzi kwamba sasa mapato yale yatoke kwenye *ticket* moja kwa moja na wala hakuna tena kutengalishwa.

Kwa hivyo, nadhani hivi sasa siri imeonekana mapato yameongezeka na wafanyakazi wale ambao waliokuwa waking'ang'ania kwenda *Airport*, basi leo ukiwaambia waende wakafanye kazi *Airport* basi hawako tayari maana msitu umetemwa pale.

Sasa kuna haja kama sisi viongozi kwamba kesho mbele ya Mwenyezi Mungu tutaulizwa tuliwachungaje wananchi ambao walikuwa hawafiki katika chombo hiki, tuliwasaidia vipi, kwa sababu tunaona.

Mhe. Mwenyekiti, kuna Hadith ya Mtume Muhammad (*S.A.W*) inayofahamishwa kwamba, unatakiwa uzuie kosa kwa maeneo matatu, moja kupigana nalo hasa lisitendeke hilo kosa, pili kulikemea na ikiwa huwezi kukemea basi uchukie. Lakini Mtume Muhammad (*S.A.W)* anatuambia kuwa kuchukia ndani ya nafsi ni udhaifu.

Je, nani ambaye ameambiwa achukie, sio sisi tuliopo hapa kwa sababu sisi sote ni *answerable* na wala sio watu wa kuchukia, kwamba jambo hili ni baya sana tulichukie tu. Kwa kweli sisi ni watu wa kupigana nalo, yaani ni lile kundi la mwanzo. Kwa sababu hiki ndicho chombo cha kutunga taratibu za kuendesha nchi, kwa kuwa sisi ndio *answerable* moja kwa moja.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo na mimi naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja *(Makofi).*

Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Mswada huu wa Sheria ya Kudhibiti Usafishaji wa Fedha Haramu na Mapato ya Uhalifu na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya yote naunga na wenzangu waliotangulia katika kuchangia mswada huu kwa michango yao mizuri, yenye lengo moja tu nalo ni kupiga vita tatizo hili hapa nchini kwetu.

Kabla sijaendelea na mchango wangu naomba uniruhusu nimpongeze kwa dhati kabisa Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa makusudi kuamua kutayarisha mswada huu, ambao kwa kweli ni muhimu sana kwa nchi yetu

katika masuala mbali mbali ya pamoja na uhalifu na mambo ya uchumi na kadhalika *(Makofi)*.

Kwa hivyo, mimi mwenyewe binafsi pamoja na wananchi wa Jimbo la Kikwajuni naunga mkono mswada huu *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, wenzangu wameshachangia sana pengine mchango wangu zaidi utakuwa katika masuala ya kumshauri Mhe. Waziri kwa masuala yafuatayo.

Kwanza kama nilivyochangia mswada uliopita wa madawa ya kulevya, kwa kweli tatizo hili hasa lilikuwa jipya katika nchi zetu hizi, tulikuwa tukikisikia sikia tu, lakini sasa jinsi ulimwengu mdogo sana na sisi ni sehemu ya ulimwengu. Kwa hivyo, kuna haja kubwa na sisi kujipanga kwa ajili ya kukabiliana na tatizo hili.

Mhe. Mwenyekiti, kuna haja ya makusudi na napenda kumshauri Mhe. Waziri kuchukua hatua pamoja na mswada huu mzuri. Lakini mswada huu unahitaji utekelezaji, ili yale malengo yalikusudiwe yaweze kufikiwa.

Sasa utekelezaji wa sheria hii kwa jumla sheria zote basi sio Wizara ya Fedha na Uchumi peke yao, kwa sababu wizara ni watu kidogo sana. Kwa hivyo, kuna haja ya kila mmoja na hasa katika mswada kama huu kila mwananchi wa visiwa vyetu hivi na wala sio wananchi yeyote, lakini kila kiongozi, jamii ya polisi, yaani vyombo vya ulinzi na usalama, majaji, mahakimu, kwa sababu hawa wote kwa njia moja au nyengine watakutana na sheria hii.

Kwa maana hiyo, sote kwa pamoja lazima tujidhatiti na tushirikiane kwa ajili ya kukabiliana na matatizo haya. Vile vile wafanyabiashara, *NGO's* na kadhalika.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mantiki hiyo kuna haja ili mswada huu au sheria hii iweze kutekelezeka vizuri, basi ni vyema na wenzangu waliotangulia kusema nadhani kwenye mswada wa sheria ipo kwamba kuundwa au kuazishwa kwa Kitengo Maalum kitakachoshughulikia kazi hii ya utekelezaji wa mswada huu.

Kwa hivyo, tunaposema kitengo Mhe. Waziri atufahamu nini tumekusudia, kama alivyosema Mhe. Mjumbe aliyemaliza hivi karibuni, yaani pawe na watu ambao ni waadilifu na tujitahidi kutafuta watu waadilifu. Vile vile isitoshe wapewe mafunzo ya hali ya juu kabisa yanayohusika na kupambana na matatizo haya, baadaye wapewe majukumu na waweze kutekeleza wajibu wao.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani kuna haja pamoja na majukumu yao, lakini ni vizuri kila baada ya muda fulani na humu kwenye sheria haimo, yaani kila baada ya miezi mitatu au 6 ama mwaka watakavyoona inafaa kuweza kufanya tathmini, hicho chombo kitakachohusika kufanya tathmini ya kuweza kutizama utekelezaji uko vipi. Kwa mfano, umefikia asilimia ngapi au umetelekezwa vipi kwa asilimia ngapi, ili pale pazuri tuweze kufanya vizuri zaidi na kwenye kasoro basi ziweze kuchukuliwa hatua kwa ajili ya mafanikio mazuri *(Makofi)*.

Nikiendelea na mchango wangu nilisema kuhusu suala la kuelimishwa wananchi. Kwa kweli hili bila ya shaka kupitia vyombo mbali mbali vikiwemo pamoja na televisheni na redio, vijarida, matoleo tofauti na hata mabango.

Kwa hivyo, kwa makusudi kabisa vyombo vya habari televisheni na redio kama desturi yao, ambavyo tunavipongeza kwa sababu wanasaidia sana miaka hii ya karibuni wanajitahidi sana kuelemisha wananchi katika masuala mbali mbali yanahusiana na utekelezaji wa sheria. Kwa maana hiyo, vyombo vya habari viwe mstari wa mbele katika kuelimisha au kutoa taaluma kwa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, katika watu ambao nilitaja hapo mwanzo, ambao nilisema wapewe elimu tosha kuhusu utekelezaji wa mswada huu na hasa ilivyokuwa katika nchi zetu ni mpya. Kwa hivyo, pamoja na vyombo nilivyovitaja na mabenki pia, kwa sababu benki imetajwa sana kuhusu fedha za haramu au chafu ndiko zinakopitia sana. Kwa maana hiyo, hawa na wao wawe waadilifu na wapatiwe mafunzo mbali ya elimu yao ya kibenki pia wapewe elimu ya benki kuhusu masuala haya.

Kwa hivyo, kama nilivyosema Mhe. Mwenyekiti kwamba mengi yamechangiwa na wala sina haja ya kurejea isipokuwa kwa hayo machache. Nadhani nirejee tena kumpongeza Mhe. Waziri kwa matayarisho ya mswada huu, ambao umekuja kwa wakati.

Baada ya hayo, mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kikwajuni tunaunga mkono kwa asilimia mia moja mswada huu *(Makofi)*.

Mhe. Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru nami kunipa nafasi hii kwa ajili ya kuchangia Mswada huu wa Sheria ya Kudhibiti Usafishaji wa Fedha Haramu na Mapato ya Uhalifu na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na timu yake kwa kuandaa mswada uliotimia kama huu, ambao leo hii upo kwenye Baraza letu hili tukufu na tunapata nafasi ya kuchangia.

Mhe. Mwenyekiti, sitokuwa na mengi sana kwa sababu nimepata maelezo mazuri si chini ya mara mbili au tatu kuhusu mswada. Kwa kweli tumeupitia mswada huu kwenye Baraza la Mapinduzi na tulifanyiwa Semina Maalum kwenye Ukumbi wa Benki Kuu. Kutokana na hali hiyo labda nitakuwa na kichwa cha nanga kwamba nije hapa na kuuliza sijafahamu hiki na kile. Isipokuwa nichangie kwa ajili ya kutilia mkazo pale ambapo ninaona, ili watu wengine wapate kuona umuhimu.

Kwa kweli mswada huu ni muhimu sana na sisi nchi yetu hii ya Zanzibar hatuwezi kuwa tofauti sana na wenzetu, kwa sababu matatizo haya yanayowakuwa hata mataifa makubwa na sisi pia tunayo. Kwa hivyo, kwa kutembea basi lazima twende sambamba kama wanavyokwenda wenzetu, kwa hiyo sisi kwa vile ni wamoja au wasimamiaji ama tunaweza kusema *advocate* wakubwa wa utawala bora na sheria katika kuendesha nchi yetu.

Kwa maana hiyo, ni muhimu kuwa na mswada kama huu, ambao kwa kiasi fulani kukosekana kwake kunafanya kama haki haitendeki. Kwa mfano, inatokezea wale wajanja au wakorofi wachache wakawafanya wenzao wabole (wajinga), kwa sababu wanapata fedha nyingi, wanakuwa na nyumba pamoja na mambo ya starehe mengi na wale wavuja jasho wanaendelea kuumia kwa ujanja au uhalifu unaofanywa na hawa wachache.

Mhe. Mwenyekiti, kuwepo kwa sheria hii kutasaidia kusafisha uhalali na usawa na kuweka nchi kutazamika. Kwa sababu mambo mengi ya kiharamu yanapozidi, basi ndiyo haya yaliyomkumba Nabii Nuhu na Jahazi lake wakazama moja kwa moja, kutokana na mambo ya uharamu yamezidi. Kwa hivyo, Mwenyezi Mungu atusaidie na hizi sheria zetu tuweze kuwadhibiti hawa wanaofanya huo uharamia na nchi yetu iweze kwenda tukiwa kwenye utaratibu mzuri *(Makofi)*.

Kwa kweli kuna matatizo mengi Mhe. Mwenyekiti, ambayo yanasababisha uupatikanaji wa hizi fedha zinazoitwa fedha chafu na mengine yanadhoofisha na kuhatarisha nchi pamoja na kuweka maisha ya watu katika hali ambayo si ya salama, wahka, hamkani mtawalia na watu hatutambuani. Sasa kabla nchi yetu haijafika huko sheria hii itatusaidia kuwadhibiti hawa wakorofi wachache.

Mhe. Mwenyekiti, tumesikia sana na kuona athari zinazotokana na madawa ya kulevya kama vile watu wanaharibikiwa, watu wote wanakuwa na macho laini, yaani hajulikani mwanamke wala mwanamme kwa sababu ya madawa ya kulevya.

Kutokana na hali hii watu inabidi watie *grille*, mtu chumbani anatia mlango wa *grille* kwa ajili ya kumzuia mwanawe anayetumia madawa ya kulevya asiingie

na kuweza kumuibia, yaani chumba cha kulala (*bedroom*). Mhe. Mwenyekiti, tumepata kuona wapi bedroom ikatiwa mlango wa *grille*.

Sasa hayo yote na mengine pamoja na kupoteza maisha ya vijana, matatizo mengi katika familia yanayosababishwa. Halafu mtu mmoja yeye anakuwa tajiri kwa kuuza madawa haya kulevya, anajenga makasri, anakuwa na *swimming pool*, kila siku anakwenda Taiwan na kurudi. Kwa hivyo, hapa taifa na damu changa ambayo tunategemea kwa ajili ya kuendeleza hili taifa inapotea kama moshi *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, kuwepo kwa sheria hii nafikiri itasaidia, ingawaje ni kazi nzito. Kwa sababu hawa wenzetu wenyewe ambao *Super Power South America* mpaka hivi sasa suala hili ni zito sana, yaani Marekani pamoja na uwezo wake wote, lakini madawa yanapitishwa pale na tafrani moja kwa moja na wala watu hawatambuani.

Kwa hivyo, tutakapodhibiti hizi fedha pengine tutaweza kushinda hivi vita vya kupambana na matumizi na uletaji wa madawa ya kulevya. Kwa sababu wengi wameona kwamba hii ndio njia rahisi ya kujipatia utajiri wa haraka haraka.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la kushangaza ni kwamba mtu hata haelekei, kwa sababu hii ni kama lana kabisa, yaani mtu utakayemuona ukiambiwa amefanya suala hili wewe mwenyewe utashangaa. Kwa kweli yeye anao ubinafsi anajali yeye tu, kwa ajili ya kupata utajiri wa haraka haraka, yaani astarehe pamoja na kujenga makasri yake na wengine awafisidi.

Sasa fedha hizi tumeona namna gani. kwanza kuhusiana na madawa ya kulevya biashara hii inapokea vizuri ni pale ambapo mauaji yanakuwa nje, yaani wazi wazi. Kwa mfano, mtu amekaa basi anakuja mtu na *pistol* yake na kukupiga bila ya wasi wasi na wala tusiende huko.

Mhe. Mwenyekiti, sisi tunataka kuishi, kwa sababu huko tunakokwenda hatukujui na wala hajaja mtu kutuambia kwamba kule Akhera kuko hivi na vile. Kwa hivyo, ni vyema kukaa duniani kwa usalama na haya mambo ambayo yatasababisha mtu kufa bila ya kutaka katika nchi hii yasiwepo *(Makofi)*.

Kwa kweli tumeona fedha hizi kwa baadhi ya watu wengine japo kuwa hapa kwetu bado, lakini wanazitumia kwa kufanyia ugaidi na wala si jambo zuri. Kwa sababu kama unalipwa fedha kwa ajili ya kufanya jambo ambalo liko kinyume na sheria, basi ni suala lenye kuleta matatizo na linaweza kuiparaganya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, tunataka nchi yetu ya Zanzibar iendelee kuwa *Paradise* ya dunia. Sasa kama tunataka hivyo, basi lazima sheria hii tuiunge mkono ili iweze kufanyakazi vizuri na kuweza kuisha katika hali ya amani, utulivu, maelewano pamoja na mshikamano.

Kwa kweli kuna mambo yanayosababishwa katika kutafuta fedha hizi za haramu na tumeelezwa mara nyingi, kwamba kunafanywa magendo ya kusafirisha watu. Nadhani jambo hili la kusafirisha watu ni sawa na Biashara ya Utumwa, suala hili tayari limeshaondolewa hapa duniani kwa siku nyingi kwa kuona kwamba unamnyima mtu haki yake.

Mhe. Mwenyekiti, kweli ujitayarishe kwa sababu ya kwenda kumuuza mtu, tunajua kwamba dhiki zipo, lakini wakidhibitiwa watu hawa wanaofanya biashara hizi, basi uhuru wa mtu utakuwepo na kila mtu ataishi kama anavyotaka. Kwa hivyo, kama kweli ni mfanyabiashara basi atatafuta biashara nyengine yenye mwelekeo na sio biashara ya kuuza watu. Pengine mfanyabiashara huyu amefanya hivyo kwa kuona kwamba biashara hiyo inampatia fedha nyingi.

Lakini wakati unadhalilisha utu wa mtu na kukiuka Haki za Binadamu, basi ni bora tuendelee na biashara zetu ndogo ndogo ambazo tunafanya na wala hazitupelekei kupata jukumu hapa duniani na kesho Akhera. Kwa sababu kama wewe unamchukua mwenzako na kumuuza, kwa kweli hapa umekiuka Haki za Binadamu.

Kwa hivyo, ni vyema umpe nafasi yake na magendo kama haya hayafai na kuwepo kwa sheria hii itasaidia, maana tusiseme kwamba hapa yanafanyika lakini si sana. Mhe. Mwenyekiti, jambo lolote lile ambalo mtu mwengine anafanya basi na mwengine atafanya, kwa sababu binadam huwezi kumtabiria. Kwa kweli maovu ni rahisi sana mtu kuiga kuliko yale yenye maana sana.

Mhe. Mwenyekiti, nimewahi kusikia wakati fulani wenye fedha zao wana mtindo, wanatoka huko nchi kwao na kwenda nchi yengine kama vile Paris na kwenda kutafuta watoto wadogo kwa ajili ya kuwadhalilisha. Sasa kama huko yanafanyika, basi na hapa yanaweza kufanyika.

Kwa hivyo, kupitia sheria hii tunaweza kutunza watoto wetu kutokana na huko kudhalilishwa na hawa wapuuzi wawili au watatu ambao wanazo fedha, kwa sababu kama kudhalilisha kuzuri, kwa nini wasidhalishe kule kwao. Isipokuwa wanajua kwamba jambo hili ni baya na kwa sababu hizi nchi zetu za ulimwengu wa tatu zina matatizo kidogo kwa matatizo ya uchumi mtu anaweza kuhadaika kwa fedha mbili tatu na kwenda kufanya mambo mabaya au machafu.

Kwa kweli hawa wanachukulia zaidi kwamba watoto hawa ni wadogo, kwa hiyo ukiwadanganya kidogo unaweza kuwadhalilisha kwa kujiridhisha yeye nafsi yake kutokana na wazimu wake. Kwa maana hiyo, sheria hii itatusaidia sana.

Vile vile kuna tatizo jengine ambalo linatokana na hawa wenye fedha nyingi kutumia fedha zao kwa ajili ya kufanikiwa lile wanalolitaka, yaani wanafanya hongo. Mhe. Mwenyekiti, jambo hili la hongo si zuri na wala halifai hata kidogo na rushwa halikadhalika ni mbaya sana. Kwa sababu hawa wanakuwa na fedha nyingi sana ndio maana wanaweza kutumia hizi fedha, ili wapate urahisi wa kufanya au kusababisha matatizo hayo yanayotokana na fedha za haramu.

Mhe. Mwenyekiti, mengi yamesemwa ambayo ni mazito tena ni mabaya, kwa kweli yote haya yameelezwa vizuri sana katika mswada huu. Kwa hivyo, ni jukumu letu ni kuhakikisha kwamba tunayafahamu vizuri na tunaunga mkono *(Makofi)*.

Nikiendelea na mchango wangu nizungumzie kuhusu matatizo ya madawa ya kulevya kwa kweli haya nitarudia mara mbili au tatu. Kwa sababu ni mambo ambayo yako wazi na kila mtu anajua kuwa hayafai, mtu mwenye kujishughulisha anafahamu kwamba fedha nyingi zinapatikana kutokana na mambo haya.

Lakini pamoja na hayo, wale waliokuwa *blocked* na wakapelekwa na kuadhibiwa naweza kusema hakuna, yaani bado kabisa. Mhe. Mwenyekiti, kuwepo kwa sheria hii nadhani kutaweze kuwaibua na kuwaeka hadharani wale ambao wanahatarisha jamii nzima kwa kufanya vitendo hivi.

Mhe. Mwenyekiti, katika waraka huu kimetajwa hiki Kitengo cha *FIU*. Kwa kweli nakiunga mkono sana kitengo hiki pamoja na kazi zake zitakazofanya. Isipokuwa ningeomba tutafute namna zaidi ya kukiongezea uadilifu kwa watendaji wake, yaani wawe na uwezo zaidi, ambao wataifanyakazi hii kwa dhati kabisa *(Makofi)*.

Vile vile kuhusu sehemu ya mtoaji siri nataka nijiridhishe tu. Hivi huyu mtoaji siri atadhibitiwa vipi yule aliyekwenda na kutoa taarifa, kwa sababu tabia ya siku hizi *day by day* inaonesha kwamba kuweka siri ni tatizo kubwa sana, yaani jambo ambalo linasemwa kwamba hili ni siri, basi wewe hujafika mlango mwengine tayari limeshasikika au tayari lishazungumzwa. Kwa hivyo, mtu kama huyu ambaye atatoa siri ya watu wanaoshughulika na masuala ya kujipatia fedha haramu.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho anieleze kuhusu huyu mtu atakayetoa taarifa, sasa hii siri itadhibitiwa kiasi au namna gani, hivyo kutafanywa nini cha ziada ambao hawa wanaopelekewa hii siri au taarifa watakuwa wadhibiti. Kutokana na hali isijeikawa kama ile hadith ya Mfalme na jamaa zake mtu alishindwa kustahamili mpaka kuchimba shimo na kusema kwenye shimo kwamba Mfalme amemuona anayo masikio marefu.

Kwa sababu hapa kama hapatakuwa na udhibiti madhubuti, basi taarifa hizi hazitapatikana kwa kuhofia usalama wa watu wenyewe. Kwa maana hiyo, jambo na msingi ni kuhimizana tu, kwa lengo la kuliokoa taifa letu hili, taifa ambalo limezongwa na mazonge ya hawa wanaoshughulika na fedha haramu, basi lazima tuwe wazalendo na tutoe hizi taarifa.

Vile vile utaratibu ufanyike kwa hao watakaopelekewa taarifa wahakikishe kwamba wanadhibiti. Kwa hiyo, pindipo wakienda kinyume na kudhibiti hiyo siri, nadhani kuwe na namna nyengine kwa upande wao ya kuwadhibiti na kuwazuia, vyengine tutakuwa tunafanyakazi bure.

Kwa sababu tunapitisha sheria hapa na halafu watu wanatoa taarifa, badala ya yule uliyemtolea taarifa baadaye unakuja kuchukuliwa hatua wewe kinyume na utaratibu. Mhe. Mwenyekiti, nafikiri sheria yetu haitofanyakazi vizuri. Kwa hivyo, lazima tuunganishe nguvu zetu na tuhakikishe kwamba fedha haramu ni haramu kweli na wala hatutaki watu watuharibie maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kama walivyosema waliotangulia kwamba mengi yameshaelezwa sana na Waheshimiwa Wajumbe kuhusiana na vile wanavyoguswa na matatizo yanayotokana na hawa wanaoshughulika na masuala ya fedha haramu.

Katika waraka huu kuna kipengele cha upekuzi. Mhe. Mwenyekiti, nafikiri kwa sababu hawa wanafanya kazi nzito na wanaweza kukuta hicho wanachokitafuta. Kwa hivyo, mimi nilikuwa nafikiri pengine ili kuwafanya wasiwe na ushawishi hawa wapekuzi basi wapewe *allowance* maalum ili waweze kuwajibika katika kazi hiyo, vyenginevyo wataona nao ndio nafasi ya kufanya fedha haramu kiurahisi. Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu huko nyuma ninavyokumbuka *experience* yangu naomba niseme ili kuonesha namna gani litavyojitokeza tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa Mtaa wa Nyati Dar es Salaam *opposite* na nyumba yetu kulikuwa kunauzwa gongo, dirisha letu ndio tunakuwa tunaiona hiyo nyumba ya kina Moses. Mhe. Mwenyekiti, tunaona watu wanafungua kwenye karo kuna msingi wanatia gongo, sisi tunajiuliza kuna nini leo? Kumbe kina Moses wameshakuja kuambiwa na askari kwamba baada ya muda sio

mrefu utakuja upelelezi hapa. Basi Mhe. Mwenyekiti, wale kina Moses maisha yote wanauza gongo hawajakamatwa mpaka leo.

Kwa hivyo, na hii itakuwa shughuli kubwa ya upekuzi, sasa tunawajenga vipi na nilikuwa nashauri kwamba wapewe *allowance* ya kutosha kama vile wanavyopewa mishahara mizuri watu wa *TRA* na wengine kutokana na kwenda kukadiria kodi na kadhalika. Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo na hawa watunzwe kwa njia ambayo hawatashawishika ili waweze kufanya hiyo kazi na wale waliotoa ile ripoti isiwe kazi ya bure.

Mhe. Mwenyekiti, waraka huu ni mzito na kweli inabidi ifanywe tafakari ya kweli kweli ili tufahamu na tujue mbinu ya kusaidia. Kwa sababu matatizo ambayo yatadhibitiwa na sheria hii na kila mmoja wetu yatamgusa, maana yake sasa hivi huwezi kusema mimi sihusiki kwa sababu mtoto wangu hali unga. Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba haya mambo huwezi kujua kwani haya mambo ni sawa sawa na maradhi mengine yoyote ya kuambukiza na yanaweza yakamuambukia mtu wakati wowote awe amepanga au hakupanga. Kwa hivyo, ni muhimu kwamba pamoja na kuwa tutaupitisha lakini iwe tunaupitia mara kwa mara na tunajaribu kwa kadri ya uwezo wetu kuona kwamba tunadhibiti matatizo haya ambayo ni janga la taifa.

Mhe. Mwenyekiti, pia fedha haramu ni adui wa haki kwa sababu mwengine anavuja jasho anahangaika na mwengine anajifanya yuko makini anachukua unga wake anatuumizia watoto wetu halafu anakuwa milionea. Mhe. Mwenyekiti, tungesema tutamshitakia Mwenyezi Mungu lakini hatujui huko kama kweli huyu bwana atapata tabu au ataendelea kwenda kukaa kwenye bustani nzuri. Lakini lazima huyu hapa hapa tumpate tumuadhibu kwa mujibu wa sheria na kwa mujibu wa makosa yake. Mhe. Mwenyekiti, ni lazima tuunganishe nguvu zetu pamoja, naona humu kwenye mswada huu mambo mengi yanataka ushirikiano na askari polisi.

Mhe. Mwenyekiti, sijui tutafikiria vipi kuongeza utaalamu wao hawa ndugu zetu ili kazi waweze kuifanya kwa ufanisi zaidi. Kazi ya kupambana na tatizo hili ni kubwa sana lazima tugharamike sana kuwalipa watakaofanya kazi hizi, tugharamike sana kuwapatia mafunzo, tugharamike sana sisi kwa uzalendo wetu kutoa ripoti ili kukabiliana na tatizo hili. Sisi tunapata tatizo kubwa sana katika jamii yetu naomba kurudia tena ili nitilie mkazo nioneshe namna gani hawa watu wanatumia pesa. Mhe. Mwenyekiti, mara nyingi utasikia mzee amempa pipi mtoto huyo anakuwa hana pesa sana je, wale wanaopata pesa nyingi kwa hapa kwetu si watatuharibia sana watoto wetu.

Kwa hivyo, sheria hii kwa upande wetu sisi inabidi tunaiunga mkono sana kwa sababu itaweza kuwadhibiti hawa mafirauni wawili watatu ambao wanajifanya

wao hawana akili timamu na kufanya vitendo ambavyo vimekatazwa na Mwenyezi Mungu lakini bado watu wanafanya. Kwa hivyo, tutakapokuwa nah ii sheria itatusaidia sana.

Mhe. Mwenyekiti, kwa dhati kabisa mimi niseme na nitoe wito kwa wenzangu na wananchi wote wa nchi yetu tukazane na tuhakikishe kwamba sheria hii inafanya kazi sawa sawa. Baada ya hayo naunga mkono mswada huu, ahsante sana.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, ahsante nakushukuru kunipatia nafasi hii na mimi kusema machache kuhusiana na mambo haya ya fedha haramu. Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikiangalia hiki kifungu cha pili ambacho kinatoa ufafanuzi kuna baadhi ya maneno yametumika katika huu mswada. Nilikuwa natafuta maana halisi ya fedha haramu, kwa sababu mara nyengine zinaitwa fedha chafu. Kwa hivyo, nilikuwa naangalia fedha haramu maana yake nini na fedha chafu maana nini. Kwa kweli nimepekuwa sana lakini sikuona pahali palipoelezwa kwa urefu nini maana ya fedha haramu. Kuna sehemu moja nimekuta pameandika mali chafu na hiyo ikatafsiriwa kwa u ufupi sana kwamba mali chafu kuhusiana na kosa kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nahisi huu mswada moja katika kasoro zake haukueleza kwa urefu mpaka watu wakajua hizi fedha haramu maana yake nini, na hii imetoa fursa ambayo hata mimi nataka niitumie sasa hivi kutoa tafsiri mtu anavyoona yeye tu kwa saabu kila mtu amesema vyake hapa. Wengine wamesema ni fedha inayopatikana kwa ufisadi, wengine wamesema ni fedha inayopatikana kwa kuuza madawa ya kulevya, hii inawezekana yakauzwa nje ya nchi halafu mtu akaleta fedha zake hapa. Pia inawezekana yakaja kuuzwa hapa na mwenye mali akawa ndio mradi wake.

Mhe. Mwenyekiti, wengine wamesema fedha inayopatikana kwa wizi wa fedha za umma, wako wakorofi huchotachota fedha, fedha inayopatikana kwa rushwa wengine wamesema hapa pia nazo ni fedha chafu, kuna wizi unaotokea katika benki zetu, wengine wamesema fedha za kamari nazo ni fedha chafu. Mhe. Mwenyekiti, kuna mmoja mzee wangu na rafiki yangu kweli kweli yeye amesema hata kama umepewa fedha ile inayoitwa *sitting allowance* hapa kama hukusema kitu nayo ni fedha chafu. Lakini baadae akajikosoa mwenyewe kumbe ni *speaking allowance*.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa uhuru wa kutafsiri mtu atakavyo upo na hii imetokana na kwamba mswada huu hauku-*specify* maana halisi ya fedha haramu. Mhe. Mwenyekiti, na mimi nataka niongeze moja hata kama mtu anapora kitu cha mtu mishahara yote atakayopata itakuwa ni fedha haramu. Siku nyengine huitumia hiyo na bahati mbaya sana zamani ukenda Hijja kwa

pesa haramu basi ulikuwa hurudi unakufa huko huko. Lakini watu wanatumia fedha haramu kwenda Hijja sijui kama Hijja hiyo inapokelewa kweli au haipokelewi.

Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba fedha haramu zipo nyingi katika nchi mwanangu hapa alikuwa akisema nchi hii inakaribiwa na balaa jinsi fedha haramu zilivyojaa na watu wanazitumia. Mhe. Mwenyekiti, unaweza kumkuta mtu ana nyumba zaidi ya 20, amesema Mhe. Ame Mati Wadi hapa ukiangalia chanzo cha maisha yake ni kwamba hana uwezo wa kujenga nyumba 20, hizo nazo ni fedha haramu. Nafikiri mheshimiwa tuna wakati mzuri wakujirekebisha ili haya yanayoepukika tuyaepuke. Mhe. Mwenyekiti, baada ya dibaji hiyo nataka niende katika ukurasa wa 66 kifungu cha 4.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa huo kuna tafsiri ya neno kutoroka, ukiangalia hicho kifungu kina (a), (b) na (c) sasa hicho kifungu cha (c) (i) kinasema: “mtu atafariki kabla amri ya kumkamata haijatelezwa”.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sio mwanasheria lakini kufariki sio hiari ya mtu, kufariki ni majaaliwa na maandishi ya Mwenyezi Mungu. Kwa hivyo, Mahakama imetoa amri kwamba mtu akamatwe lakini kama mtu amekufa kabla hayakamatwa huyu nae kama atahesabiwa ametoroka mimi sidhani kama itakuwa tunamfanyia haki. Mhe. Mwenyekiti, nafikiri Mhe. Waziri kifungu hiki kinafaa kiondolewe kwani mtu kufa sio kutoroka.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 68 kifungu cha 7 kuna tafsiri ya Kuzuia usafishaji wa Fedha Haramu, *heading* yake inaitwa Katazo la Usafishaji wa Fedha Haramu, *marginal note* imeandika tafsiri ya Kuzuia Usafirishaji wa Fedha Haramu. Ukisoma kifungu cha 2 kinasema hivi naomba nikinukuu. “Mtu atakuwa amefanya kosa la usafirishaji wa fedha haramu akiwa: (a) anajihusisha, moja au vyenginevyo, kwenye uhaulishaji unaohusisha rasilimali inayotokana na mapato ya uhalifu wakati akijua au angeweza kufahamu au angetakiwa kutambua kuwa rasilimali hiyo ni kutokana na mapato ya uhalifu”. Mhe. Mwenyekiti, hii wakati akijua mimi sina tatizo nayo kwa sababu kama umeshajua jambo halafu ukalifanya basi hapo unakuwa ndani ya hatia moja kwa moja.

Mhe. Mwenyekiti, hii iko sahihi, lakini hii ya pili na ya tatu kama angeweza kufahamu lakini alikuwa hajafahamu na hii ya tatu mbaya zaidi angetakiwa kutambua. Mimi nafikiri hii lugha sio sahihi. Kwa mfano, mimi nikutane na Mhe. Hamza Hassan Juma Dar es Salaam anipe pesa mkoba mzima aniambie bwana hizi pesa zichukue ukifika Unguja mpe Mhe. Haji Omar Kheir. Mimi kwa nia njema nazichukua zile pesa, sijui kama pesa zile Mhe. Hamza

amezipata vipi, maana ningejua kama huyu anarudi kuuza unga sawa basi sitozichukua, lakini sasa mimi sijui nimebeba mkoba nikaja nao huku.

Kwa hivyo, sheria inasema kwamba angeweza kufahamu, ningeweza kufahamu vipi na mimi sijui, au angetakiwa atambue mimi nina miujiza gani yakutakiwa nitambue, sio sahihi sheria kutungwa hivyo. Mimi nafikiri ingelibakishwa hiyo hiyo alikuwa akijua na bahati mbaya imejirudia katika kifungu cha 2 (b), (c) na (d) inaonekana haikuandikwa kwa makosa mimi nashauri hii itolewe kwa sababu tutawaonea watu bure. Mhe. Mwenyekiti, nafikiri mantiki iliyokusudia itahamika.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka katika kifungu hicho niende kwenye ukurasa wa 69 kifungu cha 10 (1) (2). Mhe. Mwenyekiti, pale panaanzishwa taasisi inaitwa FIU ndivyo ilivyoandikwa katika hili dokezo. Huko mbele katika kifungu cha 12 yameelezwa masharti ya sheria iliyopitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano yanayohusu kuwepo kwa FIU na kamati ya kitaifa ya kushughulikia udhibiti wa usafishaji wa fedha haramu yatatumika na kufanya kazi Zanzibar kama kwamba masharti hayo yamepitishwa chini ya sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa katiba sio mtaalamu sana mimi wa katiba lakini tulikuwa tukiogelea kuna sheria inatungwa na Bunge la Jamhuri kama hiyo sheria ya Muungano maana yake inatakiwa ije Barazani na Baraza liikubali, hiyo inakuwa ni sheria ya Muungano moja kwa moja. Kuna sheria inatungwa na Baraza la Wawakilishi peke yake hiyo inakuwa ni sheria ya Zanzibar. Lakini sheria hii ukiiangalia ni sheria inayotungwa na Baraza la Wawakilishi sasa hivi, lakini kuna vifungu vimetungwa na Bunge la Jamhuri na hapa vimetajwa.

Mhe. Mwenyekiti, hii ni sheria gani maana yake hii ni sheria ya mtiririko wa tatu sijui tuite sheria chotara maana yake sio ya Jamhuri wala sio ya Zanzibar. Mimi mawazo yangu nilikuwa nahisi kama tuliona haya ni mazuri kuyatia ilikuwa tuyatie tu bila ya kutaja kama imetungwa na Bunge au vyenginevyo. Sasa sheria hii tutaitafsiri vipi ni ya Zanzibar au ya Muungano. Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa nahisi tungelitafuta lugha nzuri ya kuitaja, lakini tusitaje kama imetungwa na Bunge, tuseme tumeitunga sisi hapa.

Mhe. Mwenyekiti, ukisoma kifungu cha 12 (2) anasema: “masharti ya sheria hii yaliyoelezwa chini ya kifungu cha 1 cha kifungu hiki ambacho jadweli ya sheria hii yatalazimika kwa matumizi yake hapa Zanzibar, kutokuwa yamerekebishwa moja kwa moja endapo yatafanywa marekebisho na Bunge”. Inaonekana hii sheria sio yetu hapa wanaweza wakaifanyia marekebisho kule Bungeni, wakiifanyia kule sisi hapa tufanye nini maana yake tuje tena na sisi tubadilishe sheria hii au tuitumie kama ilivyo na kama tutaitumia kama ilivyo

kule kama imetokezea matatizo ndio tutaifanyia marekebisho. Mhe. Mwenyekiti, hili linatokea kwa sababu ya kuchukua jambo si letu. Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nahisiti ni bora tutunge kifungu kama hiki lakini tusiseme kwamba kimetungwa Bungeni tukisema hivyo itakuwa sio chetu na ndio tunapata matatizo huku.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 45 (7) ukurasa wa 93 naomba nikinukuu:

"Askari polisi anayefanya kazi kwa mujibu wa hati iliotolewa chini ya kifungu hiki, anaweza kumtaka mtu na kuvua nguo zote alizovaa ikiwa kuvua nguo hizo ni muhimu kwa kumfanyia upekuzi mtu huyo".

Mhe. Mwenyekiti, hii ni hatari kubwa vyenginevyo hili neno kumtaka isiwe kumtaka likibadilishwa pengine wamekusudia kumkamata, lakini kama ni kumtaka mtu halafu akamvua nguo zote hiyo ni hatari kubwa. Mimi nilikuwa naomba sana kwanza huo uwezo askari polisi asipewe na hii lugha inabadilishwe maana atakuja kutumia fursa anayoitaka na atasema kwamba sheria imeniruhusu. Kwa hivyo, ukiangalia kama ni makosa ya kiuandishi kwanza yarekebishwe halafu mantiki nzima yakuwa ya kumvua nguo zake zote hivyo ni kwenda kinyume na haki za binadamu. Mhe. Mwenyekiti, hizi ni taratibu wanazotumia Chuo cha Mafunzo na hivyo wanazitumia isivyo halali kwa sababu huwezi kumdhalilisha mtu hii ni dunia ya sayansi na teknolojia hatushindwi kuweka kitu chochote ambacho kinaonesha kilicho ndani ya mwili wa mtu.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 94 kifungu cha 47 (b) upekuzi wa dharura katika kifungu kidogo (b) kinasema: "Upekuzi, au ukamataji unafanyika katika mazingira ya muhimu na haraka kwa kuelewa na kutathmini umuhimu wa upekuzi au ukamataji bila ya idhini au amri ya Mahakama iliyotolewa kwa mujibu wa sheria hii".

Mhe. Mwenyekiti, tukizungumza pale ambapo pana nia njema si tatizo kifungu kubakia maana inawezekana kuna mazingira ambayo ukikosea basi ushahidi unaweza ukapotea. Lakini Mhe. Mwenyekiti bahati mbaya sana ni kwamba hapa Zanzibar tumetawaliwa na siasa chafu na mambo mengi tunayoyafanya hatuyafanyi kwa nia njema. Inawezekana ikawa anatafutwa Abdalla Juma atiwe hatiani kikatumika hiki kifungu akakamatwa bila ya amri ya Mahakama. Mimi nilikuwa nataka nishauri hiki kifungu kiondolewe, lakini kina mambo mawili ikiwa itatekelezwa kwa nia njema hakuna tatizo, lakini kama mtu atatumia mambo yake anayoyataka mwenyewe anaweza akamuweka mtu pahali pabaya bila ya hatia. Hapa mimi sina cha kushauri lakini nina wasi wasi nacho sana na kama siogopi kwamba kuna nia njema ningesema kifutwe, lakini pengine kuna nia njema.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba humo ambapo nimetoa maoni yangu na wasi wasi wangu namuomba sana Mhe. Waziri afanye marekebisho ili kuondoa tatizo katika huu mswada. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nakushukuru na mimi kunipa nafasi nitoe mchango katika mswada huu unaohusiana na fedha chafu pamoja na fedha haramu.

Mhe. Mwenyekiti, mswada nimeupokea kwa niaba ya wananchi walionileta hapa na naomba ruhusa niendelee kuchangia. Mhe. Mwenyekiti, nikianza katika ukurasa wa 57 kifungu cha 1 Jina fupi na kuanza kutumika.

Mhe. Mwenyekiti, jina fupi linaambiwa sheria hii itajulikana kama Sheria ya Kudhibiti Usafishaji wa Fedha Haramu na Mapato ya Uhalifu ya 2009 na itaanza kutumika mara tu baada ya kutiwa saini na raisi.

Baraza letu kwa mujibu wa kanuni tunatumia lugha ya Kiswahili, na ni vyema mambo yote ambayo tunayatumia Mswahili anapoliona neno ambalo tunalitumia kila mmoja aweze kulifahamu. Sasa mimi katika sheria hii waziri kutumia neno ‘usafishaji’ kwa sababu hii sheria hatutotumia sisi tu, napendekeza tutumie neno ‘uhalalishaji’. Sheria hii ya kudhibiti uhalalishaji wa fedha haramu. Kwa sababu kwanza huku kuna haramu, sasa kinyume cha neno haramu ni uhalali. Kwa hivyo, sheria hii inadhibiti kuhalalisha kitu kilichokuwa haramu hivyo mimi naona ndio itakuwa ni sawa.

Mhe. Mwenyekiti, sheria hii baada ya kutiwa saini kifungu kinasema itatumika na masuala ya fedha haya siku hizi si ya pekeetu, kwanza tuna wenzetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania benki kuu yetu moja, *currency* yetu moja. lakini pia tumepiga hatua, hivi sasa tuko kwenye soko moja nchi za Afrika Mashariki na Kati. Lakini uhusiano huo haukuishia hapo umekwenda mpaka katika Jumuiya ya *SADC*. Je, hivi sasa hao wenzetu sheria kama hizi wameshaanza kutunga? Au sisi tu ndio tuna kiherehere ndio wa mwanzo?

Kwa sababu jambo la kuchupia nalo lina matatizo yake, tusiwe na hamu kwenda Geneva huko au *IMF* tumeona hili jambo lipo tukasema sisi tuwe wa mwanzo. Je, wenzetu hili wamelipokea vipi na wamefanya utafiti wa aina gani? Je, wameshalitungia sheria?.

Mhe. Mwenyekiti, nimuulize Mhe. Waziri, hili jambo kwanza yeye kalipokea kutoka wapi? Na kwa kiasi gani amelifanyia utafiti ili na sisi litusaidie? Namuomba kama kalifanyia utafiti ni wa kiasi gani na vipi utatusaidia? Kwa hivyo, mimi kuhusiana na kifungu hicho bado nilikuwa nina wazo hilo.

Lakini kwenye kifungu hicho hicho cha mwanzo suala hili ni pana mno na hata mswada wenyewe ni mrefu. Baada ya sheria hii kuipitisha takriban serikali peke yake haitoweza kukamilisha kutumika kwa sheria hii, tunao wadau wengine. Mhe. Waziri ningependa akatusaidia, kwa kiasi gani wadau wameshirikishwa kama vile watu wa benki, wafanyabiashara na wawekezaji. Kwa sababu hili ni eneo pana na wao pia watahitaji wasaidie katika utekelezaji wa sheria hii. Waziri amewashirikisha katika kuandaa mambo haya? Mchango wao umo humu? Hii itatupa moyo sisi kuona kiasi gani tutapotengeneza sheria hii na wao wajue kuwa tutashirikiana kufanya kazi kwa pamoja.

Kazi iliyotajwa kwenye mswada huu ni kubwa mno, kwa serikali peke yake haitofua dafu ikiwa fedha au bidhaa chafu. Kwa hivyo, hilo ni eneo jengine.

Lakini nikija katika kifungu cha 2(1) penye tafsiri kuna eneo pale linazungumza idhini, maana yake ni idhini iliyotolewa na waziri kimaandishi kwa madhumuni. Sasa hapa katika tafsiri nimesoma mote sijaona waziri gani huyu ataetoa idhini, ni waziri tu imekuwa kimya ambapo neno hilo limerejewa tena hata katika kifungu cha 14(a). Sasa ni Waziri wa Mambo ya Ndani, Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ, Waziri wa Fedha, waziri yupi. Basi kama kasahau ninamkumbusha Mhe.Waziri katika tafsiri kwa mujibu wa sheria hii atwambie waziri gani ataekuwa na mamlaka ya kutoa idhini hiyo. Mimi humu sikuona nimesoma sana au sijui nimekosea atakuja kunieleza. Lakini mimi nimeona mapungufu huyu waziri kamtaja tu kimya hakumtia na baba yake.

Mhe. Mwenyekiti, benki zimetajwa hapa Benki Kuu ya Tanzania au benki kama ambavyo imeelezwa na benki na taasisi za fedha. Hapa pia sijafahamu Mhe. Waziri naomba anieleze. Je, hii Benki yetu ya Watu wa Zanzibar inaingia kwenye fungu gani? La (a) au inaingia kwenye fungu la (b), *Western Union, FBME, Barclays,* hizi nazo zinaingia kwenye kifungu kipi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo nije katika suala zima la fedha haramu. Mimi nimshukuru Mhe. Waziri kwa sababu alijua mswada huu una *terminology* nyingi na ngumu akatupa mafunzo ya semina ya siku moja. Namshukuru sana kidogo imesaidia angalau tunaweza kusema maneno mawili matatu, la si hivyo tungepiga makofi tu hapa halafu tukamwambia tumekubali kwa kuitikia ndio, ndio, halafu tukiulizwa hatufahamu kitu.

Sasa kwa mujibu wa taaluma tuliyopewa pale hizi fedha haramu na ndio nikauliza je hawa wenzetu vipi? Ina tafsiri mbali mbali na itategemea nchi baada ya nchi. Kwa sababu fedha haramu itategemea na sheria ya nchi inasemaje. Mimi nina mashaka juu ya hili, ndio nilipouliza katika huu mtandao wetu wa nchi tulizoungana.

Kwa mfano, hapa sisi pombe ni haramu na polisi kila siku wanakwenda kwa jamaa zangu Manzese wanakamata madebe wanayatupa na kila kitu, kwa sababu ni haramu. Je, fedha ambazo wanazipata ziko vipi?

Lakini pia tumeelezwa hapa kwenye mambo ya madawa ya kulevya peke yake ni haramu, lakini nchi nyengine za Kiislamu hata zile riba ni haramu. Benki zote za nchi za Kiarabu wakiweka pesa laki moja basi laki moja, na wao wanaweka pesa zao nchi za nje hivyo hivyo hasa benki za mashariki ya mbali za Ulaya huko. Nchi za Kiarabu hupendwa kwenda kuweka pesa kule kwa sababu ile faida yao wanachukua wao kwa vile wao wenyewe hawachukui riba.

Mhe. Mwenyekiti, sisi katika mtazamo wetu nahisi sheria hii inakuja kwetu, niulize sisi Zanzibar juu ya hii riba tuna mtazamo gani. Nimeona humu kwamba ukiweka pesa au ukikopa shilingi laki moja baada ya mwaka mmoja una shilingi laki moja na ishirini na tano, kwenye *SACCOS* pale tumeambiwa shilingi mia moja na asilimia kumi na mbili ulipe. Nimuulize Mhe. Waziri hii nayo haitokuwa pesa chafu kwa mujibu wa somo tulilolizungumza au sikufahamu?

Mhe. Mwenyekiti, hata kwenye mali za magendo kwa mujibu wa sheria hii zinaambiwa ni pesa chafu. Lakini tuseme hapa hapa kwetu nchini kuna magendo ya karafuu yanakamatwa lakini sijasikia hata siku moja serikali inateketeza mali ile, badala yake huuzwa na watu wanagawana. Ni fedha chafu lakini tunagawana. Je, tunatunga sheria hii si tutakuja kujikomoa sisi wenyewe?

Magendo ni moja ya fedha chafu lakini mimi sijasikia kuteketezwa au kuchomwa moto badala yake zinapelekwa *ZSTC* zinagawiwa, aliyekamata sijui asilimia ngapi, na nani sijui, hizi jamani si pesa chafu? Tunajitia kisu wenyewe tutajipiga kwa bakora yetu kama mwimbaji wa Tumbe. Tuziachie basi sasa hivi au tukizikamata tujue tunaziangamiza, si bora tukamwachia mwenyewe aende nazo huko, kwa sababu tukizikamata ni mali ya magendo kwa mujibu wa sheria hii, sasa si tunajitia kitanzi wenyewe kwa wenyewe. Sijui hapa Mhe. Waziri amepaona au vipi.

Mhe. Mwenyekiti, kuna biashara za Maalbino wanaouzwa viungo vile vile, kwanza ni kitendo kibaya lakini pia ni haramu. Sisi hapa kwetu Mwenyezi Mungu katupishia mbali biashara hii haijaingia na tunamuomba atukinge nayo. Lakini pia tunapiga vita mambo haya ya vileo.

Mhe. Mwenyekiti, lazima nimpongeze sana Waziri Hanuni pamoja na Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo. Kwanza kupiga marufuku misaada yote inayotokana na kampuni za vileo kusaidia michezo yetu, kwa sababu ingekuwa ndio tunaivaa hasa ile pesa chafu.

Mhe. Naibu Waziri Kiongozi hongera sana na uendelee, pesa zile kweli ni chafu na umejua mapema kabla ya sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa utaendelea kesho.

(Saa 1:45 Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 27/10/09 saa 3:00 asubuhi)